**10 APRILI, 2026**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Sita – Tarehe 10 Aprili, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD - KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA):**

(i) Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2025 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Central Government for the Financial Year 2024/2025)*;

(ii) Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2025 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Local Government Authorities for the Financial Year 2024/2025)*;

(iii) Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2025 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Development Projects for the Financial Year 2024/2025)*;

(iv) Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mashirika ya Umma kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2025 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of the Public Authorities and Other Bodies for the Financial Year 2024/2025)*;

(v) Ripoti ya Jumla ya Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalum kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Machi, 2025 *(The Annual General Report on the Performance and Specialised Audits for the Period Ending 30th March, 2025)*;

(vi) Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2025 *(Annual General Report on the Audit of Information Systems for the Financial Year 2024/2025)*;

(vii) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Upatikanaji wa Dawa Muhimu katika Vituo vya Afya vya Umma *(Performance Audit Report on the Availability of Essential Medicines in the Public Health Facilities)*;

(viii) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utoaji wa Huduma za Afya ya Mfumo wa Fahamu na Neva kwa Watoto. *(Performance Audit Report on the Provision of Neurological Healthcare Services to Children)*;

(ix) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utoaji wa Huduma za Afya ya Uzazi. *(Performance Audit Report on the Provision of Maternal Healthcare Services)*;

(x) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Taratibu za Ushirikishwaji wa Wazawa katika Sekta ya Madini

*(Performance Audit Report on the Management of Local Content Provisions in the Mining Industry)*;

(xi) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utoaji wa Chakula, Makazi na Huduma za Malezi kwa Wazee. *(Performance Audit Report on the Provision of Social Care Services for Elderly People);*

(xii) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Huduma za Usafiri Mjini katika Majiji Makubwa. *(Performance Audit Report on the Efficiency of Urban Transport Services in Major Cities)*;

(xiii) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utoaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria kwa Wananchi Wasiojiweza *(Performance Audit Report on the Accessibility of Legal Aid Services to the Indigent Population)*;

(xiv) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Nishati Jadidifu *(Performance Audit Report on the Management of Renewable Energy Projects);*

(xv) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Udhibiti wa Huduma za Maji *(Performance Audit Report on the Regulation of Water Utilities in Tanzania);*

(xvi) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Fedha za Ruzuku za Uendeshaji wa Shule za Umma *(Performance Audit Report on the Management of Capitation Grants in Public Schools);*

(xvii) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Ukusanyaji wa Mapato yasiyo ya Kodi *(Performance Audit Report on the Management of Non-tax Revenue Collection)*;

(xviii) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Uendeshaji wa Mizani *(Performance Audit Report on the Management of Weighbridge Operations to Control Overloaded Vehicles)*;

(xix) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Mchakato wa Upangaji wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Barabara *(Performance Audit Report on the Management of the Planning Process for the Road Infrastructure Improvement)*;

(xx) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Hifadhi ya Nafaka za Kimkakati *(Performance Audit Report on the Management of Strategic Grain Reserve to Guarantee Food Security)*;

(xxi) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utekelezaji wa Hatua za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi nchini Tanzania *(Performance Audit Report on the Implementation of Climate Change Adaptation Actions in Tanzania)*;

(xxii) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Shughuli za Urejeshaji Misitu *(Performance Audit Report on the Management of Reforestation Activities in the Country)*;

(xxiii) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utoaji wa Huduma za Fidia kwa Wafanyakazi *(Performance Audit Report on the Provision of Workers' Compensation Services)*;

(xxiv) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Ukaguzi wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi *(Performance Audit Report on the Management of Occupational Safety and Health Inspections at Workplaces)*; na

(xxv) Taarifa ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi za Ufanisi zilizofanyika na kuwasilishwa Bungeni Mwaka 2022 *(Follow Up Report on the Implementation of Performance Audits Recommendations Issued and Tabled to the Parliament in 2022)*.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ufafanuzi wa Spika kuhusu utaratibu wa kushughulikia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)*.

Waheshimiwa Wabunge, mapema leo hii ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imewekwa Mezani kwa

utaratibu uliowekwa chini ya masharti ya Kanuni ya 46 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2025. Utaratibu huu utazingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura 418 ambazo kwa pamoja zinajenga msingi wa uwajibikaji kwa matumizi ya fedha za umma.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa hii ni ripoti ya kwanza ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilishwa katika Bunge la Kumi na Tatu, ninachukua fursa hii kufafanua baadhi ya mambo ya msingi kuhusu utaratibu wa kuifanyia kazi ipasavyo.

Waheshimiwa Wabunge, ufafanuzi huu ni pamoja na kuonyesha mabadiliko makuu ya utaratibu utakaotumika katika Bunge la Kumi na Tatu kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji. Mabadiliko haya yenye msingi katika Kanuni za Bunge ni kama ifuatavyo: -

Utaratibu wa Kamati za kusimamia matumizi ya fedha za umma kufanyia kazi ripoti hizo kwa kuwahoji Maafisa Masuuli, unaanza baada ya ripoti hiyo kuwekwa Mezani Bungeni hadi Mkutano wa Bunge wa Oktoba – Novemba. *(Makofi)*

Jambo hili sasa limepewa nguvu ya kikanuni chini ya Kanuni ya 139(16) ya Kanuni za Bunge. Lengo lake ni kutoa fursa ya uchambuzi wa kina kwa hoja za kiukaguzi kwa mtazamo wa Kibunge na kwa niaba ya wananchi. Ili kuweza kubainisha hatua za uwajibikaji, Kamati zinapendekeza hatua hizo kwa kuzingatia dosari zilizobainishwa na *CAG*. Kazi ya *CAG* ni kubainisha dosari, wajibu wa Bunge ni kubaini hatua za moja kwa moja na kiuwajibikaji. *(Makofi)*

Bunge la Kumi na Tati litatekeleza wajibu wake inavyostahili. Baada ya kujadili taarifa za Kamati na mapendekezo yake yanayotokana na taarifa za *CAG*, Bunge litatoa maazimio. Masharti ya utaratibu wa kuyafanyia kazi maazimio haya, yameainishwa katika Kanuni 139(16). Lengo lake ni kuzitendea haki ripoti za *CAG* kwa mujibu wa Kanuni za Bunge na kuweka nguvu ya kikanuni kwenye mjadala wa ripoti hizo muhimu katika uwajibikaji.

Utaratibu wa Bunge kufuatilia hatua za uwajibikaji na utekelezaji kwa ujumla, umebainishwa kikanuni. Utaratibu huo unahusisha Serikali kuripoti Bungeni hatua zilizofikia katika utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu ripoti za *CAG* kwa mujibu wa Kanuni ya 139(17).

Aidha, masharti hayo yanazitaka Kamati zinazosimamia matumizi ya fedha za umma *(PAC na LAAC)* kuripoti maoni yake kuhusu hatua za utekelezaji kwa maazimio hayo. Lengo lake ni kuhakikisha kuwa kuna uwajibikaji wa kweli unaoleta matokeo, yaani *effective and enforceable accountability*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa ujumla utaratibu utakaotumika katika Bunge la Kumi na Tatu utajumuisha utaratibu mpya ambao unaitaka Serikali kuripoti hatua za utekelezaji Bungeni wakati wa Mkutano wa Bunge wa Januari – Februari na *PAC* na *LAAC* kufuatilia utekelezaji na kutoa maoni yake kwenye Mkutano wa Januari – Februari. *(Makofi)*

Masharti hayo yanalenga kufanikisha desturi ya uwajibikaji ambapo kwanza, makosa yanabainishwa; pili, yanachambuliwa; na tatu, utekelezaji wake unathibitishwa na Bunge ili kuanza mchakato wa uwajibikaji. Hatua hizo zinajenga mzunguko wa uwajibikaji, yaani *accountability loop* na ni muhimu kuzingatiwa na Bunge la Kumi na Tatu, kwani ndiyo moyo wa uwajibikaji na zinasaidia kuweka uwajibikaji wenye matokeo *(result-oriented accountability)*.

Waheshimiwa wabunge, utaratibu niliousema, ndiyo viwango vya Mabunge ya Nchi Wanachama Jumuiya ya Madola. Kwa mfano, katika Bunge la Uingereza, mzunguko wa uwajibikaji *(accountability loop)* unahusisha *PAC* kutumia taarifa za Wizara ya Fedha kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, yaani *Treasurer Minutes*. Kwa upande wa India, Bunge linakamilisha mzunguko wa uwajibikaji kwa *PAC* kutumia taarifa rasmi za hatua za utekelezaji, yaani *Action Taken Note*.

Waheshimiwa Wabunge, ufafanuzi wangu ni nyongeza kwenye namna *PAC* na *LAAC* zilivyojipanga kuwezesha uwajibikaji kwenye matumizi ya fedha za umma. Muda

utakaotumiwa na Kamati hizi utakuwa kwa ajili ya kuchambua kwa kina, kukusanya ushahidi, kulinda haki ya asili ya Maafisa Masuuli kusikilizwa *(natural justice)* na kutafsiri hoja za *CAG* katika uwajibikaji. Kufanya hivyo ni jambo linaloendana na viwango vya juu vya Bunge kwenye Nchi za Jumuiya ya Madola.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya yote niliyoeleza, msisitizo wangu ni kuwa *PAC* na *LAAC* zinalisaidia Bunge kusimamia na kufanikisha uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma ili matokeo yake yajitokeze kwenye kutimiza lengo kuu la Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 8(1)(b) ya Katiba ambayo ni ustawi wa wananchi ambapo kwa kweli linajikita kwenye kuwapa wananchi tabasamu.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Ofisi ya Waziri Mkuu, maswali. Mheshimiwa Yahya Ally Mhata.

Na. 46.

**Ujenzi wa Nyumba za Watumishi wa Afya - Nanyumbu**

**MHE. YAHYA A. MHATA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba za watumishi wa afya ngazi ya kata katika Jimbo la Nanyumbu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Jimbo la Nanyumbu, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na nyumba za watumishi katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Kutokana na ongezeko la ujenzi wa vituo vipya, kumepelekea mahitaji makubwa ya nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya tathmini ya mahitaji ya nyumba za watumishi ambapo jumla ya nyumba 25,690 zinahitajika kote nchini, nyumba za watumishi zilizopo ni takribani 7,696 sawa na 30%. Aidha, katika Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu takwimu zinaonesha kunahitajika nyumba 147 na zilizopo ni 43 sawa na 29%.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu imetenga jumla ya shilingi milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba mbili za watumishi kwenye Kituo cha Afya Mnanje na Zahanati ya Kazamoyo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhata.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Wilaya ya Nanyumbu ina kata 19 ambazo hazina nyumba za watumishi na ina vituo vya afya viwili ambavyo havina nyumba za watumishi. Kwa majibu haya ya Serikali kwamba imetengwa shilingi milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba mbili maana yake itatumia miaka 10 kukamilisha nyumba hizi.

Mheshimiwa Spika, swali; sasa hivi tunajadili bajeti ya Waziri Mkuu, ningependa kufahamu ni kiasi gani kimetengwa kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kwa ajili ya kukabiliana na changamoto hizi za ukosefu wa nyumba za watumishi wa afya katika jimbo langu?

Mheshimiwa Spika, pili, je, Serikali haioni kwamba wakati umefika sasa tuka-*engage private sector* au tukashirikiana na taasisi (*National Housing*, *TBA*, JKT) ili kuongeza nguvu katika ujenzi

wa nyumba hizo za watumishi kule vijijini ili kukabiliana na changamoto hii? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Ally Yahya kwa kuwasemea watumishi wa Jimbo la Nanyumbu na kule waliko watumishi wanafarijika sana kuona Mheshimiwa Mbunge anawapambania.

Mheshimiwa Spika, Serikali tumeshafanya tathmini, tuna hitaji la nyumba hizi zaidi ya 25,000, lakini tayari tumeshafanya mpango wa utafutaji wa fedha zaidi ya shilingi bilioni 241 kwa ajili ya kuanza kujenga ujenzi angalau wa nyumba 2,000 zile *three in one* kwenye maeneo yenye uhitaji mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili Mheshimiwa Mbunge kwanza ni ushauri wa Kamati ya TAMISEMI, tulipata ushauri lakini pia tumepata mwongozo kutoka Wizara ya Mipango na Uwekezaji kwamba sasa tufanye *engagement* kwa *private sector* ili nao waweze kuingia kuwekeza katika ujenzi wa nyumba za watumishi, iwe ni chachu ya kuwafanya watumishi waweze kutulia katika maeneo yao ya kazi na isiwe chanzo cha uhamisho kwa sababu ya nyumba.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Masama kina nyumba kadhaa za watumishi, lakini zimekuwa chakavu sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati nyumba hizi za watumishi ili ziweze kutumika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika,

naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha Mafuwe kwamba tayari tuna mpango pale TAMISEMI Wizarani kwa ajili ya ukarabati wa nyumba chakavu za watumishi ili ziweze kuendana na ubora na hali ya kisasa. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mafuwe kwamba katika vipaumbele, na nyumba hizi chakavu zipo katika kipaumbele chetu na tutaweza kuzirekebisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amethibitisha kwamba kukosekana kwa makazi katika baadhi ya maeneo kumesababisha watumishi kuhama na kutokutulia kwenye maeneo hayo, je, Serikali iko tayari kuweka kipaumbele katika maeneo ya vijijini, maeneo ya pembeni katika ujenzi wa nyumba hizo za watumishi ili kuweka utulivu huko?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, hakika kwenye tathmini ambayo tuliifanya kama Wizara, hizi nyumba 2,000 tunazielekeza hasa maeneo ya pembezoni yenye uhitaji mkubwa zaidi ambapo unakuta tumejenga kituo chetu cha afya, lakini hata nyumba za kupanga watumishi hazipo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutaelekeza katika maeneo hayo zaidi ili kuweza kuwa-*hold* watumishi wetu na waweze kutumikia jamii yetu kule vijijini na maeneo ya pembezoni zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nawanda.

**MHE. DKT. YAHYA E. NAWANDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Vituo vipya vya Afya vya Mkwedu, Malatu pamoja na Nandwahi hakuna kabisa nyumba za watumishi. Je, nini mpango wa Serikali kuhakikisha vituo hivyo vinapata nyumba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, Serikali inakiri ongezeko la vituo vipya vya afya na zahanati, kwa hiyo kuna upungufu wa nyumba hizo. Tutaelekeza kwenye hizi nyumba 2,000 za *three in one* angalau ziweze kufikia katika yale maeneo ambayo tumejenga vituo vipya hasa yale maeneo ya vijijini ili watumishi wetu waweze kupata *comfort*.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Emmanuel Nuwas.

Na. 47

**Kuongeza muda wa Marejesho kwa Watu Wenye Ulemavu**

**MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kuongeza muda wa marejesho ya Mikopo ya asilimia mbili kwa Watu wenye Ulemavu ili kujenga usawa?

**SPIKA**: Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Mwongozo wa utoaji, usimamizi na urejeshaji wa fedha za mikopo ya 10% kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, hakuna ukomo au muda maalum wa marejesho uliowekwa.

Mheshimiwa Spika, muda na utaratibu wa marejesho kwa makundi yote ikiwemo kundi la watu wenye ulemavu hufuata makubaliano kati ya halmashauri na wakopaji kwa kuzingatia aina ya miradi na aina ya mtiririko wa fedha katika shughuli iliyoombewa mkopo ili kuongeza ufanisi wa shughuli za wajasiriamali na marejesho ya mikopo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kusimamia Sheria, Kanuni na Miongozo ili kuwezesha makundi haya kunufaika na fursa hizi za mikopo ya 10%, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nuwas.

**MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Kwa kuwa watu wenye ulemavu wana changamoto ya kuweza kufika katika ofisi za umma kutokana na wengi wapo katika maeneo ya vijijini, je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia kuweza ku-*access* huduma za mikopo? *(Mikopo)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini kwa namna anavyowasemea wananchi wa jimbo lake. Vilevile, nampongeza kwa namna anavyofuatilia maslahi ya watu wenye ulemavu katika upatikanaji wa mikopo ya 10%.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeweka utaratibu: kwanza, tunazo Kamati za Mikopo ya 10% ngazi ya halmashauri, ngazi ya kata mpaka ngazi za vijiji. Pia tunao Maafisa Maendeleo ya Jamii ambao moja ya kazi yao ni kuhakikisha wanawafikia watu wenye ulemavu wenye uhitaji, na vikundi vingine vya wajasiriamali kwa maana ya vijana na wanawake wenye uhitaji kutoa elimu, hamasa na kuwawezesha kupata mikopo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, watu wenye ulemavu ambao hawawezi kufika katika ofisi za halmashauri, wanafikiwa kupitia *outreach services*. Pia tutaendelea kuboresha ili Maafisa Maendeleo na wataalamu wawafikie kwa ukaribu zaidi watu wenye ulemavu ili wapate fursa ya kupata mikopo ya 10%.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ikupa.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, kwenye jibu la msingi, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba mikopo hii

haina muda maalum wa urejeshwaji. Hata hivyo, huko *site* watu wenye ulemavu wamenyang'anywa bajaji kwa madai kwamba hawajakidhi masharti ya kurejesha mikopo hiyo ndani ya miaka miwili au mitatu.

Mheshimiwa Spika, je, nini kauli ya Serikali kwa zile bajaji ambazo zimeshanyang'anywa kwa watu wenye ulemavu kwa kigezo cha kushindwa kurejesha mikopo ndani ya muda uliokuwa umewekwa wa miaka mitatu au miwili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa swali zuri sana. Katika maelezo yangu ya msingi, nimesema mikopo ya 10% utaratibu wa marejesho hauna muda maalum, kwa maana kwamba kila mkopo unalipwa ndani ya mwaka mmoja au miwili au mitatu. Kila aina ya mkopo unategemea aina ya shughuli inayokwenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano ziko shughuli za kilimo ambapo wakopaji, au wajasiriamali wanahitaji kufanya shughuli za kilimo na kuanza mavuno, maana yake wale hawawezi kupewa muda sawa na mtu anayefanya shughuli ya ujasiriliamali kama mama lishe au baba lishe. Pia wapo ambao wanakopa bajaji au pikipiki, wale tunakubaliana kwamba ndani ya miaka miwili au miaka mitatu wawe wamerejesha.

Mheshimiwa Spika, haimaanishi kwamba aliyekopeshwa pikipiki ni sawa na aliyekopeshwa gari, mfano lori kwamba naye atalipa ndani ya miaka miwili. Hiyo ndiyo maana ya utaratibu wa mikopo ya 10%, hauna ukomo maalum. Uko *specific* kulingana na aina ya mkopo na aina ya marejesho ya fedha na aina ya shughuli ya ujasiriamali ambayo inatekelezwa na kikundi husika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Mtima.

**MHE. RASHID M. MTIMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Halmashauri ya Mji wa Newala ni miongoni mwa halmshauri ambazo mikopo hii hupitia benki ya *NMB*. Upatikanaji wa mikopo hii kupitia benki ya NMB umekuwa wa shida sana mpaka sasa vijana, wanawake na walemavu kutoka Halmashauri ya Newala Mji, bado kuna ugumu sana wa kupata mikopo hii.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali haioni haja ya kufanya ufuatiliaji na kufanya marekebisho ili kupitia benki hii, basi wananchi hao waweze kupata mikopo kwa wakati? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Newala Mjini. Ni kweli Serikali imeona changamoto: kwa mfano katika mikopo hii ya 10%, tangu tumeanza utaratibu mwaka wa fedha 2024/2025, zile halmashauri 174 ambazo tumeendelea na mfumo wa ukopeshaji kupitia halmashauri, zaidi ya 85% ya fedha ambazo zilitengwa kwa ajili ya mikopo zimeshakopeshwa ukilinganisha na 22% tu ya fedha zilizopitia kwenye benki ambazo zimekopeshwa kwenye halmashauri zile kumi zinazopitia utaratibu wa benki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni kweli kwamba kuna changamoto ya kasi ya upatikanaji wa mikopo kupitia benki kwa halmashauri zile kumi ambazo ziliwekwa kama *pilot* ikiwemo na Halmashauri ya Mji wa Newala. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tayari tumeshakaa na benki husika *CRDB*, *NMB* na wadau wengine kuona namna nzuri ya kuongeza kasi ya kutoa mikopo hii. Pia kuona namna nzuri ya kupitia utaratibu ili lengo la Serikali la kuwafikia wajasiriamali wote kupata mikopo kwa wakati ili waendelee na shughuli zao liweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutalifanyia kazi na hivi karibuni tutaona matokeo makubwa na mabadiliko makubwa kwa halmashauri

zote kupata fedha za mikopo mapema na wajasiriamali kunufaika mapema zaidi.

**SPIKA**: Mheshimiwa Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa akina mama waliozaa watoto wenye ulemavu wanapata shida sana kulea wale Watoto, kwa sababu inakuwa ni vigumu kukopesheka katika makundi ya akina mama.

Mheshimiwa Spika, katika halmashauri zetu, kuna fedha za watu wenye ulemavu. Sasa ni kwa nini Serikali isiangalie uwezekano wa kuwajumuisha akina mama waliozaa watoto wenye ulemavu katika sheria husika ili waweze kukopeshwa na kuwalea watoto wao kwa ufanisi zaidi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge wa Jimbo la Kilolo kwa kazi kubwa anayoifanya kwa wananchi wa Jimbo la Kilolo. Hata hivyo, naomba nimhakikishie tu kwamba kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya Mikopo ya Ujasiriamali 10%, tunayo makundi matatu, kundi la wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba wanawake waliozaa watoto wenye ulemavu, wanawajibika kuwatunza na kuwalea, lakini wanawake hawa pia wanaweza wakanufaika kupitia dirisha la mikopo ya wanawake kwa asilimia nne na wakaweza kufanya shughuli za ujasiriamali na kuendelea kuwalea watoto wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, pia tunatumia fursa hii kuendelea kuwashauri akina mama au wazazi na walezi wenye watoto wenye ulemavu, kwenda kueleza changamoto hizo kwenye halmashauri ili zifanye tathmini na kuona uwezekano wa kuwapa

upendeleo maalum katika vikundi vya wanawake ili waweze kupata nafasi nzuri ya kulea watu wenye ulemavu, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mfumo huu wa *Decentis* umefungwa na Bunge kupunguza matumizi ya karatasi. Bado kuna Waheshimiwa Wabunge wanaomba kuchangia kwa kuleta makaratasi. Haya makaratasi yanaharibu mazingira punguzeni, kila ukitumia karatasi unachafua mazingira kwenye nchi yetu. Niombe sana, mfumo huu ni mwepesi kutumia, bonyeza tu kitufe nami nakuona. *(Makofi)*

Kwenye ndege kuna *system* inaitwa *ILS (Instrument Landing System)*, rubani hatazami nje, anatazama mfumo wake. Nami wala siwatazami, natazama hapa. Hata kama mtu haingii kwenye mfumo, atapata. Mheshimiwa Matiko uliniletea ki-*note* nafikiri, siyo wewe! Basi siku nyingi sijakuona ndiyo maana nimekukumbuka. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Festo Sanga.

Na. 48

**Ongezeko la Bajeti aa Barabara – Makete**

**MHE. FESTO R. SANGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaongeza bajeti ya ujenzi na ukarabati wa barabara za *TARURA* za Wilaya ya Makete zenye urefu wa Km. 680.3 kutoka shilingi bilioni 3.2 hadi shilingi bilioni saba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara za vijijini na mijini kwa kutoa huduma za usafirishaji na usafiri kwa wananchi, imeendelea kuongeza bajeti za ujenzi na ukarabati kwa wilaya zote nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Makete.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Makete, Serikali imeendelea kuongeza bajeti ya fedha za ujenzi na ukarabati na ukarabati wa barabara kutoka shilingi milioni 834.59 katika mwaka wa fedha 2020/2021 hadi kufikia shilingi bilioni 3.9 katika mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha bajeti ya barabara za vijijini na mijini kote nchini zikiwemo barabara za Wilaya ya Makete.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sanga. Kuna mtu *mic* yake iko *on* zaidi ya Mheshimiwa Sanga! Bonyeza, Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza natumia nafasi hii kuishukuru Serikali kwa majibu mazuri kuonesha kwamba *trend* ya maongezeko ya fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara za *TARURA* Wilaya ya Makete, kwa niaba ya wananchi wa Makete, tunaishukuru sana Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami, bado kuna changamoto katika majimbo kwa sisi Waheshimiwa Wabunge hususan vijijini hata wa mjini. Kuna majimbo ambayo kilometa ni nyingi, lakini bajeti yake bado ni ndogo na kuna majimbo ambayo kilometa ni chache, lakini bajeti yao ni kubwa na hakuna uwiano wa fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, je, utaratibu upi uliowekwa na Serikali kutengeneza uwiano wa ugawaji wa fedha za ujenzi wa barabara za *TARURA* kwenye majimbo hayo?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa Wilaya ya Makete tuna changamoto kipindi hiki cha mvua. Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba kuna barabara ambazo zimekatika. Mfano, Barabara ya Mang'oto – Ibaga, Mlondwe, Kipengele, Ijangala –

Igole, na Maliwa – Sunti. Ziko barabara nyingi zimekwama kipindi hiki. Ni nini maelekezo ya Serikali kwa Meneja wa *TARURA*, Mkoa wa Njombe pia na Wilaya ya Makete ili kutumia fedha za dharura *(Emergency Fund)* ziweze kujengwa na kukarabati barabara zipitike?

**SPIKA:** Kwa kusimama kwake, ninawakumbusha *Bunge Marathon*. Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete, hakika anawatendea haki wananchi wa Jimbo la Makete, anafanya kazi kubwa. Nimhakikishie tu kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tangu mwaka 2021 mpaka leo mwaka wa fedha 2025/2026 imeendelea kuongeza bajeti za Mfuko wa Barabara kupitia *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano mwaka wa fedha huu bajeti yetu ambayo tunaitekeleza ni shilingi bilioni 710.31, lakini bajeti ijayo imeongezeka kwa zaidi ya shilingi bilioni 160.93 mpaka kufikia shilingi bilioni 871.24. Kwa hiyo, hii ni dalili ya wazi ya dhamira ya Serikali kuendelea kuongeza fedha za barabara ili kutatua kero za barabara kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Jimbo la Makete na baadhi ya maeneo ambayo yana changamoto kubwa za barabara. Kuna tofauti ya fedha ambazo zinazopelekwa kwenye majimbo. Kwa sasa vigezo ambavyo vinatumika ni vitatu, kigezo cha kwanza ni urefu wa mtandao wa barabara katika eneo husika, kigezo cha pili ni idadi ya wananchi katika eneo husika na kigezo cha tatu ni hali ya uchakavu wa barabara.

Mheshimiwa Spika, sasa katika eneo hili tumegundua changamoto kwamba yako maeneo yenye hali tofauti za kijiografia, maeneo yenye milima mingi, mvua nyingi ambayo yanahitaji fedha zaidi za barabara. Hivi sasa tuko hatua za mwisho za kupitia *formula* ya mgawanyo wa fedha za *TARURA* kwenye wilaya tukizingatia sana hali ya kijiografia *terrain*, milima,

mvua, mabonde na kadhalika ili barabara hizi ziweze kupata fedha ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutahakikisha Jimbo la Makete ambalo lina milima, barabara zina kona nyingi, lakini mvua za kutosha tutahakikisha kwamba zinapata fedha ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, la pili, Serikali kila bajeti inatenga fedha za dharura kwa ajili ya matengenezo ya dharura za barabara. Hivi sasa tunapoongea Serikali, tayari imeshatoa fedha zaidi ya shilingi 21,000,000,000 kwa ajili ya matengenezo ya barabara zilizoharibiwa na mvua.

Mheshimiwa Spika, hii ni fedha ya bajeti ya dharura. Serikali itaendelea kutenga fedha hiyo ili kuhakikisha kwamba barabara hizi zinatengenezwa zikiwemo barabara za Makete ambazo amezitaja Mheshimiwa Mbunge, na tayari tunapeleka fedha za dharura.

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kumwelekeza Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Njombe na Wilaya ya Makete wahakikishe wanakamilisha tathmini na kuleta gharama zinazohitajika kwa ajili ya matengenezo ya barabara zilizokatika.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, madaraja ya Nyasebe na lile la Kimoge kwenda Nyakisese yaliyopo Halmashauri ya Mji wa Tarime yamesababisha madhara makubwa sana ya kijamii na kiuchumi. Wiki iliyopita tu kuna raia walipelekwa na maji na wakapoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Daraja la Kimoge na Nyakisese limekuwa likitengewa fedha, lakini hamna utekelezaji, je, Serikali ina mpango gani sasa wa kunusuru na ukizingatia kwamba ni la kiuchumi zaidi kuhakikisha fedha ambazo zimetengwa mwaka huu wa 2026/2027 takribani shilingi 900,000,000 zitapelekwa ili ziweze kukamilisha ujenzi wa lile daraja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Esther Matiko kwa kuwawakilisha vyema wananchi wa Jimbo la Tarime Mjini, lakini nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Tarime Mjini kwamba kipaumbele cha Serikali ni kuhakikisha shughuli za kiuchumi na za kijamii za usafirishaji zinaendelea kutekelezwa bila mkwamo wowote.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, bajeti ambayo imetengwa ya shilingi 900,000,000/= kwa ajili ya daraja hilo na barabara ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja, tutasimamia *TARURA*, lakini Ofisi ya ya Waziri Mkuu TAMISEMI kuhakikisha zinapelekewa na kazi ya ujenzi inafanyika kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunda.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Lipembe ambayo inatoka Mbinga Mjini – kikolo – Kihungu sasa hivi imeharibika, liko katika hali mbaya na haipitiki na maeneo yale ni maeneo ya milima.

Mheshimiwa Spika, pia eneo la Kihungu kuna kituo cha afya mara nyingi wagonjwa wanatakiwa wapelekwe katika hospitali la wilaya. Nini tamko la Serikali kuhakikisha kwamba barabara hiyo inatengenezwa sasa hivi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunda, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Mjini. Hata hivyo, ni kweli kwamba barabara inayotoka Mbinga Mjini kwenda katika eneo alilolitaja ni barabara muhimu, na amekuwa akiifuatilia mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, tayari Meneja wa *TARURA* wa Mbinga na Mkoa wa Ruvuma wameshawasilisha taarifa ya mahitaji ya fedha ili kufanya matengenezo ya barabara hiyo. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunda pamoja na wananchi wa Mbinga Mjini kwamba Serikali ipo hatua za mwisho za kupeleka fedha ili matengenezo yafanyike na barabara hiyo iweze kutumika vizuri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kawamba Mustafa.

**MHE. JUMA R. MUSTAFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itafanya tathmini na kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa madaraja katika Kata ya Igalula katika Kijiji cha Vumilia, katika Kata ya Kizengi – Kisuli – Ndaki, katika Kata ya Tula – Chatulieni – Mihama, katika Kata ya Mmale, Kijiji cha Mbulumbulu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Mustafa, lakini ninamhakikishia kwamba Serikali imeweka mpango mkakati kwanza wa kutathmini na kutambua maeneo yote yanayohitaji madaraja kote nchini. Tuna *database* ya kila Jimbo, kila Mkoa; eneo gani linahitaji daraja? Eneo gani linahitaji kalvati na eneo gani linahitaji Barabara?

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, wamekuwa wakiwasilisha hoja hizo na sisi TAMISEMI tumezichukua na tumeziweka kwenye *database* zikiwemo madaraja ambayo Mheshimiwa Mbunge wa Igalula amesema. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tuko hatua za mwisho za kutafuta fedha na kuhakikisha kwamba tunakwenda kujenga madaraja hayo kwa awamu ili yaweze kupitika vizuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly.

Na. 49

**Kukamilisha Ujenzi wa Barabara ya Mtange – Kineng'ene Kibaoni**

**MHE. MOHAMED M. UTALY** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Barabara ya Mtange hadi Kineng'ene Kibaoni kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly, Mbunge wa Jimbo la Lindi Mijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kipande cha Barabara ya Mtange – Kineng'ene chenye urefu wa kilometa 5.5 hadi kufika Kituo cha Afya Kineng'ene ni sehemu ya Barabara ya Mtange – Kibaoni yenye urefu wa kilometa 19.3 iliyopo katika Jimbo la Lindi Mjini. Ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami umekuwa ukifanyika kwa awamu, ambapo mpaka sasa kipande cha kilometa 2.3 tayari kimejengwa kwa kiwango cha lami kwa awamu tatu tofauti ambazo zimegharimu kiasi cha shilingi bilioni 1.449.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali imetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa urefu wa meta 600 kwa kiwango cha lami. Aidha, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa mita 600 za kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu ili kuendelea na ujenzi wa barabara hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Utaly.

**MHE. MOHAMED M. UTALY:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ikiwemo pamoja na barabara iendayo katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa pamoja na barabara inayopita katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Lindi zilishaidhinishwa kujengwa katika awamu hii ya mwaka 2025/2026 ambapo mwaka huu wa fedha unaishia mwezi Juni.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mpaka sasa TAMISEMI haijatoa kibali, ili *TARURA* iweze kusaini mkataba na mkandarasi. Je, ni lini TAMISEMI itatoa kibali ili *TARURA* iweze kusaini mkataba na mkandarasi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly, Mbunge wa Lindi Mjini kwa kazi nzuri anayoifanya kwa ajili ya wananchi wa Lindi Mjini.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kwa nia njema imeweka utaratibu, baada ya kutangaza zabuni na kupata wakandarasi kuna utaratibu wa kutoa kibali baada ya kujiridhisha na uwepo wa fedha ili miradi ikianza na wakandarasi wakiwa *site* kusiwe na mkwamo wa kukosa fedha.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tayari Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kupitia *TARURA* imeshapokea maombi ya kupata kibali hicho na sasa wako hatua za mwisho za kutoa kibali hicho ili mkataba huu uanze kutekelezwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Johannes.

**MHE. JOHANNES L. LUKUMAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Tarehe 01 Oktoba, 2025 Mheshimiwa Dkt. Samia alifanya ziara katika Jimbo la

Arumeru Magharibi. Katika ziara hiyo aliahidi kujenga Soko la Kisasa la Mji wa Ngaramtoni. Ninapenda kujua Serikali itajenga lini Soko la Kisasa la Mji wa Ngaramtoni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Johannes Lukumay, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Magharibi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alishatoa maelekezo ya ujenzi wa Soko la Kisasa katika Jimbo la Arumeru Magharibi na tayari Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tumeshaliingiza kwenye mpango wa vipaumbele vya ujenzi wa soko hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Arumeru Magharibi kwamba Serikali hii inaahidi na kutekeleza. Maelekezo na ahadi za Mheshimiwa Rais ni kipaumbele namba moja. Tutahakikisha fedha zinaletwa, tunajenga soko hilo ili kuboresha huduma za biashara kwa wananchi wa Arumeru Magharibi. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha Motto.

Waheshimiwa ambao hamwongei sasa zimeni *mic* zenu. Ninawaomba mzime *mic* zenu wale ambao hamwongei.

Mheshimiwa Asha Motto.

**MHE. ASHA S. MOTTO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara kutoka Mnivata – Newala kuelekea Masasi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa

Spika, ninampongeza Mheshimiwa Asha Motto, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mtwara kwa kufuatilia maendeleo ya barabara na maendeleo mengine katika Mkoa wa Mtwara na kote nchini kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali imeweka *database* ya barabara zote ikiwemo Barabara hiyo ya Mtange kwenda Masasi kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi kwa awamu. Tunaendelea kukusanya fedha, kuweka mipango na kutafuta makandarasi kwa hatua na kwa awamu ili tuhakikishe barabara hizo zinajengwa. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kapoma.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Morogoro Mjini tuna Barabara ya Tungi ambayo imebakiza kipande kidogo sana, na hii barabara ni kati ya barabara za suluhisho za *diversion* endapo barabara kubwa ya Msamvu kuelekea Dar es Salaam ina shida. Sasa nilikuwa ninataka kujua mpango wa Serikali wa kumalizia hiki kipande kidogo cha kuunganisha Kihonda – Tungi kuelekea Dar es Salaam.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Josephine, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Morogoro, lakini nimhakikishie kwamba Serikali inatambua kwamba ziko barabara katika Manispaa ya Morogoro ambazo kwanza zimeharibiwa na mvua nyingi, lakini barabara nyingine ni chakavu ikiwemo barabara ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja. Lengo na dhamira ya Serikali ni kuendelea kujenga na kuboresha barabara hizo kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Manispaa ya Morogoro kwamba tutaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI nitumie fursa hii kuwasisitiza Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka kipaumbele kwenye fedha

za mapato ya ndani kwa mujibu wa maelekezo ya halmashauri ambazo zinakusanya zaidi ya shilingi bilioni 10, ni lazima watenge fedha kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa barabara.

Mheshimiwa Spika, hata halmashauri ambazo zinakusanya chini ya shilingi bilioni 10 kama barabara ni kipaumbele kikubwa katika eneo hilo, ni muhimu watenge fedha kwa ajili ya ukarabati wakati tunasubiri fedha za Serikali Kuu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnesta. Mheshimiwa Asenga zima *mic*, na kule nyuma kule Mheshimiwa zima *mic* huko.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kuniona. Mradi wa *DMDP II* ndani ya Kata ya Vingunguti, Liwiti, Kimanga na Tabata ume-*stuck* tangu 2023 na sababu kubwa ni Serikali kutokulipa fidia kwa wananchi ambao mradi huo unawapitia, na sasa barabara ni mbovu sana, Naibu Waziri utakubaliana nami. Swali langu kwa Serikali, ni lini italipa fidia na lini ujenzi utaanza kwenye hizi Barabara za *DMDP II*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninampongeza sana Mheshimiwa Agnesta Lambert, Mbunge wa Segerea kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya kuwasemea wananchi wa Jimbo la Segerea.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kupitia dhamira nzuri ya Serikali hii ya kuboresha barabara katika Jimbo la Segerea, Mradi wa *DMDP II* ulianzishwa kwa ajili ya Kata ya Vingunguti, Liwiti, Kimanga na Tabata na eneo lile la barabara lilihitaji fidia kwa wananchi. Serikali ilifanya tathmini na kupata gharama ya awali ya fedha kwa ajili ya kulipa fidia.

Mheshimiwa Spika, kutokana na malalamiko ya baadhi ya wananchi kutoridhishwa na malipo ya fidia, na pia wengine ambao waliendeleza maeneo ambayo walihitaji pia kufanyiwa tathmini, Serikali ililazimika kurejea tena kufanya tathmini mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari mwezi wa tatu tumekamilisha uthamini kwa mara ya pili na sasa tuko hatua za mwisho za kulipa fidia, na baada ya kulipa fidia, wakati wowote mapema iwezekanavyo tutaanza ujenzi wa barabara hizi kupitia Mradi wa *DMDP II.*

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Zuena Bushiri.

Na. 50

**Ujenzi wa Chanzo cha Maji Kata ya Maore - Same Mashariki**

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga chanzo cha maji kilichobebwa na mafuriko katika Kata ya Maore Same Mashariki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa muda mfupi, Serikali kwa kushirikiana na wananchi wa Kata ya Maore imekamilisha ukarabati wa dharura wa chanzo cha maji Maore na sasa zaidi ya wananchi 14,000 wa vijiji vitatu vya Maore, Kadandu na Mheza vinavyopatikana katika kata hiyo, wanapata huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa muda mrefu, Serikali inaendelea na usanifu wa mradi utakaojumuisha pia maboresho ya ujenzi wa chanzo cha Maore. Usanifu wa mradi huo unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2025/2026 na utekelezaji wake kufanyika baada ya fedha kupatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bushiri.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza ninaomba nirekebishe jina la Kijiji kimoja, siyo "Kadandu" ni "Kadando."

Mheshimiwa Spika, katika majibu ambayo yamewasilishwa hapa kidogo yananitia utata, siyaelewi, kutokana na hali halisi ya *site* ilivyo. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuongozana nami kwenda *site* kuona hali halisi ilivyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Zuena kwa kazi nzuri, kwanza akiwa Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, kwa mchango wake wenye tija katika kuhakikisha kwamba tunaendelea kuboresha huduma ya majisafi na salama kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, ninafahamu kazi kubwa aliyoifanya katika ushawishi wake na Mradi wa Maji wa Same – Mwanga – Korogwe wenye zaidi ya shilingi bilioni 406 uliotekelezwa katika maeneo ya Same, katika Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, kwa ombi la Mheshimiwa Mbunge, Serikali dhamira yake ni kusikiliza changamoto za wananchi na kuchukua hatua. Serikali kupitia Wizara ya Maji, tuko tayari kuongozana na Mheshimiwa Mbunge kwenda kujionea hali halisi kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameomba ili tuweze kuchukua hatua kulingana na tathmini ambayo tutakuwa tumeifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, nami niulize swali dogo la nyongeza. Hivi tunavyozungumza, miradi ya Bunda ya Maji ya kati ya yenye thamani ya shilingi bilioni saba imesimama. Mradi wa Wariku, Mradi wa Migungani kwenda

Kaswaka, Mradi wa Kisangwa ambao maji yanaenda mpaka Chuo cha Kisangwa imesimama.

Mheshimiwa Spika, lini fedha zitakuja ili wakandarasi waendelee na kazi? Katika hili wala sitaki tuambatane wote kwa sababu Mradi mmoja alikuja akauzindua, sasa tunahitaji fedha ili miradi ya maji ikamilike, wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini wapate majisafi na salama. Lini wataleta shilingi bilioni saba? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na ninamshukuru sana Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Bunda Mjini kwa kazi nzuri sana ambayo anaifanya, na ninatambua kwamba mimi pamoja naye tulikuwepo Jimboni kwake na tulifanya shughuli mbalimbali, lakini pia tunatambua kwamba tunayo miradi mingi ambayo inaendelea.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba Mkandarasi alikuwa ana madai yake, alikuwa hajalipwa na tumeshapokea hati zake na tayari tumeshaziandaa kwa ajili ya kuziwasilisha Wizara ya Fedha. Tutakachokifanya ni kuongeza msukumo kuhakikisha kwamba fedha hizi zinafika kwa wakandarasi ili waweze kuendelea na mradi huu ambapo tunaamini utakapokamilika na maji yatakapotoka, wananchi wa Bunda wataweza kufurahia sauti ya Mbunge wao anapokuwa anawasemea. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kawawa.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Ninaomba nianze kwa kuipongeza Wizara ya Maji kwa jitihada za kutumia maji ya Mto Rufiji kama Mradi wa suluhisho la kudumu la kutuletea maji katika Mkoa wetu wa Lindi ambapo sehemu nyingi zitanufaika. Mradi huu ni mpango wa muda mrefu, lakini bado haujaanza nadhani, kwa hiyo, unatupa tu matumaini.

Mheshimiwa Spika, swali langu sasa, kwa kuwa tunavyo vyanzo vingine vya mito ama vya maji ambavyo vinaweza vikatumika wakati tunasubiria mradi huu uje kuanza, kwa mfano katika taarifa…

**SPIKA:** Mheshimiwa twende kwenye swali…

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** … Kijiji cha Nahama ambacho kina uhaba mkubwa wa maji, tuna vyanzo vya mapango ya Nang'ole katika Kijiji cha Nandete ambavyo vina maji ya kutosha. Je, ni nini mpango wa Serikali wa kutumia chanzo hiki kama suluhisho la muda, wakati tunaendelea kusubiria mradi mkubwa ambao unakuja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni mpango wa Serikali na umekuwa utaratibu wa Serikali kuendelea kuchukua hatua za muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu kulingana na uhitaji wa maji katika maeneo mbalimbali nchini. Ombi la Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Serikali kupitia sekta ya maji tunalipokea badala ya kusubiria suluhisho la kudumu. Wananchi wa eneo lake wanahitaji kupata huduma ya maji na sisi tutaenda kufanya hivyo ili waweze kupata maji wakati tukiwa tunasubiri utekelezaji wa mradi mkubwa.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Juliana Shonza. Mheshimiwa Shonza, subiri.

Waheshimiwa Wabunge, huu mfumo kila ninayemsoma hapa yuko *active*, kwa maana mwenye swali sasa hawezi kusema; na mwenye swali akisimama, mimi simwoni katika *screen* yangu. Ninawaomba unapotaka swali la nyongeza usijiweke kwenye foleni, subiri Waziri akishamaliza kujibu bonyeza kitufe chako mimi nitaku-*capture*. Ninaomba sana Waheshimiwa Wabunge. Sasa wote zimeni ving'amuzi vyenu.

Mheshimiwa Shonza.

Na. 51

**Utekelezaji wa Mradi wa Maji Kutoka Mto Momba**

**MHE. JULIANA D. SHONZA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza utekelezaji wa Mradi mkubwa wa Maji kutoka Mto Momba ili kuboresha huduma ya maji kwa wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza utekelezaji wa mradi mkubwa wa kutoa maji Mto Momba kwenda miji ya Vwawa, Mlowo na Tunduma kwa gharama ya shilingi bilioni 119.95. Miongoni mwa kazi zinazotekelezwa kupitia mradi huo ni pamoja na ujenzi wa chanzo cha maji chenye uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 21.5 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mtambo wa kuchuja na kutibu maji *(treatment plant)* chenye uwezo wa kutibu maji lita milioni 20 kwa siku, ujenzi wa matanki matatu yenye jumla ya ujazo wa lita milioni 10 sanjari na ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 317.

Mheshimiwa Spika, mradi huo upo kwenye hatua za awali za utekelezaji ambapo unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2027 na kunufaisha zaidi ya wananchi 1,245,000 wa miji ya Tunduma, Vwawa, Mlowo pamoja na vijiji 31 vya Wilaya ya Momba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shonza. Mheshimiwa Nassari, Mheshimiwa Makoi, Mheshimiwa Lufungija, Mheshimiwa Midimu, wote mmewasha *mic* zenu, mnamsumbua mwenye swali la msingi.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Kwa kuwa, mradi huu ulizinduliwa mwezi Machi, 2025 na mpaka sasa ni mwaka mmoja kamili umepita bado tuko kwenye hatua za

awali. Kwenye majibu ya msingi Mheshimiwa Waziri amesema kwamba mradi unatarajiwa kukamilika mwaka mmoja na nusu tu kutoka sasa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, haoni sasa kuna haja kubwa ya Serikali kuanza kuongeza kasi ya utoaji fedha, na vilevile usimamizi, ili mradi huu uweze kukamilika kwa wakati, ikizingatiwa kwamba, wanawake wenzangu wa Mji wa Tunduma, Mji wa Mlowo pamoja na Mji wa Vwawa wanapata shida kubwa sana ya maji? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalumu, kwa swali lake. Ni kweli kabisa Mheshimiwa amekuwa sehemu ya utafutaji wa miradi ya maendeleo ndani ya Mkoa wa Songwe na amekuwa akishirikiana vizuri kabisa na Waheshimiwa Wabunge wenzake wa majimbo. Pia, tunatambua kwamba, mradi huu ambao ni uwekezaji mkubwa sana wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, zaidi ya shilingi bilioni 119 zimewekezwa pale.

Mheshimiwa Spika, pia, tunafahamu kwamba, mkandarasi alikuwa anahitaji *advance* ya zaidi ya shilingi bilioni 17. Hivi sasa tayari tumemlipa shilingi bilioni 5.9 na tunaendelea na hatua nyingine za kumalizia ile fedha iliyobaki. Tayari tumefanya *site possession,* tarehe 18 mwezi wa Tatu, yuko *site,* mradi umeanza na uko katika asilimia moja nukta saba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninamtoa hofu Mheshimiwa Mbunge, Serikali dhamira yake ni kuhakikisha kwamba, mradi huu unaenda kuendelea vizuri na ukamilike kwa wakati. Pale tutakapoona inabidi, huwa tunatoa maelekezo kwa wakandarasi kuongeza wafayakazi na kufanya kazi usiku na mchana. Lengo ni kwamba, ukamilike ndani ya muda wa mkataba. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nassari.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kuniona na mimi niulize swali dogo la nyongeza kwa Waziri wa Maji hapo. Kuna miradi mingi ya maji pale Arumeru, ambayo Serikali imeiasisi, lakini miradi ile imesimama kwa sababu ya kukosa fedha. Mathalani Mradi wa Imbaseni, Maji ya Chai, Kikatiti mpaka Maroroni, halikadhalika Mradi wa kule Uwiro, yote imesimama kwa sababu, *certificates* hazijalipwa. Je, Serikali inatoa *commitment* gani, ili wakandarasi waweze kurudi *site*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Nassari, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza pamoja na kuuliza swali, Mheshimiwa Nassari tumekuwa tukizungumza sana mara kwa mara kuhusiana na suala hili. Kuna kipindi tulipanga ziara ya kwenda kuona namna gani tunaweza tukachukua hatua, ili miradi hii iweze kukamilika; lakini nimtoe hofu, miradi na wakandarasi wake tumeanza kufanya *engagement,* ili kuona namna gani tunakubaliana wakati tunashughulika kuhusu malipo ya hati zao za madai. Wao warudi *site,* ili kuhakikisha tusiwe na *gap* lolote hapa Katikati. Lengo ni kwamba, mradi ukamilike kwa wakati, na fedha zao waweze kulipwa wasije wakawa na changmoto yoyote ya kifedha. Ninakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, Kata za Fukayosi na Makurunge, Jimbo la Bagamoyo, zina changamoto kubwa ya maji kwa vile tu zimeunganishwa na miundombinu ya maji kutoka Mto Wami, ilhali wapo karibu na chanzo cha maji cha Mto Ruvu Chini na mara kadhaa kumekuwa na ahadi ya kuwaunganisha sasa na miundombinu ya maji kutoka Ruvu Chini, je, wananchi hawa wawe na matumaini na mwaka wa fedha 2026/2027 kwamba, ahadi hiyo itatimizwa? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali dogo la Mheshimiwa Subira Mgalu, Mbunge wa Bagamoyo. Bahati nzuri ni kwamba, mradi ambao unaenda kutatua changamoto ya wananchi wa Bagamoyo, na kwa vile ameuliza matumaini, ni kweli kabisa wananchi wawe na matumaini katika mwaka 2026/2027; tunaenda kuwaingiza kwenye bajeti hiyo ili waweze kufikishiwa huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Spika, kikubwa tu ni kwamba, tuendelee kuwa na subira kwa sababu, miradi iko mingi ambayo bado iko kwenye utekelezaji; zaidi ya miradi 200 na kitu kwa mijini, na ni zaidi ya miradi 878 ambayo ina gharama ya shilingi trilioni 1.3. Bado tutahitaji kuanzisha miradi ambayo itakuwa ya kimkakati, ikiwemo ndani ya Jimbo la Bagamoyo. Ninakushukuru sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa *Engineer* Ulenge.

Na. 52

**Kutwaa Maeneo ya Karibu na Bandari ya Tanga**

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatwaa maeneo ya karibu na Bandari ya Tanga, ili kuongeza eneo la utekelezaji wa shughuli za Bandari?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa Mnyaa, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Ulenge, Mbunge wa Viti Maalumu, Mkoa wa Tanga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto ya uhaba wa eneo katika Bandari ya Tanga, Serikali kupitia *TPA,* inaendelea na taratibu za utwaaji wa eneo karibu na Lango Namba Mbili na

eneo la *Police Marine,* ili yatumike kwa ajili ya shughuli za kibandari.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utwaaji wa maeneo hayo, *TPA* inaendelea na mpango wa matumizi bora ya maeneo yaliyopo ndani ya bandari, ikiwa ni pamoja na uhamishaji wa baadhi ya maghala, ili kuongeza maeneo ya kufanyia shughuli za kibandari.

**SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Ulenge.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Mchakato wa kutwaa maeneo aliyoyataja Naibu Waziri katika Bandari ya Tanga ulianza mwaka 2014 na mwaka 2015, takribani miaka 10 sasa. Ninaomba kuelewa, mpaka sasa Serikali inafeli wapi kuweza kutwaa maeneo hayo?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Serikali ilishatwaa maeneo katika Bandari ya Mwambani zaidi ya miaka 10 sasa. Takribani shilingi bilioni 10 zilitumika kuwalipa wananchi wale waliopisha maeneo yale. Je, ni nini mkakati wa sasa wa kuendeleza maeneo ya Bandari ya Mwambani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'azi Ulenge kwa ufuatiliaji wake mkubwa, makini wa Bandari ya Tanga na miradi yote ya kimkakati, ambayo ina maslahi makubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pili, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali haijafeli, inatambua umuhimu wa Bandari yetu hii ya Tanga kwa uchumi wa Taifa letu na wananchi wa Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana bandari hii ambayo ilianzishwa miaka 146 iliyopita ilifanyiwa maboresho karibu mara mbili, mwaka 1913 na mwaka 1954. Ni Mheshimiwa Dkt. Samia

Suluhu Hassan mwaka 2023 aliyetimiza ndoto za kufanya mabadiliko na mageuzi makubwa ya kibandari katika Bandari ya Tanga, ambapo alitoa fedha shilingi bilioni 429.1 ambazo zilikwenda kuleta mabadiliko makubwa kwenye bandari, tumeona kina kimeongezeka, eneo la kugeuzia meli limeongezeka, pamoja na vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko hayo makubwa ya kibandari, tumeshuhudia shehena imeongezeka zaidi, mzigo umetoka tani 735,000 mpaka takribani tani milioni 1.4. Tumeona magari ambayo yalikuwa hayahudumiwi mwanzoni kwenye Bandari ya Tanga, kwenye mwaka wa fedha uliopita yamehudumiwa magari 15,618. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata mawakala wa meli wamechangamkia fursa. Tulikuwa na mawakala 29 tu, wakafika 33, na hata idadi ya meli zimeongezeka zaidi kutoka 113 mpaka takribani meli 458; hata makasha yalitoka 7,000 mpaka 9,000. Unaweza kuona kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia ameifanya kwenye bandari hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu mkubwa, leo Bandari ya Tanga watu wengi wanakimbilia kwenda kupata huduma zao. Ninakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge makini anayefuatilia jambo hili kwamba, sasa tunahitaji maboresho makubwa. Ndiyo maana hata ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokwenda huko hivi karibuni aliiagiza Wizara hii na kumwagiza Mheshimiwa Waziri wetu na sisi wote tuhakikishe kwamba, tunabuni zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge wetu kwamba, Serikali kama ambavyo nimesema, haijafeli, imeshaanza mchakato wa kutwaa ekari saba pembeni mwa Bandari ya Tanga. Hivi ninavyozungumza, kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, mchakato umeshaanza. Tunachokifanya ni tuweze kulipa fidia, tuweze kuongeza gati nyingine tatu zifike tano. Vivyo hivyo kwa upande wa Mwambani, kama alivyozungumza, tayari tumepokea maelekezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wetu na wenzetu wa *TPA* wameshaanza mchakato.

Mheshimiwa Spika, katika zile *acre* 174 zilizokuwa zimetwaliwa takribani miaka 10 iliyopita, ambalo ndiyo swali lake la pili, tumeshakamilisha upembuzi yakinifu. Sasa tumetwaa eneo, huwezi kupanga matumizi bila kujua unataka kwenda kufanya kitu gani? Tumemaliza upembuzi yakinifu, na tayari tunaanza kwenda kutekeleza. Pengine mwaka wa fedha ujao, nini tutakwenda kukifanya? Ninawaahidi, wakati tunasubiri kuanza kutumia eneo hilo kubwa tayari ndiyo eneo ambalo tunalitumia kwa ajili ya maegesho yetu ya magari.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, ninawaomba wenzetu wa Wizara ya Ardhi watusaidie kukamilisha kwenye utwaaji wa ardhi hiyo na kuiagiza Mamlaka ya Bandari Tanzania, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri kwamba, wakamilishe haraka iwezekanavyo kwa sababu, uhitaji wa Wanatanga na Watanzania kuona bandari hiyo inazidi kuboreshwa zaidi ni mkubwa zaidi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Cornel Maghembe.

**MHE. CORNEL L. MAGEMBE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wapo wananchi wengi katika eneo la Kata ya Katende na Bukome katika Jimbo la Chato Kaskazini, ambao maeneo yao yalitwaliwa, kwa ajili ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Chato. Mpaka sasa, karibu miaka saba hadi nane, hawajawahi kulipwa fidia yao, na wananchi wale hawana maeneo mengine ya kwenda kufanya shughuli za kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Spika, sasa kauli ya Serikali ni nini juu ya wananchi hao? Ni lini sasa wanakwenda kulipwa fidia yao, ili waendelee na shughuli zao za uzalishaji mali? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na eneo lake na pengine, kwa sababu yanaweza kujitokeza maswali ya namna hii mengine, ni kwamba, tayari Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi na

Mamlaka ya Bandari ya Tanzania imeshaanza kuandaa orodha ya maeneo yote ambayo tumeshayatazama, kama ni *potential*, ambayo ni muhimu, ili kutazama namna ya kuwalipa fidia wananchi hao na kisha tuweze kuyapangia matumizi.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge akubaliane na mimi kwamba, tulikuwa na miradi mingi, Dar es Salaam mradi mkubwa, Tanga, Mtwara na kwenye Maziwa Makuu, kama vile Kigoma, *Mbamba Bay* kule Nyasa, Kemondo na kadhalika. Naomba Mheshimiwa Mbunge atupe muda kidogo, siyo muda mrefu. Tutakapokuwa tumekamilisha tutakwenda kuipangia matumizi na kwenda kulipa maeneo yote ambayo pengine tulikuwa hatujakamilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kijakazi.

**MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi, ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Tunafahamu kwamba, hakuna mpango wa Serikali ambao hauna *timeframe* kwa hiyo, na mimi ningependa kuuliza swali, kama ilivyo kwa Jimbo la Mheshimiwa Magembe kule Wilaya ya Kilwa, hususan eneo la Kilwa Masoko, wanakabiliana na changamoto ya namna hii.

Mheshimiwa Spika, upanuzi wa *airport* umeahidiwa kwa muda mrefu sana, maeneo ya watu yamechukuliwa na mpaka sasa hawajalipwa fidia, wananchi wale wanaendelea kuteseka. Napenda kufahamu, ni lini wananchi wa Kilwa Masoko watalipwa fidia ili waweze kuendelea na maisha yao? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Kijakazi amezungumza, ni kweli kabisa. Serikali kwa kutambua umuhimu wa eneo la Kilwa Masoko kuendeleza kiwanja kile, tulishatazama takribani wananchi karibu 600, na fedha tuliainisha. Siyo eneo hilo tu moja peke yake, tayari na maeneo mengine ya viwanja vya ndege nchini ambayo

tumeona ni muhimu kwenda kuyaendeleza tumekamilisha kufahamu mahitaji, tumepeleka Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kulingana na upatikanaji wa fedha, tunakwenda kulipa fidia katika eneo hili.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Fedha. Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila.

Na. 53

**Matumizi ya Rasilimali za Taifa Kama Dhamana ya Wafanyabiashara**

**MHE. CHARLES M. NJAMA K.n.y. MHE. MABULA J. MAGANGILA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza kutumia rasilimali zake kama dhamana, ili Wafanyabiashara wa Kitanzania waweze kukopesheka zaidi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila, Mbunge wa Jimbo la Msalala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania imefanya jitihada za kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa wafanyabiashara wawekezaji kwa kutumia rasilimali zake kama dhamana, kupitia mikopo yenye masharti nafuu inayotolewa kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati kupitia Benki ya *NMB* kwa riba ya asilimia saba tu kwa mwaka. Hatua hii inalenga kuongeza uwezo wa kukopesheka na kukuza uchumi wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na jitihada za kuwawezesha wananchi kiuchumi. Imeipatia Benki Kuu ya

Tanzania wajibu wa kusimamia Mifuko ya Udhamini wa Mikopo, ambayo inatoa udhamini kwa Watanzania wenye miradi yenye tija katika sekta mbalimbali za uchumi, lakini wana changamoto za dhamana zinazohitajika wakati wa kuomba mkopo, ili waweze kupata mikopo kupitia taasisi za fedha.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wanaweza kunufaika na huduma za Mfuko wa Udhamini wa Mikopo ya Mauzo ya Nje ya Nchi *(Export Credit Guarantee Scheme)* huku wajasiriamali wadogo na wa kati wakinufaika kupitia Mfuko wa Udhamini wa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati *(Small and Medium Enterprises Credit Guarantee Scheme)*. Mfuko huu una lengo la kurahisisha upatikanaji wa mikopo, kukuza miradi ya kiuchumi na kuongeza tija katika sekta zote za uchumi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mabula.

**MHE. CHARLES M. NJAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ninapenda kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, wananchi wengi wa Jimbo la Msalala wamejiajiri na kuajiri watu wengi katika uchimbaji mdogo wa madini ya dhahabu na wamekuwa wakishindwa kukua kufikia uchimbaji wa kati na mkubwa kwa kukosa mitaji mikubwa na nafuu, je, ni lini Mheshimiwa Waziri utakuwa tayari kukutana na wafanyabiashara wa Msalala, ili kuwapatia elimu ya namna wanavyoweza kunufaika na mfuko huu wa dhamana? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nachukua fursa hii kumpongeza sana Mbunge wa Jimbo la Msalala, Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila, kwanza kwa kuendelea kupigania haki za wafanyabiashara na wachimbaji wadogo wadogo wa madini ya dhahabu ndani ya Jimbo lake la Msalala.

Mheshimiwa Spika, katika swali hilo la nyongeza, ninapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Msalala kwamba, Wizara ya Fedha, kupitia Ofisi ya Waziri, tuko tayari. Kabla ya kwisha kwa Bunge hili la Bajeti, tutakuwa tumefika katika

Jimbo la Msalala kuongea na wafanyabiashara na wachimbaji wadogo wadogo wa madini ya dhahabu kuwapa elimu hii ya Mifuko ya Dhamana, ambayo ni hitaji kubwa kwa wafanyabiashara hao, ili waweze kupata mikopo hiyo kwa masharti nafuu na riba ndogo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaomba... *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kija, *microphone* yako bado iko *active* kwangu. Ninaomba uzime *microphone* yako.

Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Mifugo, Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi.

Na. 54

**Wananchi Kushiriki kwenye Uchumi wa Bluu**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza: -

Je, Serikali inachukua hatua gani kuwawezesha Wananchi hususan Vijana na Wavuvi wadogo kushiriki kikamilifu katika uchumi wa buluu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ya kuwawezesha wananchi, hususan vijana na wavuvi wadogo, kushiriki kikamilifu katika uchumi wa bluu kwa lengo la kuongeza ajira, kipato, na mchango wa sekta ya uvuvi katika uchumi wa Taifa. Serikali inaendelea kutekeleza Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora, ambapo katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara imepokea kiasi cha shilingi bilioni 30.7 (shilingi bilioni 25.9 katika Uvuvi na shilingi bilioni 4.75 katika Mifugo), kwa ajili ya

kuwawezesha wavuvi wadogo pamoja na vijana katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha, kupitia Programu hii ya *BBT,* vijana 308 kutoka mikoa yote nchi nzima wamepatiwa mikopo isiyo na riba na yenye masharti nafuu kwa ajili ya kutekeza miradi ya ufugaji wa samaki kwenye vizimba, ufugaji wa majongoo bahari, unenepeshaji kaa na kilimo cha mwani.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania *(TADB)* inaendelea kutekeleza zoezi la utoaji wa mikopo isiyo na riba na yenye masharti nafuu kwa wavuvi wadogo, wakiwemo vijana, kwa kuwawezesha kupata nyenzo za uvuvi ikiwemo maboti ya kisasa pamoja na nyavu za uvuvi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza: Je, Serikali inashirikiana vipi na sekta binafsi na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali ili kuongeza fursa kwa wanawake katika uchumi wa bluu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, ni vigezo gani vinatumika kupima mafanikio ya wananchi wanaoshiriki katika uchumi wa bluu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Ninampongeza sana Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, kwanza kwa kuaminiwa na wanawake waliompa ridhaa ya kuwepo Bungeni hapa, lakini kwa kuendelea kupambana kwa maslahi mapana ya wanawake hawa.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la kwanza kuhusu nia na madhumuni ya sekta ya Serikali yetu ya Mheshimiwa Dkt. Samia

Suluhu Hassan, Serikali ya Awamu ya Sita na maelekezo mahsusi ya Rais ni kwamba, tuendelee kuziwezesha na kuzilea sekta binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali na kushirikiana nayo kwa karibu sana katika sekta zetu.

Mheshimiwa Spika, nasi katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi hatupo nyuma, katika sekta yetu ya uvuvi, tunaendelea kuhakikisha kwamba tunazisogeza sekta binafsi na taasisi zetu za kifedha hasa mabenki, kuendelea kuwapunguzia vikwazo mbalimbali katika utendaji wao wa kazi ili kuhakikisha kwamba tunawanyanyua na kuwapa fursa nyingi zaidi hasa wanawake ili kuhakikisha kwamba wananyanyua uchumi wao na kushiriki katika sekta yetu ya uvuvi.

Mheshimiwa Spika, pia katika swali lake la pili la kuhusu vigezo gani tunatumia ili kupima maendeleo au upandaji wa sekta yetu ya uvuvi katika makundi haya maalum; tumeendelea kufanya kazi na vijana, wanawake na makundi maalum kwa karibu sana na kuchukua takwimu kwa kila mwaka, kuangalia namna gani tumewawezesha, kuwafuatilia kwa karibu kuhakikisha kwamba uwezeshaji tunaowapa unazaa matunda.

Mheshimiwa Spika, hivyo, tunazo takwimu za kutosha Wizarani kuona kwamba kila mwaka kadri tunavyotoa uwezeshaji huu na kadri Serikali inavyotenga bajeti, basi fedha hizi zinavyowafikia wanufaika hawa zinawapa manufaa yanayostahili.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Injinia Kija.

Na. 55

**Uhitaji wa Eneo la Ujenzi wa Kituo cha Zimamoto – Katoro**

**MHE. KIJA L. NTEMI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatoa eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Zimamoto ili kusaidia majanga ya moto yanapotokea Katoro?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali Na. 55 la Mheshimiwa Injinia Kija Limbu Ntemi, Mbunge wa Katoro, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kusogeza huduma za zimamoto na uokoaji karibu na wananchi ikiwemo ujenzi wa vituo vya zimamoto na uokoaji. Aidha, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limepata kiwanja Na. 1384 kilichopo Kitalu Namba "A" chenye ukubwa wa mita za mraba 4,987 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Zimamoto na Uokoaji katika Mji wa Katoro, na utaratibu wa kupata hatimiliki zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Kija.

**MHE. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimwulize Waziri maswali ya nyongeza mawili. Swali la kwanza, kwa sababu ya uharaka wa ujenzi wa kituo hiki, na kwa sababu sasa hivi wale zimamoto wanapata shida sana sehemu ya kuishi, je, ni lini sasa hiyo hati itakamilika, kwa sababu tulipita kwenye mfumo wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan uliokuwa unaitwa Samia Ardhi na ulikuwa kwake Mheshimiwa Waziri, nadhani na katika sehemu nyingi alipita, lini sasa tutapata hiyo hatimiliki kwa ajili ya kuanza ujenzi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari baada ya kupata hiyo hati kuambatana na mimi kwenda kutukabidhi hilo eneo ili kuleta motisha katika jamii na watu wa Katoro? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kumpongeza sana Injinia Kija, kwanza kwa ukaribu wake na wananchi wake, anayeweza kufuatilia changamoto za wananchi wake. Ninakiri kuwa jambo hili analifahamu kwa kina na ndiyo maana analifuatilia kujua lini hati itatoka?

Mheshimiwa Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba swali lake limekuja kwa wakati muafaka, hati hii nikitoka hapa leo nitaenda kuifuatilia na ndani ya wiki ijayo nitampatia jibu ambalo nina uhakika atapata lini hati yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili la Mheshimiwa Injinia Kija ni kwamba Wizara ipo tayari na mimi nipo tayari kuongozana naye katika muda ambao atapanga ili twende kwenye eneo hilo, huku nikifahamu jimbo lake ni kubwa na lina ukuaji mkubwa wa kiuchumi. Ninafahamu hata Kata tu ya Katoro pale jinsi ilivyo na watu wengi zaidi ya 92,000 inahitaji huduma za zimamoto za haraka. Kwa kweli tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na gari ipo, tukijenge kituo hiki, tunawaletea na gari kabisa, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Alan Thomas.

**MHE. ALAN T. MVANO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Wilaya ya Kakonko ilianzishwa tarehe 8 Machi, 2013 na hadi leo hatuna Ofisi ya Zimamoto wala gari la Zimamoto. Je, ni lini Serikali italeta gari la Zimamoto na kujenga ofisi kwa kuwa tayari eneo lilishatengwa? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mbunge kutoka Kakonko kwa kazi nzuri ambayo anaifanya, nimhakikishie tu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amefanya mapinduzi makubwa sana kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani, hususan Jeshi hili la Zimamoto.

Mheshimiwa Spika, nikuhakikishie mpaka sasa hivi kwa mkopo ambao ameupata zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 100 ameweza kununua magari zaidi ya 237 ambayo yamesambazwa katika mikoa na wilaya zake.

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyozungumza sasa, kuna Wilaya sita tu ambazo hazijapata magari haya na siyo kama hawajapata kwa sababu hawastahili, hapana, ni kwa sababu madereva wanaotakiwa kuendesha magari hayo bado hawajapatikana katika Wilaya hizo.

Mheshimiwa Spika, nikuhakikishie, kwa jitihada ambazo Serikali inazifanya, hao madereva, hao Askari sasa hivi wapo vyuoni na watafundishwa na watapatikana na tutampelekea gari pamoja na madereva kwa ajili ya vituo hivyo sita. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Nassoro Rashid Nassoro.

Na. 56

**Kuweka Kituo cha Uhamiaji Eneo la Makangale**

**MHE. NASSORO RASHID NASSORO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaweka kituo kidogo cha uhamiaji katika eneo la Makangale linalokua kwa kasi kiutalii kwa ajili ya ukaguzi wa wageni?

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nassoro Rashid Nassoro, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma za kiuhamiaji katika maeneo yote ya kimkakati yenye utalii ikiwemo Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha ujenzi wa Ofisi ya kisasa ya Uhamiaji katika Wilaya ya Micheweni Pemba, ambayo inatoa huduma katika Shehia 25 ikiwemo Shehia ya Makangale. Aidha, katika vipaumbele vya bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali ina mpango wa kununua kiwanja katika eneo la Makangale kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Nassoro.

*(Hapa Mhe. Nassoro Rashid Nassoro alizungumza bila Kutumia kipaza sauti)*

**SPIKA:** Mheshimiwa huingii kwenye *Hansard.* Huku kuna *microphone*.

**MHE. NASSORO RASHID NASSORO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri aliyonipa, lakini katika eneo hilo la Makangale ambalo sasa hivi linaendelea kukua kiutalii na wageni wanaingia na kutoka, na wengine bila kuripoti katika Ofisi za Uhamiaji. Juzi tu kuna mgeni tulimkamata ana wiki mbili hajaripoti katika Ofisi za Uhamiaji na tukaweza kumpeleka katika Ofisi za Uhamiaji. Je, Waziri ana mpango gani kwa sasa hivi kuweza kuidhibiti hiyo hali au kuiondoa kabisa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kumshukuru Mheshimiwa Nassoro Rashid Nassoro, kwanza kwa uzalendo wa kujua na kuifanyia kazi Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hususan kwa kuwa mlinzi wa eneo ambalo unatoka.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili naomba nikuhakikishie kuwa eneo hilo ni la kimkakati, ni kati ya shehia ambazo zipo kwenye eneo ambalo watalii wengi sana wanakuja. Nikuhakikishie kwamba nitaongeza idadi ya askari ambao watakuja kushirikiana na viongozi wote wa shehia ili kuweza kufanya doria na kuimarisha vipenyo vyote ambavyo kuna uwezekano wa hao wanaokuja kuingia na kutoka bila kufuata utaratibu.

Mheshimiwa Spika, pia tutaendelea kuwachukulia hatua wote ambao watapatikana kadri ya vile ambavyo itathibitika kuwa wameingia na kutoka bila kufuata utaratibu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana. Kwanza ninakushukuru wewe hutoi maelekezo, unaongeza mwenyewe, hongera sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Amosy.

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Sikonge ni miongoni mwa wilaya za zamani, lakini mpaka hivi sasa hatuna Ofisi ya Uhamiaji. Hivi sasa watendaji wa Ofisi hii ya Uhamiaji wapo katika kijumba kidogo sana na wanafanya kazi katika mazingira magumu kweli. Je, ni lini sasa Serikali itaona haja ya kwenda kujenga kituo cha Uhamiaji katika Wilaya ya Sikonge? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kuimarisha miundombinu ya utoaji huduma kwa Askari wa Idara hii ya Uhamiaji, hususankwenye upatikanaji wa Ofisi za Mkoa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, naomba nikuhakikishie, bajeti ya 2026/2027 moja kati ya vipaumbele vyake ni kuweka bajeti kwa

ajili ya ujenzi wa ofisi hizi. Sasa katika Wilaya ya Sikonge ninaomba tuipe kipaumbele kwa ajili ya upatikanaji wa ofisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Happiness Ngwando.

Na. 57

**Ujenzi wa Barabara za Mipakani**

**MHE. HAPPINESS D. NGWANDO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza barabara za usalama mipakani ili kuwezesha vyombo vya ulinzi na usalama kufanya doria?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Happiness Daniel Ngwando, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara za usalama mipakani ni barabara zinazoambaa na mipaka ya nchi yetu kwa ajili ya kuwezesha vyombo vya usalama kuimarisha ulinzi na usalama mipakani. Kwa kutambua umuhimu wa barabara hizi, Serikali inaendelea kuzijenga kwa kiwango cha changarawe ili ziweze kutumika na vyombo vya usalama kufanya doria mipakani.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Serikali kupitia *TANROADS* imejenga jumla ya kilometa 1,759 kwa kiwango cha changarawe katika Mikoa ya mipakani. Aidha, Serikali inaendelea kujenga sehemu zilizobaki kwa awamu kwa kiwango cha changarawe kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Happiness.

**MHE. HAPPINESS D. NGWANDO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara hizi zimekuwa na umuhimu sana hasa kwa wananchi wanaoishi mipakani kiuchumi pamoja na ulinzi wao; kwa mfano, tukiongelea Dapoli - Mbinga, Mitomoni Songea, Magazini - Namtumbo kuelekea Wenje na Nalasi – Tunduru, je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka fedha kwa haraka ili kuzuia watu wabaya na wahalifu ambao hawaitakii mema nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Barabara ya Mtwara - Pachani kuelekea Nalasi Lingusenguse imefanyiwa upembuzi yakinifu kuanzia mwaka 2022 na usanifu wa kina. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwenye barabara hiyo ukizingatia ni barabara ambayo wananchi wake wanalima ‘pesa’ nikimaanisha inalima korosho pamoja na ufuta, lakini kilometa 200 kutoka kwenye hospitali ya Kata moja mpaka kufika kwenye Wilaya ndiyo mama mjamzito anaweza kufika huko?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali haioni umuhimu wa barabara hii kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma hususan Wilaya ya Namtumbo na Tunduru? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi, kipaumbele cha kwanza kwa barabara za mipakani ni kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa salama, kwa maana ya kusaidia vyombo vya usalama kuweza kupita muda wote inapohitajika na ndiyo maana tunaziimarisha, pale ambapo hatujazifungua, tunahakikisha kwamba tunazifungua.

Mheshimiwa Spika, ninatambua pia zikishajengwa inakuwa ni msaada mkubwa kwa wananchi ambao wanazitumia hizo barabara kwa shughuli zao za kawaida ikiwa ni pamoja na kiuchumi na za kijamii. Kwa hiyo, nimhakikishie Mbunge kwamba, Serikali kama tulivyosema, tutaendelea kuziimarisha na kuzifungua na kuhakikisha kwamba zinapitika muda wote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, ni kweli kwamba tuna barabara hiyo ya Mtwara - Pachani - Nalasi kwenda Tunduru

yenye urefu wa kilometa 300, barabara ambayo tumeshakamilisha usanifu, lakini imekuwa ikiombewa fedha, na kwa kuwa bajeti bado haijaruhusu kuijenga barabara yote, tunachofanya kwanza ni kuhakikisha inapitika muda wote na maeneo yote yale korofi, tunachokifanya sasa hivi ni kuhakikisha kwamba tunajitahidi kujenga ama zege, ama lami, ama kama kuna daraja ambalo limekwama, huo ndiyo mkakati ambao tunasema tuijenge ili iweze kupitika kwa muda wote, tukiwa tunatafuta fedha kuijenga barabara yote kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza niwape pole sana wananchi wa Wilaya ya Rungwe kwa maporomoko makubwa yaliyotokea, yaliyosababishwa na mvua iliyopelekea ndugu zetu 21 kutangulia mbele ya haki, '*ndaga wana Rungwe, ndaga mgonie upepo.*'

Mheshimiwa Spika, mvua ile ilisababisha kuporomoka kwa daraja kubwa sana liitwalo Lubangalala. Daraja hilo linaunganisha Kata kwa upande wa Rungwe Kata ya Ikuti, Lupepo, Iponjola, Kyimo na Kiwira. Daraja hilo pia linaunganisha na Wilaya ya Ileje ambalo Kata za upande wa Ileje ni Kata za Ngulugulu, Ngulilo, Sange, Lubanda na Luswisi.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali baada ya kuona daraja hilo ni la muhimu, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ilituma fedha kwa haraka ili kuhakikisha daraja hilo linajengwa. Je, ni lini daraja hilo litakamilika kwa umuhimu huo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kwanza nami niungane na Mbunge kuwapa pole sana wananchi wa Mkoa wa Mbeya na hasa Wilaya ya Rungwe ambao walipata changamoto ya maporomoko kutokana na kunyesha kwa mvua kubwa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara hiyo ambayo inatoka Ileje kwenda Rungwe kuna daraja lilikatika ambalo lilikata mawasiliano kati ya Wilaya hizo mbili. Kilichofanyika kwanza, ilikuwa ni kujenga kivuko cha dharura walau watu wapite kwa miguu na baada ya hapo Serikali baada ya kuona changamoto hiyo iliwapa maelekezo Meneja wa Mkoa wa Mbeya kuhakikisha kwamba anarejesha mawasiliano haraka.

Mheshimiwa Spika, tunavyoongea hivi, daraja la muda ambalo litapitisha magari mpaka jana limekamilika. Kwa hiyo, tuna hakika baada ya muda mfupi, baada ya taratibu zote za kihandisi itakapokuwa imekaa, wataanza kupita kwenye hilo daraja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumechukua hatua kwa haraka kuhakikisha kwamba tunaunganisha mkoa wa Mbeya na Songwe lakini pia Wilaya ya Ileje na Wilaya ya Rungwe ambayo ni muhimu sana hiyo barabara kwa maisha yao. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Barabara ya kutoka Rangitatu, Majimatitu mpaka Mbande ni barabara ambayo imezidiwa sana na msongamano wa magari, kiasi kwamba mpaka bodaboda sasa zinapanga foleni. Je, Serikali ina mpango gani wa kuipanua barabara hiyo ili wananchi waweze kupita kwa urahisi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Jiji la Dar es Salaam, sehemu kubwa ina misongamano mikubwa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tumeshafanya *study* ya kuhakikisha kwamba sehemu zote ambazo zina changamoto zinajengwa upya, kwa maana ya kuongeza upana wa barabara ama kufanya njia nne.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Dar es Salaam, hasa wa maeneo ambayo ameyataja Mheshimiwa Chaurembo, nayo ni maeneo

ambayo tayari yameshafanyiwa *design,* kwa maana ya kuijenga kwa njia nne ama kuipanua ili iweze kupunguza foleni ambayo ipo katika hayo maeneo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Christina Mndeme.

**MHE. CHRISTINA S. MNDEME:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imekuwa ikiendelea kuboresha miundombinu ya barabara nchi, je, Serikali ina mango gani wa kujenga barabara kwa kiwango cha Puge kwenda Ziba mpaka Choma ili kuwaondolea changamoto ya ubovu wa barabara wananchi na hususan wanawake wanapokwenda kupata huduma za afya katika Hospitali ya Rufaa ya Nkinga iliyopo Wilayani Igunga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, hii barabara ilikuwa kwanza haijafanyiwa usanifu, tulikuwa tunakamilisha usanifu. Pamoja na hayo, tulishapata kibali cha kuanza kujenga walau kwa awamu, na tutaanza pande zote mbili. Tulikubaliana hivyo, tuanze pande mbili, huku na huku. Hivi ninavyosema, sasa hivi tunaanza na kilometa 12 kujenga kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, kibali kilishatolewa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bonnah Kamoli.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninataka nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri, je, wana mpango gani na barabara ya Kinyerezi ambayo inapita Bonyokwa ambayo wameanza kutengeneza, lakini sasa haiko kwenye matengenezo na mkandarasi hayupo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninachofahamu ni kwamba, huyu mkandarasi ameshalipwa fedha, na mkandarasi ambaye yuko *site* ndiye anayetakiwa afanye hayo matengenezo, kwa sababu ni suala la kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue nafasi hii kumwelekeza Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Dar es Salaam ahakikishe anasimamia; na kwa kuwa mvua zinanyesha,

ahakikishe anamsimamia mkandarasi na kufanya marekebisho, ikiwa ni pamoja na kukarabati *diversion* ili wananchi wa eneo hilo waweze kupita kwa amani na usalama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Edibily Kinyoma.

**MHE. EDIBILY K. KINYOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itaanza kujenga Barabara ya Uvinza – Kasulu kwa kiwango cha lami, ikizingatiwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni kweli Barabara ya Uvinza kwenda Kasulu ina kama kilometa 60 hadi 62. Tumeshakamilisha usanifu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi ya Mheshimiwa Rais ni kipaumbele. Sisi kama Wizara ya Ujenzi na *TANROADS* tumeichukulia hii barabara kwa kipaumbele kikubwa sana, kwa sababu ndiyo barabara ambayo inatoka Tunduma – Sumbawanga – Mpanda – Uvinza – Kasulu – Kibondo hadi Nyakanazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninavyoongea sasa hivi, hicho kipande ndicho pekee ambacho kitakuwa kimebaki hakijajengwa kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali inatafuta fedha ili kuhakikisha kwamba hicho kipande tumekikamilisha ili tuweze kukamilisha hiyo barabara yote ambayo ni *T*9.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed.

Na. 58

**Kusaini Mkataba wa Kuchakata Gesi Asilia – Lindi**

**MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED** aliuliza: -

Je, lini Mkataba wa kuchakata Gesi Asilia *(LNG)* Lindi utasainiwa na kuanza utekelezaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Kijakazi Yunus Mohamed, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali na wawekezaji wa mradi wa kuchakata gesi asilia *(LNG)* Mkoani Lindi wapo katika hatua ya mwisho ya majadiliano, hususan kwenye masuala ya kisheria ili kuwezesha usainishaji wa mikataba na makubaliano, na hatimaye utekelezaji wa mradi kuanza. Aidha, wabia wa mradi wameendelea na miradi ya kijamii ikiwemo ujenzi wa Shule ya Msingi Mpya ya Likong'o ambayo ujenzi wake umefikia 90%.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kijakazi.

**MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini tulimsikia pia jana Mheshimiwa Waziri Mkuu akitoa maelezo yanayofanana na haya. Ningependa kufahamu, au ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mosi, kama ilivyoeleza Serikali kwamba wako kwenye majadiliano ambayo yanaelekea ukingoni kwenda kusainiwa kwa mkataba, je, Serikali imeweka mkakati gani wa kuhakikisha kwamba wanatoa elimu, sambamba na uwezeshaji kwa wananchi wa Tanzania hususan wanawake wa Mkoa wa Lindi pamoja na vijana ili kuhakikisha kwamba wanaweza kuzipata fursa, hususan zile zinahusiana na sheria ya *local content* ili waweze kunufaika na mradi huu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Mwaka 2023/2024 Wizara ya Nishati iliingia makubaliano na Wizara ya Elimu kupitia *Arusha*

*Technical College* kwa ajili ya ujenzi wa chuo kitakachofundisha masuala ya nishati na mafuta; na Halmashauri ya Manispaa ya Lindi ilitoa eneo lenye ukubwa wa *square meter 256,000* katika eneo la Kikwetu pale Lindi. Kwa mujibu wa makubaliano, ilikuwa ujenzi wa chuo kile ujengwe haraka iwezekanavyo,...

**SPIKA:** Mheshimiwa twende kwenye swali lako.

**MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED:** ...lakini mpaka sasa bado ujenzi haujaanza, ningependa kufahamu, je, ni lini ujenzi wa chuo kile utaanza? La, kama Serikali haipo tayari, kwa nini, isirejeshe eneo lile kwa manispaa ili waendelee na shughuli nyingine, ikiwemo kuuza maeneo yale ili manispaa iweze kupata mapato?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Kijakazi Mohamed, almaarufu Binti Lindi kwa kazi kubwa anayoifanya ya kufutilia mradi huu wa *LNG*. Ninajua kuwa anafanya hivyo kwa sababu anajua kuwa huu ni mradi wa kihistoria ambao ukifanikiwa kuanza mikoa ya kusini itabadilika sana kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza, linahusiana na kuwajengea uwezo wanawake na wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara. Sasa Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, inaendelea kutoa elimu kupitia *VETA, SIDO* na vyuo vingine, lakini pia kuna ujenzi mkubwa wa shule ya amali unaendelea kwa ajili ya kutoa elimu juu ya namna ambavyo wananchi wanaweza kuchangamkia fursa zitokanazo na mradi huu wa *LNG* ambao utaanza hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na chuo cha elimu ya juu ambacho Mheshimiwa Mbunge amekitaja, ni kweli. Kwanza tunawashukuru Wanalindi kwa kutoa eneo kwa ajili ya ujenzi wa chuo hiki; na hii ni kwamba elimu juu ya uchakataji wa mafuta na gesi bado ni jambo geni kidogo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza kwa hilo, na Serikali ina nia ya dhati ya kuhakikisha kwamba chuo hiki kinajengwa ili

wananchi waweze kupata ujuzi na kushiriki katika mradi huu wa kimkakati na tutafanya hivyo kwa kadri ambavyo upatikanaji wa fedha utakavyowezekana. Ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Premji.

**MHE. ARIF S. PREMJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Tunaongelea Mradi wa *LNG* wa shilingi trilioni 100. Chombo cha habari cha *Citizen* na *Reuters* ya London vilichapisha habari tarehe 27 mwezi wa kwanza mwaka huu; na kwenye habari hiyo ilimnukuu mmoja wa Waziri akisema kwamba mkataba utasainiwa mwisho wa mwezi wa Sita. Jana tumesikia kwamba kuna majadiliano bado. Je, ni ipi kauli rasmi ya Serikali kuhusiana na kusainisha mkataba huo? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Mbunge. Kama ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa kauli jana, na kama ambavyo majibu yangu ya msingi ya swali hili nimeyaeleza hapa leo mbele ya Bunge hili Tukufu, mradi wa *LNG* upo katika hatua za mwisho za kukamilisha makubaliano ya kisheria na ya kimkataba ili waweze kusaini mikataba na kuanza mradi huu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea Wizara ya Afya, Mheshimiwa Erick Shigongo.

Na. 59

**Chanjo ya Homa ya Ini kwa Watanzania**

**MHE. JOHN F. NZILANYINGI K.n.y. MHE. ERICK J. SHIGONGO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatoa chanjo ya homa ya ini kwa Watanzania wote?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge wa Buchosa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, chanjo ya ugonjwa wa homa ya ini inatolewa nchini kama sehemu ya ratiba ya chanjo za watoto wachanga, ambapo mtoto hupatiwa chanjo hiyo muda mfupi baada ya kuzaliwa, pamoja na kutolewa kwa makundi maalum yaliyo katika hatari zaidi, wakiwemo watoa huduma za afya na makundi mengine yenye uwezekano mkubwa wa kuambukizwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Chanjo ya Homa ya Ini inatolewa katika Hospitali za Taifa, kanda, mikoa na hospitali zote za wilaya na halmashauri, ambapo mwananchi anaweza kupata chanjo hiyo baada ya kupimwa na ikibainika hana virusi vya Homa ya Ini aina B hupewa chanjo hiyo ambayo hutolewa kwa dozi tatu kwa vipindi tofauti.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeunda timu ya wataalamu kwa ajili ya kuandaa andiko litakalotoa mwelekeo na maoteo ya gharama zinazohitajika kutekeleza lengo la kutoa huduma ya Chanjo ya Homa ya Ini kwa Watanzania wote. Mara litakapokamilika hatua za utekelezaji wa maoni ya maandiko hayo yataweza kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Sika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shigongo.

**MHE. JOHN F. NZILANYINGI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Erick Shigongo, Mbunge wa Jimbo la Buchosa, ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto yanazidi kuongezeka na hii ni kwa sababu chanjo hii ya

homa ya ini hutolewa miezi sita baada ya mtoto kuzaliwa; na hivyo watoto wengi wanapata maambukizi haya katika kipindi cha miezi kuanzia sifuri mpaka miezi sita. Je, Serikali haioni haja ya kuanza kuitoa chanjo hiyo mapema tu pindi mtoto anapozaliwa, kama ambavyo nchi nyingi duniani zinafanya?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Gharama za chanjo hii zinaonekana kuwa kubwa kwa Watanzania. Je, Serikali haioni haja ya kuziweka kwenye bima ya afya ili watoto wengi na wananchi wengi waweze kupata huduma hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuuliza maswali ya nyongeza kwa Mheshimiwa Shigongo ambaye amekuwa kinara wa kupambana na ugonjwa wa homa ya ini katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaomba nikuthibitishie, chanzo ya homa kwa mtoto inatolewa mara tu baada ya mtoto kuzaliwa na siyo baada ya miezi sita. Kwa hiyo, hakuna takwimu zinazoonesha kwamba maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto yanaongezeka kutokana na chanjo.

Mheshimiwa Spika, chanjo hii ya mtoto inatolewa bure na Serikali, na chanjo hii imeanza kutolewa tangu mwaka 2002. Hiyo kuchangia, kwamba watoto wote waliozaliwa mwaka 2002 hadi leo, kwa maana ya watoto wa mwaka mmoja hadi 24 wamekingwa kuambukizwa na ugonjwa wa homa ya ini. Chanjo hiyo hutolewa bure kwa watoto wote hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, kuhusu gharama ya chanzo. Kwanza kabisa hapa niaipongeza Serikali ambayo kwa makusudi kabisa ilileta chanjo kwa watu wazima, kwa maana sasa ni wale wa umri wa 25 na kuendelea ambao hawakupata ile chanjo ya utoto. Chanjo hii inatolewa katika hospitali zote baada kuwa umepimwa na kuthibitisha kwamba huna chanjo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa makusudi kabisa iliwalipia watalaamu wote wa afya kupata hii chanjo ya homa ya ini bure nchini ili wasiweze kupata maambuziki kwa sababu wako katika hatari. Hata hivyo, wale ambao wanajilipia gharama ya chanjo ni shilingi 10,000 kwa sindano moja ya chanjo hiyo ya homa ya ini. Serikali imeshaanzisha rasmi huduma ya Bima ya Afya kwa Wote ambayo tumeshaanza utekelezaji wake kwenye Kundi la *pilot*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, lengo la Serikali na lengo la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha kwamba Watanzania wote wanakuwa na afya njema. Kwa kupitia bima ya afya, hakuna mwananchi atakayebaki nyuma bila kupata huduma hii ya chanjo.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwaasa Watanzania wote waende hospitalini wakapime, wakajue hali yao ya homa ya ini, kwa sababu changamoto kubwa ni kwamba mpaka sasa chanjo hiyo ya homa ya ini kwa watu wazima *uptake* yake ni ndogo, Watanzania hawaendi kuchanja ilhali chanjo hiyo ipo. Kwa hiyo, waende wakachanje kwa sababu ipo na hospitali zote nchini zinatoa hiyo chanjo. Ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kuniona. Ugonjwa huu wa homa ya ini kwa Watanzania wengi unaonekana kama ni ugonjwa mgeni ambao haujafahamika sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kwa Watanzania walio wengi kwa ugonjwa huu hatari ili waweze kufika kwenye vituo vya afya ama kwenye hospitali zetu ili waweze kupimwa na ikigundulika waweze kupatiwa tiba ama kupatiwa chanjo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza ninampongeza Mheshimiwa Hawa kwa kuwa alilolisema ni suala dhahiri kabisa. Watanzania wengi wanaona kwamba ugonjwa huu wa homa ya ini hauwahusu, lakini nikuhakikishie,

kwamba takwimu zinaonesha *prevalence* ya ugonjwa huu katika nchi hii ni asilimia tatu nukta tano ya Watanzania wana ugonjwa huu. Iko mikoa ambayo iko juu sana kama Katavi, Rukwa, Kigoma, na Geita, imefika mpaka asilimia sita, nne, ambapo wako juu ya kiwango cha nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa wajawazito takwimu zinaonesha *prevalence* ni asilimia saba. Kwa hiyo, hili tatizo la homa ya ini ni tatizo katika nchi hii, na ni tatizo dunia nzima. Katika Afrika nzima watu milioni 60 wanaishi na tatizo hili la homa ya ini. Kama Wizara ya Afya kupitia Kitengo cha Kutoa Elimu ya Afya tumeendelea kuwaelimisha Watanzania, waende hospitalini wakaangalie afya zao na kujua kama wameathirika ili waweze kupata chanjo au tiba; na hasa ni *Hepatis B* ambayo imeonesha uwezekano mkubwa wa kusababisha kwanza kuleta ugonjwa wa ini wa kudumu ambao unaweza kupelekea mpaka ini kushindwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuwaasa Watanzania wote, tukiwemo sisi wenyewe Wabunge twende tuka-*check* hali zetu za homa ya ini. Ugonjwa huu upo na unaathiri Watanzania wengi. Chanjo ipo na tiba ipo. Kwa hiyo, tukapime. Kinga ni bora kuliko tiba.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Stella Ikupa.

Na. 60

**Dawa kwa Wagonjwa wa Akili Wenye Ulemavu**

**MHE. STELLA I. ALEX** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Wagonjwa wenye Ulemavu wa Akili wanapata Dawa bure kwa kuwa siyo wote wana Bima ya Afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza Sera ya Afya ya Mwaka 2007 inayoelekeza kutoa huduma za msamaha wa gharama za matibabu kwa watu wasio na uwezo na wenye magonjwa sugu kama saratani, UKIMWI, kisukari pamoja na wagonjwa ya akili.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshatangaza rasmi kuanza kwa utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote awamu ya kwanza, itakayohusisha makundi ya wananchi ikiwa ni pamoja na watoto, wajawazito, walemavu na wengine wasio na uwezo, ambapo kundi hili litagharamiwa na Serikali. Kukamilika kwa hatua hii kutawawezesha wananchi, wakiwemo walemavu wenye tatizo la afya ya akili kupata huduma pasipo kuwa na kikwazo cha fedha.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ikupa.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Nitumie nafasi hii kumshukuru sana Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo anaendelea kulijali kundi hili la watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, tunaona kuwa, katika siku za kwanza 100 za uongozi wake amewezesha kundi hili la watu wenye ulemavu kuwa kwenye huu mpango mzima wa Bima ya Afya kwa Wote. Pamoja na haya mazuri, ninaiomba Serikali iendelee kuwatambua watu wenye ulemavu wasiokuwa na uwezo wa kugharamia matibabu ili waendelee kunufaika na mpango huu.

Mheshimiwa Spika, pia, ninaiomba Serikali, majibu haya mazuri ambayo yameongelewa hapa kuwe kuna utaratibu mzuri wa kufuatilia utekelezaji wake kwa sababu huku *site* hali siyo nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuwe kuna ufuatiliaji wa haya ambayo yamezungumzwa ili sasa kundi hili la watu wenye ulemavu na hasa hawa wagonjwa wa akili waweze kupata hizi dawa kwa wakati kwa sababu wasipozipata kwa wakati, wanafanya mambo ambayo yanakuwa hayana staha katika jamii yetu. Vilevile, wanashidwa kuendesha maisha yao kwa maana ya kushindwa kufanya kazi za msingi za kimaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Naibu Waziri apange muda ili sasa aweze kukutana na kundi hili na aweze kusikia kutoka kwao wao wenyewe, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante kwa ushauri. Mheshimiwa Naibu Waziri ninafikiri alikuwa anatoa ushauri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nimeupokea ushauri.

**SPIKA:** Hongera kwa kazi nzuri.

Waheshimiwa Wabunge, maswali yetu yamekwisha. Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Kwanza ni wageni waliokaa Jukwaa la Spika. Tunao wageni 14 Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wakiongozwa na Ndugu Charles Kichere, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Salvina Mkumba, Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mkaguzi Taasisi za Umma; Ndugu Wendi Masoi, Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; na Ndugu Benja Majura, Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ukaguzi wa Hesabu. *(Makofi)*

Vilevile, yupo Ndugu Kubela Mwakatundu, Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Serikali za Mitaa; Ndugu George Haule, Naibu Mkaguzi Mkuu, Ukaguzi Ufanisi wa Kiufundi; Ndugu Aziz Dachi, Afisa Masuuli; Ndugu Nobert Mfalamagoha, Mkurugenzi wa *Division* ya Utawala na Rasilimali Watu; na Ndugu Elibariki Lyatuu, Mkuu wa Kitengo cha Uratibu Shughuli za *CAG* Bungeni. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Fausta Othmani, Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Kiufundi; Ndugu Gabriel Mtengo, Msaidizi wa CAG; Ndugu Focus Mauki, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano; Ndugu Seleman Mwamba, Mkuu wa Kitengo cha Mipango; na Ndugu Patrick Bwelindo, Mkaguzi Mkuu wa Nje, Ofisi ya Bunge. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Salehe Mbwana Mhando, ni Viongozi wa Wilaya ya Kilindi Mkoani Tanga, karibuni. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Khalid Mussa Nsekela, ni Wapigakura wake kutoka Jimbo la Kyerwa Mkoani Kagera. *(Makofi)*

Wengine ni wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wapo Wajumbe watano kutoka kwenye Kamati Tendaji ya Muungano, Makampuni ya Ulinzi Tanzania.

Wapo wanafunzi 90 na walimu wawili kutoka Shule ya Sekondari Dodoma.

Pia wapo wanafunzi 195 na walimu 15 kutoka Shule ya Awali ya Msingi ya Feza Jijini Dodoma, karibuni, hongereni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ninamwita Mwenyekiti Mheshimiwa Paresso aendelee na kikao.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Cecilia D. Paresso) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**10 APRILI, 2026**

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu Mwaka wa Fedha 2026/2027

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano na mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Charles Mhando Njama, ajiandae Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Jason Samson Rweikiza.

**MHE. CHARLES M. NJAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia hoja hii, ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema ambaye amenibariki kupata nafasi ya kushiriki katika Bunge hili Tukufu kuwawakilisha wananchi wa Jimbo la Korogwe Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nikishukuru Chama changu Cha Mapinduzi chini ya uongozi wa Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniteua kati ya wengi kuwa mgombea wa Chama cha Mapinduzi katika Jimbo letu la Korogwe Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninawashukuru sana wananchi wa jimbo langu la Korogwe Mjini ambao wamenipa imani kubwa, ambao wameniunga mkono kwa kura nyingi katika uchaguzi uliofanyika Oktoba 29. Imani waliyonipa nami ninawaahidi nitawalipa kwa kufanya kazi usiku na mchana kuhakikisha kwamba tunatetea maslahi ya Jimbo la Korogwe Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeze Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo anatekeleza majukumu yake na hasa kwa namna alivyotekeleza ahadi zake alizoziweka kwa ajili ya siku 100 za kwanza katika uongozi wake. Hakika mama ameamua kuitumikia nchi na tunaona akifanya

kwa vitendo na Mungu ambariki azidi kumpa afya njema aendelee kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa namna ambavyo anaendelea kufanya kazi usiku na mchana pasipo kuchoka. Vilevile, tunamshukuru kwa ziara alizozifanya katika maeneo mengi ya nchi hususan sisi Wabunge wa Mkoa wa Tanga kwa namna ambavyo ziara yake aliyoifanya katika mkoa wetu wa Tanga imeleta tija kubwa na imeleta mwamko na uwajibikaji kwa watumishi wa Serikali katika Mkoa wetu wa Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Jimbo la Korogwe Mjini wanamwomba, kwa kuwa katika ziara yake hawakupata nafasi ya kutoa kero zao kwa sababu kwa bahati mbaya ratiba haikuruhusu kuwa na wakati wa maswali alipokuwa katika eneo la Mswaha, basi wakati mwingine akipita atenge muda wa kukutana na wananchi wa Korogwe Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mkuu wangu wa Mkoa Dkt. Batilda Buriani kwa namna ambavyo anaendelea kufanya kazi kwa maslahi mapana na maendeleo ya Mkoa wa Tanga, na pia Mwenyekiti wetu wa Chama Ndugu yetu Rajabu Abdallah kwa namna ambavyo amekuwa kinara wa kuhakikisha duka la Mkoa wa Tanga linaendeshwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hakika katika awamu yake ya uongozi, miradi mingi mikubwa ya maendeleo imetekelezwa katika jimbo letu la Korogwe Mjini. Tumeona shule nyingi za sekondari zikiwa zimejengwa katika jimbo letu la Korogwe Mjini, tumeona sasa hivi ujenzi wa barabara ya *TACTIC* kilometa 10.4 ukiwa unaendelea na tunatazamia kabla ya mwisho wa mwaka huu, ujenzi ule utakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi ule utakwenda kubadili sura na mwonekano wa jimbo letu la Korogwe Mjini. Tutakuwa tunakwenda kupata barabara za lami, lakini pia taa za barabarani pamoja na mifereji, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imejaa matumaini makubwa kwa wananchi, imejaa nuru kwa wafanyabiashara, lakini vivyo hivyo pia matarajio ya maendeleo katika maeneo mengi na nyanja tofauti tofauti katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwa upande wa Jimbo letu la Korogwe Mjini tunapoongelea mageuzi ya kiuchumi na ongezeko la ajira, tuna vitu kadhaa ambavyo kwetu ni kipaumbele. Katika ziara ya kampeni ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alivyopita katika jimbo letu la Korogwe Mjini tulimwomba na aliridhia ujenzi wa bandari kavu katika Jimbo la Korogwe Mjini katika eneo letu la Kata ya *Old Korogwe*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari kavu hii ina maana kubwa sana katika uchumi wa watu wa Korogwe. Bandari kavu hii itakwenda kupunguza *congestion* ya malori katika barabara ya Tanga – Segera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari kavu hii itakwenda kuongeza mzunguko wa fedha kwa wafanyabiashara wadogo wadogo, na wa kati katika Mji wetu wa Korogwe Mjini. Kwa hiyo, tunaomba, katika bajeti itakayoletwa, tuone utekelezaji wa ujenzi wa bandari kavu katika mji wa Korogwe, kwa sababu kwetu sisi hii inakwenda kukuza uchumi na kuongeza ajira kwa vijana wa Korogwe Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ilipitisha ujenzi wa bonde la umwagiliaji katika Kata yetu ya Kwamsisi kwa takribani shilingi bilioni 24.5 na pia, katika Kata ya Kwamndolwa kwa takribani shilingi bilioni nne. Ujenzi ule hauendelei kwa sasa. Tunaomba katika bajeti ya kilimo itakayokuja, basi miradi hii ioneshwe namna gani inakwenda kutekelezwa katika kipindi cha bajeti hiyo inayokuja kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nayo inakwenda kuchochea uchumi na uzalishaji wa mazao ya chakula pamoja na mbogamboga katika maeneo yetu ya Jimbo la Korogwe Mjini.

Miradi hii ina tija kubwa, ninaomba tuipe kipaumbele cha juu ili kuhakikisha tunakwenda kuitekeleza na kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Kwamndolwa umekaa kwa muda mrefu, wakandarasi wameenda pale zaidi ya watatu wakiwa wanabadilishwa badilishwa kwa kushindwa kutekeleza mradi ule. Sasa wananchi wa Kata ya Kwamndolwa hawana imani kama kweli ahadi iliyowekwa itakwenda kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa imani yangu kubwa tuliyokuwanayo kwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Waziri mahiri wa Kilimo tunaamini mradi ule unakwenda kutekelezwa na ninaomba upewe kipaumbele cha kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba alipofanya ziara yake Mkoa wa Tanga tulimwomba kuhusiana na hospitali yetu ya Magunga. Kutokana na eneo iliyopo, Hospitali ya Magunga inahudumia watu wengi na siyo tu wakazi wa Jimbo la Korogwe Mjini, bali Wilaya za Lushoto, Handeni, na maeneo ya karibu ya Wilaya ya Muheza wote wanapata huduma hapa. Siyo hayo tu, kwa sababu ipo katikati ya barabara kubwa, wagonjwa wanaotokana na ajali za barabarani wengi wamekuwa kimbilio lao la kwanza ni Hospitali ya Magunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali hiyo imekuwa kongwe kwa kuwa imejengwa tangu mwaka 1952, na sasa ina umri wa miaka zaidi ya 73. Tuliomba hospitali ile ijengwe upya na tunashukuru Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imetuletea shilingi bilioni moja ambayo tunatazamia kuanza ujenzi wa *maternity complex.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa badala ya kuweka viraka katika hospitali ile, bajeti ya mwaka huu 2026/2027 na kuendelea, sasa iwekwe angalau kila mwaka tupate jengo moja kubwa jipya ili baada ya miaka mitatu au mitano tuwe tumepata majengo yote mapya ya Hospitali ya Magunga, iendane na

hadhi ya ukuaji wa Mji wa Korogwe, na pia uendane na barabara hii sasa ambayo tunaitoa kutoka *NMB* kwenda katika Hospitali ile ya Magunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika upande wa barabara pamoja na kupata kilometa 10.4 za *TARURA* kupitia *TACTIC,* na bado jimbo letu lina changamoto kubwa sana ya barabara. Hivi tunavyoongea, na mvua zinazoendelea katika Mkoa wa Tanga Kata zetu za Mtonga, Bagamoyo, na Kilole miundombinu yake haipitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba wenzetu wa TAMISEMI katika bajeti yao watutengee angalau kuongeza kilometa 10 - 15 za changarawe katika Jimbo la Korogwe Mjini. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumepunguza changamoto ambazo watakuwa wanazipata.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. CHARLES M. NJAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tukumbushane, kuwa mzungumzaji anapoongea, kanuni zetu hazituruhusu tupite mbele yake. Hairuhusiwi kukatisha kati ya Kiti na mzungumzaji, ninaomba tuzingatie hilo.

Nilimtaja Mheshimiwa Ester Amos Bulaya na Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza ajiandae.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara muhimu ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabla sijaanza kuchangia Wizara ya TAMISEMI, wananchi wa Bunda Mjini wamechoka kusikia Habari ya mchakato unaendelea kuhusiana na mradi wa *TACTIC*. Wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini wanaungana na Rais

wao Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba wanahitaji matokeo, wanataka stendi ya kisasa, barabara za lami, na wanahitaji soko la kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kumsaidia Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Sisi tutawaunga mkono hasa kwa *style* ya Waziri Mkuu wetu ya kukemea uzembe, kuhitaji uadilifu na uchapakazi. Hayo yote ndiyo yataenda kufanya Dira yetu ya 2025 - 2050 iweze kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, ninyi na mimi tutakubaliana kwamba nchi yetu inapiga hatua. Tunajenga miradi mbalimbali, tunajenga shule, na tunajenga hospitali. Hivi tumeshajiuliza, tutalindaje hii miradi ili vizazi na vizazi waweze kuviona?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu bado hatujawa na utaratibu wa kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati *(maintenance)*. Pia, ninyi mnajua, nyumba yako tu unayoishi, ukiijenga ukaiacha, baadaye ikachakaa, itakupa gharama kubwa kuirudisha katika ubora wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nimetoka Dar es Salaam, kila unapopita *construction* zinaendelea za miundombinu mbalimbali. Hivi tumekujaje? Tumejiuliza hii miundombinu tutaitunzaje ili ibaki katika ubora wake? Lazima kama Taifa kupitia Dira hii tunayoiweka ni wakati muafaka wa kutenga fungu maalum tutakalolitafutia chanzo na kukiwekea sheria kwa ajili ya ukarabati na kulinda miradi yetu mbalimbali na miundombinu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninapitia bajeti iliyopita, TAMISEMI peke yake imetekeleza miradi nane ya shilingi trilioni 8.9. Hii miradi tutailindaje? Tutahakikishaje inabaki na ubora na ukizingatia kwenye miradi ya Serikali hasa majengo yanapaswa kudumu kwa miaka 55? Hii miaka 55 *yes*, tutahakikisha inakuwa na ubora, haiwezi ikadumu kama tusipotenga fedha kwa ajili ya ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tuna shule za msingi chakavu 11,000, tuna shule za sekondari chakavu 405, na tuna madarasa chakavu 7,741. Hii tu ni sekta ya elimu, tunahitaji shilingi trilioni 3.8 ili shule hizi 11,000 za *primary*, shule 405 za *secondary* (madarasa) 7,700 zirudi kwenye hali yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu gani? Tuliacha zikachakaa, tumejenga, watoto wametumia, tukasahau kuweka fungu la ukarabati, na hii utaandika historia kuwa Waziri Mkuu wa kwanza utakayeweka historia ya kuhakikisha miundombinu ya Watanzania inalindwa vizuri kwa kutenga fungu maalum kwa ajili ya ukarabati, tukalitungia sheria. Tulinde miundombinu yetu ya barabara tunayojenga, tulinde shule zetu, na tulinde hospitali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo nilikuwa nimetaja sekta ya elimu. Tukija kwenye sekta ya afya, tuna zahanati 1,785 zinahitaji shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima kama Taifa kwenye dira yetu, tuanze kuwa na *culture* ya kuweka fedha kwa ajili ya kulinda miradi yetu mbalimbali ambayo tunaijenga. Hapo nimesema zahanati, ukija kwenye vituo vya afya 534 zinahitajika fedha za ukarabati shilingi bilioni 192.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejenga, tumefanya maendeleo sana, tuna wajibu wa kulinda miundombinu yetu kwa kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati. Tusipofanya hivyo, tutakuwa tunajenga; *yes,* tunasema tumejenga barabara, tumejenga shule, tunapiga hatua kumi mbele, tunarudi sita nyuma, kwa sababu sisi wenyewe tumeshindwa kuweka *mechanism* ya kulinda miundombinu yetu ya kulinda miradi mikubwa tunayoijenga, ya kulinda miundombinu ya shule, ya kulinda miundombinu ya zahanati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapo nimezungumzia hivi vilivyopo, tukija kwenye maboma, maboma ambayo yanahitaji kukamilishwa. Tuna maboma 1,596 ya zahanati: mbali na hizi shule zilizojengwa, mbali ya zilizochakaa, haya maboma kukamilika kwake yanahitaji shilingi bilioni 115, haya tumeyakamilisha,

tunayalindaje ili wananchi wetu waweze kupata huduma kwenye hospitali zilizobora kwenye zahanati zilizo bora? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye hospitali ambazo bado zinahitaji shilingi bilioni 2.4 kwa ajili ya ukarabati, sisi tu kwenye Serikali yetu, tumeweza kukarabati maboma 346 yenye thamani ya shilingi billion 30. Kupanga ni kuchagua, hii kasi ya maendeleo inayofanywa na Serikali yetu chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, lazima tuweke mkakati wa kuhakikisha miradi yote inakuwa na ubora, na kwa kuwa na fungu la ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isipojibu hili, nitashika shilingi, kwa sababu tunataka miundombinu tunayoijenga, shule tunazozijenga, hospitali tunazozijenga zibaki na ubora wake, tuwe na *culture* ya kuhakikisha tunatenga fedha kwa ajili ya ukarabati, na hili linawezekana. Tukiweka nidhamu tu, hata kile tunachokitengea kitumike kwa matumizi sahihi. Hata hivyo, tukienda kwenye culture, kama tunatenga fedha za mfuko wa barabara zipo kwenye *ring-fence* lakini mpaka leo 42% tu wamepokea, haitakuwa na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba sana tulinde miradi yetu, tulinde miundombinu tunayoijenga ili iwe na tija. Vizazi na vizazi, vitakuja kutukumbuka Bunge hili kwenye dira hii ya 2025 - 2030 kwamba, kulikuwa na Bunge, liliamua kuweka utaratibu wa kuhakikisha miradi inayojengwa inabaki kwenye ubora, ili tuweze kupiga hatua kwa namna ambavyo tunataka Taifa letu liende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, narudi Jimbo la Bunda Mjini. Jana, Mheshimiwa Waziri Dkt. Dugange nimempa *document* ya miradi viporo na maboma ya zaidi ya shilingi bilioni 2.4 inahitaji kukamilika kwenye Jimbo la Bunda Mjini, ili wananchi wangu waweze kupata huduma bora za afya, huduma bora ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ester Amos Bulaya kwa mchango wako, nilimtaja Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, ajiandae Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo na Mheshimiwa Haji Amour Haji.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Awali ninapenda kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri ambayo imesheheni mipango mizuri ya maendeleo yetu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa sana anayoifanya kwa kuleta maendeleo nchi yetu ya Tanzania. Anapamba vilivyo kwa juhudi kubwa sana. Sisi ni mashahidi sana kwa kazi zinazofanyika kwenye maeneo yetu, kwenye majimbo yetu, mikoa yetu, kujenga barabara, shule, zahanati, miradi ya maji, miradi ya umeme na mingine mingi ambayo anapambana ili tupate maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kama nilivyosema ilisheheni mipango ya mendeleo na mambo yaliyofanyika na yatakayofanyika. Sasa kwenye maendeleo yoyote changamoto hazikosi. Changamoto zipo mara kwa mara, mara nyingi tu, na ndiyo maana tupo hapa kujadili na kuleta mapendekezo mazuri ya kuboresha maendeleo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamesema Waheshimiwa Wabunge wenzangu hapa, barabara mwaka huu 2026 zimeharibika sana ninadhani kutokana na mvua nyingi nchi nzima, zimechimbika mashimo, lami zimeharibika, *system* zile za udongo vijijini ndiyo kabisa, zimeharibika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inanikumbusha jambo moja kwamba katika mgao wa fedha za *Road Fund (Mfuko wa Barabara),* wanaopewa fedha nyingi ni *TANROADS*. Siyo vibaya, ni vizuri kwamba wanahusika barabara kubwa, madaraja makubwa na wana kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hii isitusahaulishe kwamba kule vijijini ndiyo kuna kazi kubwa sana ya kuzalisha mazao, kupeleka pembejeo, kutoa mazao kule kuyaleta kwenye masoko, na kuna watu wengi sana kule vijijini wanaishi huko. Sasa kuwapa *TARURA* fedha kidogo, inasababisha barabara za kule ziwe mbaya sana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninatoka vijijini, ni Mbunge wa Bukoba Vijijini. Barabara zangu za vijijini zina hali mbaya sana na *TARURA* hawana fedha. Sasa hii inakuwa kidogo ni changamoto kubwa zaidi kwenye upande wa barabara. Ningetamani *TARURA* apewe 70%, *TANROADS* 30%. Siyo kwa kuwafifiza *TANROADS,* lakini tuweke mkazo kwenye barabara za vijijini. Tusionekane kwamba tunapendelea watu wa mijini, barabara za *TANROADS* hizi, tunawasahau wa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA* waongezewe fedha, wapate fedha nyingi, barabara zitengenezwe. Ni za udongo zile ndiyo zinazoathiriwa sana na mvua kuliko za lami. Sasa kama hawawezi kupewa 70%, basi angalau wapewe hamsini, hamsini wote. *TARURA* 50% ya zile fedha, *TANROADS* 50% ya zile fedha, ili tuweze kupata barabara nzuri maeneo yote ya nchi yetu. Hilo ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni la maendeleo. Tuna vijiji vingi nchi hii, tuna ardhi nyingi sana ambayo tunaitumia kwenye kuzalisha vyakula, mazao ya biashara na mengine. Ni jambo jema, lakini ardhi ile thamani yake ni hiyo tu basi, kuzalisha chakula na mazao ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ni kichocheo kikubwa cha maendeleo, ni uchumi mkubwa sana. Tatizo ni kwamba ardhi hii haijapimwa wala kusajiliwa. Tuna mabenki mengi sana Tanzania, zaidi ya 45, mabenki mbalimbali, tukiongozwa na *CRDB* na *NMB* kwa ukubwa. Hizi benki 45 na zaidi zina fedha nyingi sana za maendeleo. Mnaona wanavyokuja hapa tukianza Bunge jipya, wanavyokuwa pale nje getini wanatuita njoo uchukue hela, njoo uchukue hela, wanazo hela nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili benki itoe fedha kwa mtu yeyote, lazima iwe na usalama wa fedha yako. Usalama mkubwa wa kwanza ni ardhi, lakini ardhi ambayo haijapimwa, haijasajiliwa, haina haki, haina thamani yoyote zaidi ya chakula tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninatoa wito kwa Serikali, ardhi hii ipimwe yote Tanzania, ipimwe yote. Tutenge bajeti kubwa, siyo kubwa sana ni kawaida tu. Tayari kila mkoa una masjala ya ardhi, na kila baadhi ya wilaya nyingi tu masjala zipo. Hatua kubwa kwenye kuelekea huko, tuzitumie masjala hizi ili ardhi ipimwe yote, kila mwenye ardhi yake, robo eka, eka kumi, eka mia awe na hati yake, aende benki, achukue fedha, aingie kwenye maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutapata kuchochea uchumi wetu kwa kasi kubwa sana. Watu wataanza miradi ya mbao, kukata mbao, viwanda vya selemara, viwanda vidogo vidogo, kuboresha vyakula vyetu, kuvipeleka hata nchi za nje, wataingia kwenye madini, amesema Mbunge mmoja hapa wachimbaji wadogo, wadogo daima, hawakui kuwa wachimbaji wa kati. Watapata kuchukua fedha benki kama wana hati, wataendeleza uchimbaji wao, tutapata maendeleo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutapima ardhi yetu yote, ikawa na hati, benki zitoe fedha, watu wajiendeleze, wataajiri wenzao, vijana watapata ajira, kwa sababu kutakuwa na miradi mingi, watu wakiwa na fedha kutoka benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni Jimbo langu la Bukoba Vijijini. Ninashukuru miradi ya maji inaendelea na ya umeme na mingine niliyoisema. Hata hivyo, kuna mradi mmoja wa maji pale Kemondo, unaitwa Mradi wa Maji wa Kemondo Maruku. Kati ya kata tano, kata mbili zimepata maji kwa ukamilifu, kata moja kwa sehemu, kata mbili hazijapata maji, ambazo ni Kata ya Maruku na Kata ya Kanyangereko. Sasa ni mwaka wa saba huu, tangu mradi umeanza. Naomba fedha itengwe ipelekwe pale, maji yaende Maruku na Kanyangereko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Jasson Rweikiza kwa mchango wako, nilimtaja Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, ajiandae Mheshimiwa Haji Amour Haji.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Pia ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia uhai na leo kuweza kutoa mchango wangu hapa Bungeni. Nikishukuru chama changu cha Mapinduzi, ninamshukuru Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali yake, Mawaziri wote na Manaibu Waziri kwa kazi kubwa waliyoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimehudumu kwenye halmashauri zaidi ya miaka 15, na huu mwaka wa kumi sasa nipo hapa Bungeni. Katika miaka mitano ambayo Serikali imefanya mambo makubwa ya maendeleo ni miaka hii ya Rais wetu Mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha nyingi za maendeleo zimekuja majimboni mwetu, na kwa wale wanaofahamu historia, Jimbo la Mbagala, Mbunge alikuwa harudi mara mbili. Safari hii nimerudi kwa sababu ya miradi mikubwa iliyofanywa na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. "*Man lam yashkurin-nas, lam yashkurillah*." Asiyemshukuru binadamu mwenziye hata Mwenyezi Mungu hatomshukuru. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala zima la fedha, kwa kweli Serikali imepeleka fedha za kutekeleza miradi ya afya, miradi ya elimu na miradi ya barabara. Miradi ya afya na elimu, majengo yaliyojengwa yanaonekana. Sitaki kuyataja kwa sababu ya muda, lakini sasa hivi kwenye jimbo langu, kuna majengo ya ghorofa ya elimu na afya, tunaendelea kushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio kingi cha Wabunge hapa, pamoja na wananchi wetu tunaowaongoza ni miundombinu ya barabara. Ukipiga hesabu, fedha zilizokwenda kwenye barabara na fedha zilizokwenda kwenye afya na elimu, ukipiga hesabu vizuri, utakuta fedha zilizokwenda kwenye barabara ni nyingi kuliko kwenye afya na elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ukija kwenye matokeo ya fedha za elimu na barabara yanaonekana kwa macho. Elimu na afya yanaonekana kwa macho, lakini matokeo ya fedha zilizoenda kwenye barabara hazionekani. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ndiyo swali la kujiuliza hapo, tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya utafiti kidogo, miaka mitano iliyopita, Halmashauri ya Manisapaa ya Temeke, imepata shilingi bilioni 50 kwa ajili ya barabara. Kwa hesabu za kawaida, shilingi bilioni 50 ni kilometa za lami 50. Ukiacha miradi hii ambayo imekuja kwa ajili ya idadi maalumu ya *DMDP*, nenda katafute kilometa 50 za lami katika Halmashauri ya Temeke. Hii ni kwa Mkoa mzima wa Dar es Salaam, na ikiwezekana kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mapato ya ndani, ndani ya miaka mitano, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke imepeleka shilingi bilioni 20 kwa ajili ya barabara. Nenda katafute kilometa 20 za lami zilizojengwa kwa mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejifunza, fedha hizi tunazipeleka na tukishakuzipeleka, tunazisambaza katika kila eneo kwa uchache sana, kitu ambacho hakikidhi mahitaji ya ujenzi wa barabara wa maeneo hayo. Jana Mheshimiwa Naibu Waziri, alinijibu katika swali langu, alisema pale Kilungule, Mtaa wa Kwa Mwarabu, kilometa 0.88 wametenga fedha shilingi milioni 165.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mita 880 kwa shilingi milioni 165 unaenda kujenga changarawe. Ukiweka changarawe bila mifereji, mwaka unaofuata lazima changarawe ile itaondoka. Ukija mwaka mwingine kuitafuta shilingi milioni 165 huwezi kuiona kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazo baadhi ya barabara ambazo nimepiga hesabu yake, kwa mfano, barabara inayokwenda kule Saku Mwisho ni kilometa 3.6 ndani ya miaka mitano, imepelekewa changarawe na kushindiliwa zaidi ya shilingi bilioni 2.6, lakini sasa hivi barabara haipitiki. Barabara hiyo ingejengwa kwa kiwango cha lami au zege, tungetumia shilingi bilioni tatu, na tusingekuwa tena na uendelezaji wa barabara ile

kwa sababu ilikuwa imekamilika kwa miundombinu yote ya mifereji pamoja na lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali, ukiangalia kwa Halmashauri za Dar es Salaam na Halmashauri za Majiji *trend* ya makusanyo inaongezeka kila mwaka. Kama ndani ya miaka mitano, tumeweza kupata fedha za barabara shilingi bilioni 50, kilometa tano, kwa nini Serikali yetu isiangalie utaratibu wa kutengeneza kilometa 100 za lami, kwa kutafuta wakandarasi sasa na kuwapa kazi, lakini tukawalipa ndani ya miaka sita au saba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo, barabara zitakuwa haziharibiki kwa sababu zitajengwa kwa ubora. Hata hivyo, uwezo wa halmashauri wa kulipa wenyewe upo. Kama ndani ya miaka mitano, halmashauri imepeleka shilingi bilioni 20 kutengeneza barabara, je, barabara kilometa 100 ambazo zitagharimu shilingi bilioni 100 zitaweza kulipwa na halmashauri ndani ya kipindi cha miaka mitano mpaka saba? Tutakuwa hatufanyi tena *sport improvement,* wala *periodic maintenance,* barabara zile zile, kazi yetu itakuwa ni kusafisha mifereji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Serikali iangalie jambo hili. Nikiwa Meya wa Temeke, Mradi wa *DMDP* ambao umekwenda kuzaa miradi hii ya *TACTIC* na miradi mingine; chanzo chake kilikuwa Halmashauri ya Temeke. Baada ya kutakiwa tulipe fidia kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo, tulitakiwa tulipe fidia ya shilingi bilioni 19, halmashauri uwezo wa kulipa shilingi bilioni 19 kwa mara moja haupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukaandika andiko, wapo tuliobezwa, lakini kwa andiko lile tulichukua mkopo *CRDB* shilingi bilioni 16 tumelipa fidia. Mradi wa *DMDP* umejenga barabara za lami, matokeo yake na Kinondoni na Ilala wamefaidika. Kwa kutekeleza mradi huo, leo tunapata mradi wa Rais na miradi mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaomba sana mipango yetu ambayo Temeke tumeipeleka kwa Wizara ambayo itatuwezesha tutoke, tu-*graduate*, tuondokane na kutegemea

fedha za Serikali Kuu, halmashauri za Dar es Salaam zinakusanya kuanzia shilingi bilioni 70 kwenda juu. Hebu ibarikini mipango yetu ili tuweze kutoka kwenye tatizo la barabara na hatimaye tuweze kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sitaki kulalamikia barabara za jimbo langu. Ninatoa mipango kwa Serikali, wakiibariki mipango yetu nitakuwa sina sababu ya kulalamika kwa sababu tunaenda kutekeleza miradi ya barabara kwa mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Haji Amour Haji, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Yahya Nawanda na Mheshimiwa Yannick Ikayo Ndoinyo ajiandae.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kabla ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia uhai ambao yeye aliweza kutufanya kuwepo katika Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya katika nchi yetu, katika maono yake na kutufanya sisi kuweza kuonekana katika himaya ya Kimataifa kama Tanzania, nchi iliyo juu sana katika hali ya maendeleo inayopiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninampongeza kwa namna yake, Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kazi kubwa anayoifanya kwa upande wa Zanzibar, kwa vile ndiko ninapoishi. Ninampongeza kwa sababu naye ni mmoja wa wasaidizi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kufanya kazi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nimpongeze sana, tena sana ndugu yangu na rafiki yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ambaye ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ya kuelekeza na kutekeleza zile ahadi za Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kusimamia vyema kazi zake na kuwasimamia Mawaziri kwa kutekeleza yale yote yaliyoagizwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninawapongeza Mawaziri ambao anafanya nao kazi katika Wizara hii ya Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Kipekee ninampongeza Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Watendaji wake kwa ubunifu, na kuweza kulibadilisha Bunge letu hili Tukufu ambalo kila mmoja kwa sasa hivi anaona kuna mabadiliko yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ukiingia Bungeni sasa hivi kuna mambo unayaona kwa macho tu. Bunge lililopita nilikuwa sijaona bendera zilizojipanga, lakini sasa hivi Bunge letu linang'ara kwa Bendera za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Bendera za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, humu ndani katika kumbi zetu zote mbili, kila mmoja anaona namna zilivyo. Kwa hiyo, naye nimpongeze pamoja na watendaji wake akiwemo pamoja na Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije upande wa hoja. Hoja yangu kubwa niielekeze upande wa kujikumbusha. Tujikumbushe katika lile Bunge la Kumi na Tatu ambalo lilikuja kuhutubiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa kama Mhimili wa Dola ambao ulikuja katika hili Bunge letu na kuja kuleta maelekezo, kutoa ahadi za kwanza na kutoa picha ya namna Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha miaka mitano itakavyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba tu kwamba niliangalie jarida hili, kulisoma kidogo wakati ule ambapo alikuja. Jarida letu hili ninadhani kila Mbunge analo na kila Mbunge amelisoma. Mimi ninadhani uniruhusu nisome mambo machache ambayo yameandikwa katika hili jarida letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kilichonivuta katika hili jarida letu, kwanza katika ukurasa wa tano kuelekea miaka 2030 tutafanya mageuzi ya Mashirika ya Umma ili kuboresha ufanisi, uwazi na tija. Tunataka kuongeza siyo tu gawio ambalo Serikali inapokea, lakini pia kufikia lengo la Mashirika na Taasisi za Umma kuchangia angalau 10% ya mapato yote yasiyo ya kodi. Hilo sisi tutasema kwamba ni agizo la Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nije katika yale mambo ambayo aliyatolea ahadi katika kipindi cha siku 100 za uongozi wake. Pale kuna vitu ambavyo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alisema, suala la kwanza linahusu utumishi na utawala bora ambalo ni suala la uundaji wa Serikali. Serikali imeshaundwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika muktadha huo huo, alikuja na hoja ambayo mimi nitasema kwamba ni ya lazima viongozi ambao atawachagua pamoja na sisi wasimamizi kuna vitu ambavyo ni lazima tuvifanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake tukizungumzia ni 'lazima' katika muktadha wa kisheria tunasema kwamba ni '*shall*.' Kwa mfano, alisema ni lazima viongozi wa Serikali kwa ngazi zote kuanzia Mawaziri hadi Maafisa Tarafa wawe karibu na wananchi ili kuweza kufahamu changamoto zao na kuwajibika kwao. Hilo ni suala ambalo ni lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumaini kwamba sasa hivi Waziri Mkuu kwa zile ziara ambazo anazifanya moja anakwenda kusisitiza hili agizo ambalo alilisema Mheshimiwa Rais na kuliweka katika hotuba yake, kwamba hili suala ni lazima tukizungumzia kwamba viongozi wa Serikali kuanzia ngazi za Mawaziri pamoja na Maafisa Tawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kinachotusikitisha ni kwamba katika ile ziara ya Waziri Mkuu kuna mambo ambayo wakati mwingine katika ile ziara yake katika ule utatuzi wa zile changamoto, maana yake kuna matatizo madogo sana ya kutatuliwa na Afisa Tarafa, lakini utakuta changamoto zile anapewa Waziri Mkuu aweze kuzitatua. Hii inaonekana wazi kwamba huko chini bado hakujawa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niishauri Serikali, maana yake kwa mujibu wa hili agizo na huu ulazimisho wa Mheshimiwa Rais ni lazima tuhakikishe kwamba kuna vitu ambavyo tunavitengeneza. Katika kuvitengeneza kwetu, iwe ni muundo maalumu. Ninaomba katika utengenezaji wetu huu tuandae kitu ambacho kinaitwa *sustainable management* ambapo kila kitu ambacho kimezungumzwa na Mheshimiwa Rais maana yake kiwe ni *sustainable* na lazima kiwe na usimamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wake maana yake tuwe na kitu tunachokiita *conducting careful monitoring*. Ipo Idara ambayo imeundwa chini ya Waziri Mkuu ambayo inafanya kazi ya *monitoring* katika vyombo vyetu na taasisi zetu. Tunachotakiwa ni kuziangalia hizo ziwe ni zina-*conduct careful monitoring* maana yake kuwe na ule ufuatiliaji wa kina ambako kila mmoja awe anafuatilia majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kisha katika hotuba hiyo hiyo ya Bunge la Kumi na Tatu maana yake kuna kitu ambacho ni cha lazima, ambacho wanasema, ni lazima tudhibiti wachache wanaotaka kuturudisha nyuma kwa kuendekeza maslahi binafsi. Hilo ni suala ambalo ni kitu cha ulazimisho. Kama katika muktadha wa kisheria nayo ni '*shall*.'

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninadhani katika utendaji wa hizi kazi zetu, ningeshauri kwamba Serikali pamoja na sisi Wabunge tuwe karibu sana kuziangalia zile hotuba na zile hoja zinazotolewa na Mheshimiwa Rais ili kuweza kuzifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna anavyofanya kazi zake pamoja na watendaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ninaunga mkono hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa asilimia mia moja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haji Amour Haji, ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Yahya Nawanda, Mheshimiwa Yannick Ndoinyo ajiandae.

**MHE. DKT. YAHYA E. NAWANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Katika jambo kubwa Mheshimiwa Rais amelifanya ni kumchagua Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kuwa Waziri Mkuu, na pia kuwa Msimamizi Mkuu wa TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI ndiyo roho ya nchi yetu. Tukizungumza kuhusu TAMISEMI karibia 20% ya bajeti yetu inakwenda TAMISEMI. Kwa hiyo, tukiwa na kiongozi shupavu kama Mheshimiwa Dkt. Lameck Nchemba tunaenda kufanya mapinduzi makubwa katika TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeshawahi kufanya kazi na Mheshimiwa Mwigulu. Yeye ni mtu ambaye anapenda matokeo, na pia ni mtu muungwa na hapendi ubadhirifu, na vile vile ni mtu ambaye anapenda wananchi wake. Kwa hiyo, ninaweza kusema Wizara ya TAMISEMI imempata mtu shupavu na kwa hakika ninaona TAMISEMI inaenda kubadilika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba nijikite katika hoja tatu, au nne. Kwanza ni barabara. Wabunge wote wamezungumza kuhusu ubovu wa barabara zetu. Katika Wilaya ya Newala sisi tuna jumla ya *network* ya barabara kilometa 966, na hizi zote zinahudumiwa chini ya *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hizi barabara zetu tunategemea kupata fedha nyingi kutoka *Road Board* au *Road Fund*. Katika fedha za *Road Fund* Wabunge wote wamezungumza, kila Mbunge hapa anazungumza kuhusu kuongeza fedha, lakini pia barabara zetu nyingi zimeharibika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika Jimbo langu la Newala Vijijini, Barabara kutoka *Mkoma Moja* hadi Mnyame haipitiki kabisa. Pia, Barabara kutoka Chiwonga – Pacha Nne mpaka Nambali – Mkongi haipitiki. Pia, ukiangalia Barabara ya

Maputi – Chilangala mpaka Ndanda pia haipitiki. Pia, hata barabara kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu mimi ni Mbunge mkazi wa Iramba, barabara ya kutoka Mtoa – Mtekente – Ndago nayo ina changamoto pia kwa sababu ya mvua kubwa ambayo imetokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeiomba Wizara na Mheshimiwa Waziri Mkuu, akija basi tuletee majawabu ya barabara zetu namna gani tunaenda kuziimarisha ili ziweze kupitika mwaka mzima na kurudisha taswira ya barabara hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninaomba nijikite katika kilimo. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya hasa katika kukuza zao la korosho. Wakati anaingia, korosho tulikuwa tunapata tani 100,000 sasa hivi tunakwenda mpaka tani 600,000. Haya ni mapinduzi makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jimbo langu kwa mwaka huu 2026/2027 pembejeo ambazo Mheshimiwa Dkt. Samia anakuja kutuletea ni zaidi ya shilingi bilioni 27 ambazo zinaenda kuhudumia hekta zaidi ya 200,000. Kwenye zao la korosho ningeweza kushauri yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ije na mpango mzuri wa kuhakikisha tunaongeza ruzuku ya pembejeo ili kila mwananchi ambaye anaweza kulima aweze kuongeza tija. Pia, Serikali imekuwa inatoa pembejeo ya *sulphur,* na dawa za maji. Ningependa kuishauri Serikali, sasa iongeze viuatilifu au dawa za kuuia magugu *(weeder)*. Hii itasaidia sana kuongeza uzalishaji na hata yale mashamba ya zamani tunaweza kuyaongezea tija na kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali inaweza kuongeza fedha za kigeni, lakini pia kwa wananchi wataongeza uzalishaji, na fedha za *export levy* zitaongezeka kwa sababu mashamba mengi ya wananchi yatakuwa yamelimwa kwa wakati, pia tutaongeza uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ningependa kujikita katika suala la maji. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais, wilaya yetu na katika mradi kwa bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu *page number* 69 amezungumza, katika miradi ambayo inaenda kunufaika na fedha nyingi ni Mradi wa Makonde, ambao unatoka katika Jimbo la Newala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameleta jumla ya fedha za mradi ule shilingi bilioni 84. Ningependa kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, ule Mradi mpaka sasa hivi Mkandarasi amepewa fedha shilingi bilioni 18 pekee yake na asilimia imefika 46%. Ule Mradi ulikuwa unatakiwa ukamilike tarehe 30 Machi, lakini mpaka leo mradi ule bado unasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, ule Mradi wa Maji wa Makonde unaenda kuhudumia Wilaya ya Newala, Wilaya ya Tandahimba, na Wilaya ya Mtwara, majimbo zaidi ya saba. Asilimia zaidi ya 45 ya wananchi wa Mkoa wa Mtwara wanaenda kunufaika na ule mradi wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa mradi ule unaenda kusaidia sana wananchi wa wilaya hizi nilizozitaja hasa Majimbo ya Newala Mjini, Newala Vijijini, Tandahimba, Lulindi, Nanyamba, na Mtwara Vijijini. Hawa wote wanategemea huo mradi mzuri wa Makonde. Kwa hiyo, ningependa kuishauri Serikali tumalize huu mradi kwa wakati ili wananchi waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nichukue nafasi hii kumshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Aweso. Huu mradi ulikuwa ni jitihada zake, alienda kumwomba Mheshimiwa Rais na akatukabidhi huo mradi. Kwa hakika Mwenyezi Mungu ambariki sana na sisi tunamwombea heri na mwisho wa siku huu mradi ukikamilika, mambo yanaenda kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye vituo vya afya, Serikali imefanya kazi kubwa ya kujenga vituo vya afya vingi sana, lakini katika Jimbo la Newala Vijijini tuna vituo vitatu vimekamilika. Pia, tunaiomba Serikali, kukamilika tu kwa jengo, tungependa kuweka vifaa pia katika vituo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vituo vya Mkwedu, Nandwahi, na Kituo cha Malatu, hivi vituo vimekamilika. Kwa hiyo, tungependa sana hivi vituo pia vipate *ambulance,* na pia vifaa ambavyo vingeweza kusaidia kufanya kazi kwa ufanisi. Pia, Vituo vya Mtunguru, Mdimba Mpelepele, pamoja na Mikumbi, hivi vipo katika *pipeline;* na katika bajeti ningeomba Serikali pia iweze kusaidia na kukamilisha vituo hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ningeweza kuleta mawazo kidogo katika migogoro ya wananchi. Serikali inafanya vizuri sana katika kuhakikisha migogoro hii inakwisha. Tunaisadia Serikali yetu kuhakikisha tunajikita zaidi katika kupunguza kero za wananchi. Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, na Wakuu wa Wilaya wanafanya kazi nzuri sana, lakini pia mimi ningeweza kushauri kuwe na *institutional framework,* ili kama mgogoro katika ngazi ya wilaya unahusu afya au ardhi, basi Afisa Ardhi, Mwanasheria wa Halmashauri, au Kilimo na hao watu watatue huo mgogoro. Kuwe na *institution framework*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka nilivyokuwa *DC* Iramba nilikwenda Shelui kutatua mgogoro ambao tayari Mzee Chiligati miaka 35 nyuma alishautatua. Kwa hiyo, bila *institution framework* tutakuwa hatufanyi ile kazi ya kuwasaidia wananchi ambayo kwa hakika tumeona kazi kubwa ambayo Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu anaifanya, na mwisho tutaendelea kuwalaumu tu Wakuu wa Mikoa na tutaendelea kuwalaumu Wakuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwajengea nguvu kubwa tutengeneze *institution framework* ambayo itawasaidia wao pia katika kuhakikisha hizi kazi zinafanyika, na migogoro inaratibiwa na hata akija kiongozi mwingine mgeni, basi anajua kama katika kijiji fulani mgogoro umetatuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Yahya Nawanda, ahsante. Nilimtaja Mheshimiwa Yannick Ndoinyo, ajiandae Mheshimiwa George Natany Malima.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kukumbusha tena, kabla hujasimama tafadhali utazame nyuma kama kuna mzungumzaji, kanuni zetu zinataka utulie na usikatishe mbele yake.

**MHE. YANNICK I. NDOINYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami nichangie hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu inayoendelea. Nianze kwa kweli kwa kuipongeza sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuiletea maendeleo nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia, Makamu wetu wa Rais, Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, pamoja na Waziri Mkuu ambaye hotuba yake leo tunaijadili. Kwa kweli, mimi naanza kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu, ameiletea nchi yetu, siyo maendeleo peke yake, bali utulivu na amani ambapo kwa kweli, tunaihitaji na tunaitumia na kwa viwango vyovyote Tanzania ni nchi bora. Binafsi najivunia sana kuwa Mtanzania na kwa kanda hii yote ya Afrika Tanzania ni nchi ambayo inatamaniwa sana na wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza, na kwa bahati nzuri, juzi tumepata nafasi ya kuhabarishwa kuhusu kazi za *CAG*. Mimi nagusia kidogo kabla sijaingia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, hiyo ndiyo dalili, ripoti zake zinaonesha uimara wa taasisi zetu za Tanzania na uhuru wa taasisi zinazofanya kazi na ndiyo maana haiingiliwi na anatoa ripoti yake kulingana na maoni yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, mimi ninataka kuitumia hiyo na Watanzania wafahamu kwamba, taasisi zetu ziko huru kama hiyo na zinafanya kazi kwa uhuru. Tukipata nafasi ya kuchangia tutachangia, lakini hiyo ndiyo sura halisi ya taasisi zetu, ziko huru kwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza pia ofisi ya Waziri Mkuu na hotuba yake pamoja na taasisi zote ambazo ziko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kama TAMISEMI ikiongozwa na Mheshimiwa Prof. Riziki Shemdoe na wasaidizi wake wengine wote, tunawashukuru. Hongereni sana kwa hotuba na *plan* hiyo

ambayo mnayo kwa kweli, ni nzuri. Imeonesha maono, kazi zilizofanyika na maono ya mbeleni kwa mwaka huu tunaouendea na mimi nataka ni-*narrow down* kwa Wilaya yangu ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ngorongoro ni kubwa kushinda mikoa mingi Tanzania, ina kilomita 14,030. Ni wilaya kubwa sana na kwa mgawanyo, inawalazimu watu kutoka tarafa moja kwenda hadi karibu kilomita 300 kufuata huduma makao makuu ya wilaya, ni eneo kubwa sana. Inatakiwa itafakariwe sasa namna ya kugawanya ile wilaya, zipatikane halmashauri angalau mbili, ili watu waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasemea hii kwa sababu, ile wilaya iko pembezoni sana na wilaya nyingine. Ni wilaya peke ambayo haiunganishwi na barabara ya lami na Mkoa wa Arusha. Kwa hiyo, ukichukua hiyo na umbali wa kufikia huduma, kwa kweli, inastahili tuwe na halmashauri pamoja na maeneo mengine mapya ya utawala, ili kurahisisha huduma yetu kwa wananchi. Wananchi wanapotaka kwenda kutafuta vitambulisho vya *NIDA*, vyeti vya kuzaliwa na vyeti vingine wanalazimika kusafiri umbali mkubwa sana kwenda wilayani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri wewe unaifahamu ile Wilaya, ni ya utalii, lakini kiuchumi pamoja na kwamba, tumegawanyika kiutawala na kiuchumi, ile wilaya imeganyika sehemu kuu mbili; Kusini, ambayo ni ufugaji na utalii na Kaskazini, ambayo ni kilimo, ufugaji na utalii. Mgawanyo huu wa kiuchumi hautumiki ipasavyo kuinufaisha nchi na watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utalii bado ni mdogo sana. Pamoja na kwamba tuna taarifa kwamba makusanyo yake ni makubwa sana kuanzia shilingi bilioni 260 na kuendelea, lakini ukilinganisha na *potential* ya utalii, bado ni kidogo sana. Mapato yale yanayotokana na utalii. Kwa hiyo, ni rai yangu kwa Serikali kuhakikisha kwamba, inaboresha utalii ulioko ndani ya Wilaya ya Ngorongoro, ili iweze kunufaisha nchi na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, pamoja na kwamba, tunachangia na kuipongeza Hotuba ya Waziri Mkuu na

taasisi zake, ni muhimu pia mkazo utolewe zaidi kwa zile sekta ambazo ni za uzalishaji, kilimo na ufugaji kwa maeneo ambayo bado hayajawekewa mkazo wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Wilaya hii ya kwangu ya Ngorongoro ufugaji ni uchumi, lakini pia, ni mila; na kwa sababu, ni mila na Uchumi, ni vizuri kuweka mkazo wa kutosha kuhakikisha kwamba, sekta ya ufugaji inainuliwa, ili kuweza kunufaisha watu. Kwanza yapatikane malisho ya kutosha kwa wafugaji kwa nyakati zote, masika na kiangazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, Serikali inatakiwa iweke mkakati wa kuhakikisha kwamba, hakuna mifugo ya wafugaji inayokufa kwa kukosa malisho. Mifugo mingi sana inakufa kwa sababu hakuna malisho wakati wa kiangazi, na ni kweli majani huwa yanaisha, lakini uwezekanao wa kuwa na malisho mbadala hatujaufikiria vya kutosha, ili kuhakikisha kwamba, wafugaji hawapotezi uchumi wao wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, sisi ni wafugaji naisihi Serikali, na hasa zile sekta zinazohusika, Wizara hii tunayoijadili sasa na ile mifugo ihakikishe kwamba inaweka mikakati ya kupata lishe na vyakula mbadala, kwa ajili ya mifugo, ili wasife wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwangu Wilaya ya Ngorongoro tuna wakulima karibu 13,000 wanaojishughulisha na kilimo. Naipongeza sana Serikali, imefanikiwa kusambaza mbegu za ruzuku na mbolea kwa wakati za kutosheleza, tunaishukuru sana Serikali kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto yetu ni masoko. Wakulima wanapopata mazao mengi sana hupotea shambani na mengine hupotea barabarani wakiyapeleka sokoni. Ni muhimu sana Serikali iweke miundombinu ya uhifadhi wa mazao baada ya kuvuna, ili wakulima wasipoteze mazao na uchumi wao ambao wanautarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, ile wilaya yangu inatakiwa ifunguliwe. Kama Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia

Suluhu Hassan, anavyofungua nchi, ile wilaya yangu inatakiwa ifunguliwe zaidi. Tunazo kilomita 49 za lami ambayo inatokea pale Wilayani Loliondo na kuishia katikati ya njia, kweli inasaidia kupunguza mwendo, lakini haisaidii kutimiza mahitaji tunayohitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda muafaka sasa wa kutuwekea barabara ya lami kutoka Mto wa Mbu kwenda Loliondo, ili zile saa 11.00 tunazosafiri zipungue ziwe saa tatu au mbili. Tunaiomba Serikali iweke huo mkazo na msisitizo wa kutujengea hiyo barabara ya lami, ili iweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwa suala la mifugo. Tunayo changamoto kidogo, mara nyingi sana mifugo inapoingia maeneo yaliyohifadhiwa, kuna wakati mifugo ile inataifishwa kwa kusingizia kwamba haina wenyewe. Ninaiomba Serikali, hasa hizi sekta zinazohusika, tuache kutaifisha mifugo ya wananchi eti kwa sababu, haijatambuliwa. Mifugo mingi ina wenyewe…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha. Malizia hiyo sentensi ya mwisho.

**MHE. YANNICK I. NDOINYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mifugo inayotambuliwa, ina wenyewe isitaifishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Yannick kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa George Malima, ajiandae Mheshimiwa *Engineer* Amosy Maganga.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza naanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, ambaye ametupa afya na nafasi ya sisi sote kufika katika jengo hili kuendelea na shughuli zetu kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninamshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya katika nchi yetu, hasa katika hizi siku 100. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais. Tatu, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Rais alipomteua hakukosea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ni mchapa kazi, ni mtu ambaye anataka kuona matokeo. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba tumemwona wakati akiwa Waziri wa Fedha, amefanya kazi yake vizuri na hata Mheshimiwa Rais akamwona, akampa cheo au nafasi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nakumbuka Januari tarehe 2, mapema tu baada ya kuteuliwa alifanya ziara katika Jimbo langu la Mpwapwa kuangalia athari za mafuriko ambayo yalitokana na kunyesha kwa mvua nyingi, ambayo iliharibu miundombinu ya reli. Kwa hiyo, ninampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ni nzuri. Uzuri wa bajeti hii umefanya wananchi wengi wawe na matumaini makubwa kwamba, mwaka huu shughuli nyingi zinakwenda vizuri sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu kazi iliyobaki ni utekelezaji wa bajeti hii, ikitekelezwa kwa ukamilifu wake, basi wananchi wetu watanufaika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika siku 100 ameanza kutekeleza ahadi zake nyingi ambazo alizitoa wakati anapita kwenye Kampeni ya Uchaguzi Mkuu wa 2025. Moja ya ahadi ambazo ameshatekeleza sasa, ni uanzishwaji wa Mpango wa Bima ya Afya Wote, mpaka sasa zaidi ya watu 1,400 tayari wameshaingizwa kwenye mpango huu, wale watu ambao wana kipato cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu ni mzuri sana, utasaidia wananchi wengi na hasa wale ambao hawana uwezo

wa kuhudumia matibabu yao. Jambo kubwa ambalo ningependa kushauri ni utekelezaji wa dhana yenyewe. Tuanze na watu wasio na uwezo, isitokee kwamba watu wenye uwezo ndiyo wanaanza kunufaika kabla ya watu wasio na uwezo. Kwa hiyo, Serikali isimamie vizuri, ili watu wasio na uwezo waanze kunufaika na mpango huu wa Bima ya Afya, halafu badaye watafuata watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mambo haya yakitokea huko nyuma, mfano mpango mzuri sana wa *TASAF* ambao Serikali iliuanzisha, lakini matokeo yake ni hata leo ukienda kwenye maeneo yetu kule kwenye majimbo, utakuta wanaonufaika na *TASAF* sio wale wenye sifa ya kuingia kwenye huu mpango. Wale ambao wana unafuu wa maisha ndio wameingia, wale ambao ni maskini kabisa wa mwisho wamekosa nafasi. Hii inatokana na nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeleta mpango mzuri, Mheshimiwa Rais alitarajia matarajio mazuri, lakini utekelezaji usiposimamiwa vizuri, basi tunakutana na tatizo hilo. Kwa hiyo, naomba mpango huu wa Bima ya Afya kwa Wote, uanze na kaya ambazo hazina uwezo kabisa wa kuhudumia matibabu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninampongeza Mheshimiwa Rais ni, ndani ya siku 100 ameanzisha mpango wa shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kundi la vijana. Kwa hiyo, ninaamini ukitekelezwa vizuri, ukiratibiwa vizuri, mpango huu unaenda kuwakomboa vijana, utaongeza ajira katika sekta mbalimbali, utaongeza ajira kwenye kilimo, kwenye biashara, kwenye viwanda vidogo vidogo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kinachotakiwa ni uratibu na hasa kule eneo ambalo fedha hizi zinatolewa, tukisimamia vizuri, tutaondoa upendeleo, ubadhirifu, kutengeneza vikundi hewa au waombaji hewa. Hayo ni mambo ambayo yanaweza kuathiri mpango huu mzuri ambao Mheshimiwa Rais ameukusudia. Kwa hiyo, lazima Serikali isimamie hasa kwenye halmashauri ambako mikopo hii inaenda kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naongelea kuhusu barabara. Sasa kuna miradi mingi ya barabara, hasa zile ambazo zimetekelezwa, kuwekwa tabaka la lami, zimesimama kwa muda mrefu. Nikirudi Jimboni kwangu Mpwapwa, Mpwapwa ni Wilaya kongwe katika Mkoa wa Dodoma, ni kati ya Wilaya saba za Mkoa wa Dodoma; wilaya zote sita zimeunganishwa kwa barabara za lami isipokuwa Barabara ya Mpwapwa – Dodoma. Tuna kipande cha barabara chenye urefu wa kilomita 32 tu kutoka Kongwa *Junction* kwenda Mpwapwa Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi yuko *site,* zaidi ya miaka miwili sasa hajaanza kazi kwa sababu, hajalipwa fedha ya awali. Naiomba sana Serikali iangalie, haiwezekani jiji kama la Dodoma, Makao Makuu ya Serikali, kuna barabara moja katika wilaya moja katika mkoa huu wa Dodoma haijawekwa lami. Wabunge waliotangulia wamepiga kelele sana kuhusu jambo hilo, lakini bado ni kizungumkuti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna wasiwasi, Wananchi wa Mpwapwa wana wasiwasi, kwamba inawezekana sasa mkandarasi akachoka akaondoka maana amekaa zaidi ya miaka miwili pale hakuna kitu kinaendelea. Wananchi wana hamu sana ya kutumia ile barabara kwa ajili ya kukuza uchumi wao. Kwa hiyo, naomba sana, Serikali iliangalie jambo hili kwa jicho la karibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongee kidogo kwenye upande wa kilimo. Kilimo ndiyo sekta ambayo inatoa ajira nyingi kuliko karibu sekta zote. Watu wengi wamejiajiri kwenye kilimo. Naipongeza Serikali kwamba, kwa sababu ya ruzuku ya mbolea tumeweza kuwa na uhakika wa usalama wa chakula kama nchi kwa 130%. Pia, matumizi ya mbolea yameongezeka kwa zaidi ya 14%, ni kwa sababu, sasa watu wameona umuhimu wa mbolea, lakini pia, ile ruzuku imefanya watu wengi waweze kupata mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali iendelee kuratibu vizuri, kama ilivyokuwa inafanya, ili tuweze kujikwamua. Ule mpango wa mabwawa ya umwagiliaji ambao ulianzishwa katika kipindi cha nyuma, ulikuwa mzuri sana, lakini

sasa mabwawa mengi utekelezaji wake hauendi kwa kasi iliyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, kule kwenye Jimbo langu la Mpwapwa, tunalo Bwawa la Msagani ambalo linatumia gharama kubwa sana ya shilingi 27.8, lakini mpaka leo ujenzi wake haujafikia hata 60% kwa sababu, unasuasua na ni zaidi ya miaka miwili sasa bwawa hilo limejengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabwawa haya ni muhimu sana, yangeweza kusaidia wananchi wakajikwamua na umaskini kwa kulima kilimo cha umwagiliaji. *Idea* ilikuwa nzuri sana kwamba, tukiwa na mabwawa maeneo mengi katika nchi yetu, wananchi watalima kilimo cha umwagiliaji, wataachana na kilimo cha kutegemea mvua; kuna mwaka inanyesha, lakini kuna mwaka mwingine hainyeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukiwa na mabwawa haya, maana yake ni wananchi wataendelea kulima, mvua ipo au haipo watafanya kilimo wakati wa kiangazi, lakini pia hata wakati wa masika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iangalie kupitia Wizara ya Kilimo mabwawa haya yajengwe haraka sana. Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Nakushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa George Malima kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa *Engineer* Amosy Maganga, ajiandae Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere na Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe.

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nakushukuru sana kwa kuniona na kuniita niweze kutoa mchango wangu katika hii Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya hatimaye leo

tumeweza kukusanyika mahali hapa. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwanza niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi ambavyo kwa kweli, ameendelea kutupigania na kututumikia Watanzania. Tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa ni mbeba maono ya Watanzania. Leo hii tunaona anatuchukua Watanzania kutoka kwenye uchumi wa chini anatupeleka kwenda kwenye uchumi wa kati wa daraja la juu. Tunamshukuru sana kwa jitihada hizi anazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, jambo hili siyo jepesi, ni jambo kubwa linalohitaji ujasiri na umakini wa hali ya juu, ambao Mheshimiwa Rais wetu amejaliwa na Mwenyezi Mungu. Katika hilo, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawatia shime Watanzania, Waheshimiwa Wabunge pamoja na wafanyakazi wote, sasa tusimame na Mheshimiwa Rais kuona kwamba, maono aliyonayo yanatekelezeka na yanafika kwenye nchi ambayo tunaikusudia, ambayo ndiyo nchi ya asali na maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba wafanyakazi tusimame vizuri, tufanye kazi zetu vizuri, lakini wakulima, wafanyabiashara pamoja na wanafunzi tunapokuwa vyuoni pamoja na kule shuleni, tuwe na kaulimbiu yetu kwamba sasa tunaenda mwezini na mwezini kwetu ni kwenda kwenye uchumi wa kati wa daraja la juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila tutakalokuwa tunalifanya Watanzania tuseme kwamba Watanzania tuna jambo letu, Watanzania tunaenda mwezini na mwezini ndiyo huko kwenye uchumi wa kati wa daraja la juu. Kwa kweli hilo na mimi nasema

kabisa kwa dhati ya moyo wangu, Wabunge wenzangu tusimame na Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri Mkuu, kwa kweli kwa kipindi kifupi toka ameapishwa mpaka hivi sasa hakika Waziri Mkuu amejitambulisha pasipokuwa na mashaka yoyote kwamba hakika yeye ni mtetezi wa wanyonge na wala hiyo haina mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu tunamsubiri kule Tabora tunaamini kwamba atafika na tutakuwa na furaha kubwa kweli kweli. Nami ninaamini kwamba mwenye macho na mwenye masikio, basi ameshaona, na ninaamini wafanyakazi wote walio chini yake, ninaamini njia wameshaiona na ninaamini kwamba sasa watafuata nyayo zake na tunaamini mabadiliko makubwa kabisa kabisa yanaenda kutokea katika Taifa letu la Tanzania. Mungu ambariki sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, aendelee kuchapa kazi, nasi tunamuunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mazuri mengi kweli yamefanywa na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunawapongeza sana. Ilikuwa ukiongelea umeme, ni vijijini, lakini leo hii ni vitongoji. Ukiongelea maji, miradi mbalimbali inaendelea katika vijiji vyetu. Ukiongelea ujenzi wa shule, ujenzi wa zahanati na mambo kadha wa kadha, yanaendelea katika Taifa letu la Tanzania. Kimsingi tunaendelea kuipongeza Serikali yetu na tunaamini kweli uchumi wa kati unawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mazuri sana ambayo Serikali yetu imekuwa inatufanyia, bado kuna changamoto ambazo zinaendelea kuwakabili Watanzania. Moja ya changamoto hizi ni ufinyu wa maeneo ya shughuli za kiuchumi katika maeneo mbalimbali ya Taifa letu hili la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikichukulia mfano katika Mkoa wetu wa Tabora na hususan katika Jimbo letu la Sikonge changamoto hii ni kubwa na imepelekea kuwa na mwingiliano mkubwa sana kati ya wakulima, wafugaji na warinaji wa asali vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, Jimbo letu la Sikonge na Wilaya yetu ya Sikonge ina jumla ya ukubwa wa kilomita za mraba 27,870, lakini kati ya kilomita hizo, ni kilomita 1,533.01 tu ndizo zinazotumika katika shughuli za kimaendeleo, katika shughuli za ufugaji, katika shughuli za kilimo pamoja na urinaji wa asali. Eneo hili ni dogo sana. Eneo lote lililobaki takribani kilomita za mraba 26,300.99 zote hizi zimebaki kama ni mapori ya akiba na mengine ni kwa ajili ya Hifadhi ya Taifa vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna mashaka wala hatuna shida na Hifadhi ya Taifa, shida yetu ipo katika mapori haya ya akiba. Tunaomba sana Waziri Mkuu hebu hawa wananchi wa Sikonge kutoka kwenye asilimia tano nukta tano wanazozitumia kwa shughuli za kilimo, hebu ziongezeke hizi angalau tufikie hata 20%, tunaomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii yale ambayo ni mapori ya akiba, kimsingi haya mapori tayari kuna wageni, kuna watu kutoka nje ya Mkoa wa Tabora wameshavamia kwa sababu wanajua haya ni mapori yamekaa tu hayafanyi kazi yoyote, yameshavamiwa kwa kiasi kikubwa sana. Hivyo tunaomba tunaomba Serikali tunaiomba hebu ituongezee haya maeneo na yale yatakayobaki kama ni akiba na hifadhi, basi kuwe na *management* nzuri ya kuona kwamba kama ni akiba basi iendelee kuwa ni akiba na kama ni hifadhi, basi iendelee kuwa na hifadhi na yasivamiwe, tunaomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano uliopita wa Bunge hili niliuliza swali la nyongeza kuhusu maeneo haya, jibu ambalo Serikali ilitoa, ilisema kwamba kuna Kamati ya Mawaziri Nane ambayo iliundwa na tathmini yao inasubiriwa ili kusudi hatua stahiki ziweze kuchukuliwa ili wananchi hawa waweze kuongezewa maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiri sasa hivi ni mwaka wa tatu na nimwombe sasa kwa vile Mawaziri hawa wanane wako chini ya Waziri Mkuu, basi hebu aitishe basi hiyo taarifa ili kusudi tathmini iweze kuonekana na ikiwezekana basi, ninaamini itawezekana kwa sababu hata Rais katika taarifa yake ya kuzindua Bunge hili alisema anaenda kuongeza takribani ekari 2,500,000, mimi

ninaamini katika nyanja zote hizo Wanasikonge wanaenda kupata maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ukienda katika kijiografia ya Mkoa wetu wa Tabora na hususan katika Wilaya yetu ya Sikonge hatuna maziwa wala mito ya kudumu. Kimsingi ni kwamba hatuna Bahari, hatuna maji, lakini tumejaliwa kuwa na mito midogo midogo ya msimu, ambapo wakati wa mvua kubwa kama mwaka huu inajaza mabwawa ya kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mto wetu Uruwa, tunalo bwawa letu la Urua na lilikuwa limeshaingizwa tayari kwenye skimu ya umwagiliaji, lakini baadaye sintofahamu ikatokea kwamba oh, iko karibu na hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani kilomita zote zile tulizozisema za mraba 26,300.99 zote hizo kukata tu kaeneo kadogo na sisi tukapata skimu ya umwagiliaji haiwezekani! Hapana. Tunamwomba sana Waziri Mkuu ili na sisi tuweze kupatiwa lile eneo tupunguze kidogo tu kule kwenye hifadhi ili na sisi tuwe na umwagiliaji tuweze kulima mpunga, tunaomba sana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha, kengele ya pili imeshalia.

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, lakini nimalizie tu mara moja. Bado kuna eneo la ajira vilevile kwa kweli vijana wetu walioko kule vijijini wanalia na wamekata tamaa, anafika kijana anakwambia, Mheshimiwa mimi siajiriki, unamwambia kwa nini huajiriki? Anasema sina *connection*. Huu msamiati wa *connection!*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa tunashukuru kwa mchango wako.

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Maganga, ahsante. Nilimtaja Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, ajiandae Mheshimiwa Exaud Kigahe.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hii hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza namshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kazi ya Urais siyo kazi ndogo ni kazi kubwa sana. Kwanza kabisa Rais analinda amani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, duniani kote Rais yeyote anayekuwepo madarakani kazi yake kubwa ni kulinda amani ya nchi yake. Rais amelifanya hivyo, anaendelea kulifanya, tunamwombea aendelee kulinda amani ya nchi yetu, nasi tuendelee kupata maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Waziri Mkuu, ana kazi kubwa sana, kila kipindi cha uchaguzi kunakuwa na hofu, mtu anapokuwa anafanya kazi wanasema huyu anaomba Urais. Sasa anayo kazi kubwa sana, sijui ni wapi ambapo watasema hataomba Urais, kwa sababu yeye ni Waziri Mkuu, anakaa na Baraza la Mawaziri, ana vikao, anakaa na *Party Caucus* vikao, ukienda mikoani yeye ni Kiongozi wa Chama, atakutana na wanachama. Sasa sijui ni wapi watasema? Kwa hiyo, anafanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishaambiwa siku moja hapa kwamba hotuba hii ni Waziri Mkuu. Kwa hiyo, Wabunge wanapokuwa wanaongea, awe anatusikiliza basi. Sasa tukiongea na Waziri Mkuu halafu hatumwoni, nayo inakuwa kazi ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kumwomba Waziri Mkuu afanye kazi bila kuangalia kwamba anasema wapi? Atende yale ambayo Katiba inasema, atende yale ambayo kiongozi wake mkuu wa juu anamwelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Mawaziri wote waandamizi wa Wizara hizi, Mheshimiwa Prof. Shemdoe, Mheshimiwa Sangu na Mheshimiwa Profesa Kabudi. Mheshimiwa

Prof. Mdoe ni mtu na nusu, yaani huyu ni mtu na nusu, sijawahi kuona Profesa ambaye hata leo ukisema bwana mimi nakuteua kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri, anarudi tena kwa sababu aliwahi kuwa Mkurugenzi huko. Anafanya kazi vizuri na watendaji wake wote, Manaibu wazuri, Makatibu wazuri na Watendaji wote wa Wizara, tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti nianze na maombi ya Jimbo la Bunda. Naomba sana Profesa na wote wanaohusika Shule ya Msingi Nyamswa A, Ikizu B, Tingirima, Mariwanda, Ikomarilo A na B hizi shule zimetitia kutokana na maji na hali ya wanafunzi wanakaa chini, wengine hali ni mbaya madarasa mengine zaidi ya matano manne tumeyabomoa. Tunaomba mfanye kazi nzuri ya kwenda kutusaidia kwenye hizo shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo shule mbili za sekondari. Shule ya Sekondari ya Tingirima, ni shule mpya, haina maabara, walijenga majengo yakabaki wazi maabara zote tatu. Tunaomba waende wakajenge yale maabara, wamalizie. Pia Shule ya Sanzati ni mpya, lakini haina jengo la utawala, ina hali mbaya sana. Walishasema wanaenda kuiona, waende wakaiangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Unyali pamejengwa majengo, lakini hakina *theater.* Jengo la upasuaji halipo, wakamalizie kituo kipya cha Mihingo, wametupatia shilingi milioni 250, watu wamemaliza fedha, naomba warudishiwe, ili wakipata hela waweze kumaliza kama ahadi ya Serikali ilivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumzia hali ya maliasili na utalii kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, kwenye Bunge lililopita, Bunge la Kumi na Mbili tulisema kwamba maliasili na utalii, watu wa *TANAPA*, taasisi ya *TANAPA, TAWA* na *TFS* tuwape fedha zao. Taasisi zile ni kubwa, zinalinda maliasili ya nchi yetu, tukakubaliana warudishe 50%. Sasa hivi wanawapa 51% na wanapata 49%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo fedha bado ziko Serikalini, wanaenda tena wanakusanya, wanawaletea ndiyo mnawarudishia. Tunaomba kwa kuanzia, waacheni wao

wakusanye halafu ninyi ndio mchukue. Mtavunja, mtaua hizi taasisi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema leo tuna watalii wameongezeka kutoka milioni moja mpaka milioni mbili, wanaongezeka, tuna bilioni tano zimeongezeka mpaka shilingi 5,000,900,000/=. Sasa kama hatuwezi kukusanya hizo fedha zilinde hiyo maliasili, tutaporomoka kwa vyovyote vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANAPA* na *TAWA* ndiyo wanalinda wanyamapori, na sisi kwenye vijiji vyangu zaidi ya 11 toka miaka 20 hawalimi mazao yao yote, yanaliwa. Naomba tafadhali sana Mheshimiwa Waziri Mkuu hili jambo mlichukue, tulizungumze, tuwekeeni fensi, kwa sababu Botswana, *South Africa*, Kenya wameweka fensi. Tupeni fensi ili wakulima wa maeneo ya Maliwanda, Kunyari, Kihumbu, Kyandege na Tingilima wapate kupata mazao yao ya kilimo wanacholima, tafadhali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie mifuko ya kijamii. Mifuko ya kijamii, tunayo *NSSF, PSSSF, WCF* na hata *OSHA*, tuipeni nguvu hii mifuko kwa sababu sasa hivi ina shilingi trilioni zaidi ya 24. Tuipeni nguvu hii mfuko ili iweze kuongeza ajira kwa wananchi. Kwa hiyo, tunaomba tuipe nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mafuta, bei ya mafuta nchini tusifanye mzaha, hapa Wabunge wameongea mambo mengi sana. Naomba cha kwanza, punguzeni zile tozo ambazo siyo za lazima, punguzeni zile tozo. Jambo la pili tuna ule mfumo wa *bulk* wa kuagiza mafuta kwa pamoja, turuhusu sasa watu binafsi nao waagize mafuta tuweke mara mbili kama walivyofanya wenzetu Wakenya. Ni lazima tufanye kila namna ili tuweze kuweka mafuta ya bei iwe nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama ni kupunguza mapato, tuna maeneo mengi ya Wizara mbalimbali ambayo yana bajeti ya vinywaji. Tupunguze huko kwenye bajeti ya vinywaji tupate nafuu ya wananchi kwenye mafuta, tutaumiza wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali, tafadhali, Waziri Mkuu afanye kila namna kwa sababu sasa hivi tunatumia *bulk,*

tumeshaagiza yale mafuta, yatakuja kwenye mwezi mzima kwa sababu hatuna mfumo wa watu, *private sector,* maana yake tutaenda mpaka mwezi mzima, itatuumiza. Ni lazima tufike wakati tufanye nafuu, tuagize mafuta kwa watu binafsi au tupunguze bei wenyewe ili mafuta yawe nafuu kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna misemo mingine ya Serikali inaumiza. Kuna maelekezo ya Serikali yanayotamkwa kila siku, lakini yanaumiza. Leo tunaambiwa Rais ameanzisha Wizara ya Vijana na ametoa shilingi bilioni 200 kwa vijana, lakini ukija kwenye lugha nyingine unakuta hii fedha shilingi bilioni 200 mara imeenda kilimo, mara sijui imeenda wapi? Imeenda sijui Wizara ya Ustawi wa Jamii! Tunaomba tafadhali, hii shilingi bilioni 200 ni ya vijana. Hii Wizara imeanzishwa na vijana waliipokea vizuri mno, kwa shilingi bilioni 200 ibaki kwenye mawazo ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunao msemo tunasema elimu bure kwa shule za msingi na sekondari, lakini leo ukienda kwenye sekondari mtoto anayeingia sekondari na anayeingia darasa la kwanza, michango 240 kidogo. Shilingi 200,000, shilingi 300,000, shilingi 400,000 mpaka shilingi 600,000, lakini sekondari hizo zinapokea ruzuku ya karo shilingi bilioni 20. Kwa mfano, kuna watoto 500 unazidisha mara 20,000 unapata hela zake, lakini kuna *grant* zinatolewa. Hela hizo zinaenda wapi? *Ream* kila siku, jembe, koleo, tuangalie hii mifumo ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za msingi tunapeleka shilingi bilioni zaidi ya 24 kwa mwaka, lakini ukienda pale mtoto anachanga kila kitu mpaka muhuri wa kupigia shati anatoa anapigiwa muhuri. Tunatoa wapi vitu? Tuangalie mifumo yetu hii kama inafanya kazi vizuri, kama haifanyi kazi vizuri tuangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za afya, leo ukienda zahanati, zahanati tunajua pale kuna Nesi, maeneo mengine hakuna Mganga, lakini kwenda pale kutibiwa lazima utoe shilingi 5,000. Hivi mwananchi wa kawaida ataitoa wapi?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anaitoa wapi shilingi 5,000 ya kuchanga? Ukienda Benjamin kutoka Jumatatu mpaka Ijumaa ni shilingi 25,000 lakini ukienda Jumamosi, Jumapili ni shilingi 70,000. Wananchi wataumia. Kwa hiyo, tuangalie mifumo yetu ili tuweze kujenga nchi yetu vizuri. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere ahsante sana kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Exaud Kigahe.

**MHE. EXAUD S. KIGAHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema aliyetujalia uzima kukutana hapa leo tukiwa na afya njema. Pili, ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya, lakini zaidi, pamoja na Makamu wa Rais, Balozi Dkt Emmanuel Nchimbi, zaidi Waziri Mkuu wetu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ambaye leo na mimi napata nafasi kuchangia katika hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweka historia katika nchi hii kwa kuweka miradi mingi ya kimkakati, tukianza na *SGR* ambayo kwa kweli sote ni mashahidi, inasaidia kukuza uchumi na hasa katika sekta ya usafirishaji hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, pia katika sekta ya usafirishaji viwanja vya ndege lakini na ndege zenyewe pamoja na sekta ya usafirishaji katika bahari kwa maana ya maji, bandari lakini zaidi kwenye barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweka historia kwa kuhakikisha miradi mingi ya kimkakati inaendeshwa vema bila kusahau sekta ya nishati, mradi mkubwa ule wa Mwalimu Nyerere ambao sasa umekuwa mkombozi kwetu sote katika masuala ya umeme, nadhani sasa

sote tunaona umuhimu na umahiri wake Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia hii iliyojengwa katika nchi hii pia Jimboni kwangu imefanyika. Nichukue nafasi hii pia sasa kuwashukuru sana wananchi wenzangu wa Jimbo la Mufindi Kaskazini ambao walinichagua kwa heshima kubwa kuwa kiongozi wao. Kule tumeweka historia kwa mara ya kwanza katika Jimbo la Mufindi Kaskazini kuanza kuwa na barabara za lami tangu kuumbwa kwa ulimwengu. Sasa haya yote ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo katika barabara tu, pia katika sekta ya maji, elimu, afya. Zaidi ya vituo vitano vya afya vipya vimejengwa ndani ya miaka minne ya uongozi wake Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hili ni jambo kubwa ambalo wananchi wa Mufindi tunamshukuru sana, katika mawasiliano pia kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hizi ni shukrani, lakini pamoja na hayo, nikiwa nachangia hotuba hii ya Waziri Mkuu, kuna mambo ambayo bado tunamwomba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Serikali yake, kuna mambo machache tunamwomba katika maeneo mahsusi. Moja, kama ambavyo wachangiaji wengi wamesema ni kwenye barabara za vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba pamoja na Wizara zake zote. Vijijini huko tuna changamoto kubwa. Sisi Jimbo la Mufindi Kaskazini ni wakulima. Tulianza kuhamasishwa kulima pareto miaka hiyo, na ndiyo maana unakuta kuna viwanda vingi na kiwanda cha pareto kiko Mufindi, kiko Mafinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wale kwa sababu ya changamoto kubwa na hasa kwenye miundombinu ya usafirishaji, sasa pareto imekufa na kiwanda kile kinahangaika kutafuta malighafi. Tukahamasisha zao lingine la chai. Chai nayo sasa inasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya changamoto ni ya barabara, na mambo mengine. Sasa hivi tumehamasisha kulima maparachichi. Ninaamini, kama miundombinu hii ya usafirishaji, hasa barabara itakuwa ni changamoto, ninaamini nayo yataanza kudoda kama ambavyo yamedoda mazao mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira kuu ya Wana-Mufindi Kaskazini ni kilimo. Sasa ninaomba, moja, tuone namna gani ya kuweka bajeti mahususi kwa *TARURA* kama ambavyo tulivyoweka kwenye *REA*, kwenye umeme. Umeme sasa umesambaa kwenye vijiji vyote, tunaenda kwenye vitongoji na mitaa. Tuone ni namna gani ya kuanza na mfuko maalum wa kuchangia kuhakikisha kuwa *TARURA* wanapata fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingi vijijini zipo chini ya *TARURA*; na mimi kwangu kule barabara nyingi ni hivyo. Wananchi wangu kule wamejiajiri. Sisi changamoto ya ajira tulishaanza kuitatua miaka ya zamani, tangu miaka ya 1970 wakati tunalima pareto na miaka ya 1980. Kwa hiyo, tunachotaka kuwezeshwa ni miundombinu wezeshi, na hasa barabara, ili tuweze kushafirisha mazao yale kupeleka katika viwanda na masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu hiyo, moja, tutafute namna kuwawezesha *TARURA* kupata fedha za kutosha ili tuhame kutoka kuwa na barabara za udongo tuseme kiwango cha chini kabisa cha barabara katika nchi yetu iwe angalau ya Changarawe. Hii itatusaidia kukuza uchumi katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, sisi kule ni wakulima wa misitu. Sasa baraka hizi za misitu zinaenda na changamoto pia. Barabara nyingi katika jimbo langu zinaharibika kwa sababu ya kusafirisha malighafi kubwa ya magogo, mbao, na bidhaa nyingine zinazotokana na misitu. Sasa wenzangu wa *TFS* ndio wanufaika wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maliasili watafute namna ya kuwafanya *TFS* nao kuanza kurejesha kama shukrani kwa wanachi ambao tulitoa maeneo yale bure kwa ajili ya kupanda miti. 60% ya misitu inayolisha viwanda vyote katika Wilaya ya Mufindi inatoka Jimbo la Mufindi Kaskazini. Tuone namna gani *TFS*

nao wanaweza kuchangia, kutengeneza, na kukarabati, kama Mheshimiwa mmoja alivyosema hapa kuhusu barabara zetu, ili wasafirishe malighafi hizo ambazo wanauzia wateja ikiwemo kiwanda kile cha *Mufindi Paper Mills (MPM)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika barabara hizi za lami tumeweka viwango kwamba isizidi tani kadhaa. Sisi barabra zetu kule hata tani 10 haziwezi kubeba, lakini yale magari yanabeba zaidi ya tani 40. Utaona ni namna gani Jimbo la Mufindi Kaskazini barabara zake zinachakaa kwa sababu ya kusafirisha mzigo mzito uliozidi uwezo wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan ametujengea barabara ya lami kilomita 14 Mtili – Ifwagi – Mkuta ambayo ninaamini itasaidia sana kusafirisha malighafi hizi kwa sababu imejengwa kwa viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo inachangia sana maendeleo ya nchi hii ni nishati ya umeme. Sisi kule katika Jimbo langu la Mufindi Kaskazini ambalo lina kata 11, kati ya kata hizo 11 kata sita zinahudumiwa na *Mwenga Hydropower*. Hawa ni sekta binafsi waonazalisha umeme na kuusambaza katika Jimbo la Mufindi Kaskazini kwenye zaidi ya vijiji 35. Ninavyoongea hii leo wananchi wenzangu wale kuna wakati mwingine wanapata umeme siyo zaidi ya masaa sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Mwenga Hydropower* tuliwashukuru sana walipoanza. Ni sehemu ya Kampuni ya *Rift Valley,* walikuwa wanazalisha ule umeme kwa ajili ya kulisha kiwanda cha chai Itona, pale *Stone Valley*. Kwa sababu umeme ulikuwa mwingi, tunashukuru walisaidia baadhi ya vijiji, lakini sasa wamepata changamoto, wakapata mkataba wa kulisha vijiji hivyo kata sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wizara ya Nishati, *EWURA* tutafute namna ya kuwapunguzia mzigo *Mwenga Hydropower*. Wanazalisha takribani *Megawatt* nne. Wakati wanahudumia vijiji vichache waliendelea kuwauzia *TANESCO,* sasa wamezidiwa hawawezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, *EWURA* na Nishati wawape mkataba wa kuwauzia *TANESCO* moja kwa moja, halafu vile vilivyobakia vihudumiwe na *TANESCO* badala ya *Mwenga Hydropower* ambao wameshindwa. Mimi hata kwangu ukiomba hata mita unaweza kuchukua mwaka mzima usipate *Mwenga Hydropower*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumbani kwangu sina umeme, nimewaomba kuingiza umeme Kijijini kwangu Nundwe hadi leo bado wanasuasua, wanasema subiri Mheshimiwa. Sasa kama kwangu mimi wanasema hivyo, je, wananchi wengine watapata huduma wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Wizara ya Nishati wawasaidie *Mwenga Hydropower.* Kama nilivyosema, sisi Jimbo la Mufindi Kaskazini suala la ajira kwa vijana, vijana wetu wanajiajiri sana kwenye shughuli za kilimo na kwenye misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto tuliyonayo, moja, barabara; pili, umeme ambao unasaidia kwenye shughuli mbalimbali za kiuchumi; na tatu, mikopo hii ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema, tuwasaidie vijana ili waweze kujiajiri, tupunguze changamoto ya kuomba ajira. Kila siku wanalia ajira, na mwingine akasema hadi waseme *connection* kwa ajili ya kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi kuhakikisha ninachangia kwenye hotuba hii. Ili tusiwakatishe tamaa wananchi wa Mufindi Kaskazini, moja, tuendelee kuboresha miundombinu ya barabara. Kama nilivyosema, tuwaongezee bajeti *TARURA,* lakini pili, *Mwenga Hydropower* wasaidiwe mkataba ule wao wawauzie umeme *TANESCO* badala ya wao kusambaza vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu, nakushukuru sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Exaud Kigahe kwa mchango wako. Mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana wa leo atakuwa ni Mheshimiwa Dkt. Regina Malima.

**MHE. DKT. REGINA C. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Bunge lako Tukufu. Kwanza kabisa, ninamshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kuwepo mahali hapa leo tukiwa na majukumu makubwa katika nchi, ili kuweza kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa nichukue fursa hii kwa moyo wa dhati kumpongeza Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono makubwa katika Taifa letu na namna ambavyo ameendelea kufanya kazi kwa kugusa maeneo mbalimbali ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, pamoja na yote haya tumeona kuwa amekuwa ni Rais wa kwanza kuhakikisha kabisa Taifa linakuwa na mpango wa maendeleo wa muda mrefu wa mwaka 2050. Hili ni jambo kubwa ambalo Mheshimiwa Rais amelifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza watendaji wake wote ambao ni wasaidizi kuanzia Makamu wake wa Rais, Mheshimiwa Nchimbi, pia Mheshimiwa Waziri Mkuu na watendaji wote katika Wizara zote, bila kusahau watendaji katika nafasi mbalimbali za mikoa, wilaya hadi huku chini, na sisi Waheshimiwa Wabunge kwa namna moja au nyingine tumekuwa tukimsaidia Rais kuhakikisha kwamba maono haya yanafikiwa kama ambavyo amepanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipitia kwa kina hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, imesheheni *data* katika kila eneo. Hiki ndicho kinachotakiwa kufanyika tunapokuwa tukitoa taarifa mbalimbali. Kwa maana hiyo, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameonyesha hili na amegusa maeneo yote. Sekta mbalimbali zimeonekana na namna ambavyo *output* zinaonekana kwa kila eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa sababu yeye ndiye anaye-*facilitate* haya yote kuhakikisha yanafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, nitakuwa na mambo machache ya kuongea. Nitaongea kwenye sekta ya elimu, eneo ambalo pia nimekuwa ni Mbunge mwakilishi wa kundi la vyuo na vyuo vikuu, kwa namna ambavyo nchi imekuwa na mwelekeo katika kuboresha sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ni msingi wa dira ya mwaka 2050. Sambamba na malengo mengine ya muda mfupi, na hata ya muda wa kati, kwa nini tuboreshe elimu? Ni katika elimu hii ndipo tunapata nguvu kazi yenye ujuzi. Ni katika elimu ndipo tunapata wahitimu mahiri ambao wanaenda kukabiliana na changamoto za karne za 21. Ni katika elimu, endapo itaboreka ndipo tutapunguza suala la umasikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja hayo, ninapongeza juhudi kubwa ambazo zimefanyika na Serikali. Tumeona mageuzi makubwa katika elimu ya msingi, elimu ya sekondari na elimu ya juu, kwa maana ya vyuo na vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya mikopo imeongezeka, miundombinu imeboreshwa, na mambo kama hayo, yamesaidia vijana wetu kusoma katika mazingira ambayo ni rafiki kwa ajili ya masomo yao. Uwekezaji huu ni muhimu ili kujenga Taifa lenye watu wenye ujuzi, lenye watu wenye maarifa na uwezo wa kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo nchi Barani Afrika ambazo zimewekeza katika elimu na wamefika mbali. Kuna nchi ya Rwanda wamewekeza katika elimu ya msingi, na pia katika elimu ya TEHAMA. Hivi sasa tunavyoongea Rwanda inaongoza katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunayo nchi ya Botswana, wao wametenga fedha inayopatikana kutoka katika sekta ya madini na kuiwekeza kwenye elimu. Mambo kama hayo yanaleta tija kwa sababu elimu inapoboreka ndipo ambapo tunapata wanafunzi au wahitimu mahiri ambao watakuwa na faida katika Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada zote hizi, kuna changamoto moja ambayo binafsi kama mtaalamu na mtafiti nimeendelea kuiona. Changamoto hii ni kuhusu ubora wa elimu sambamba na ujuzi wa wahitimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona namna ambavyo Wabunge wamekuwa wakichangia na kuona kabisa kwamba kuna changamoto ya ajira, kuna changamoto ya vijana wengi kuwa katika mitaa, na kadhalika na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti zinaonyesha kuna changamoto ya ubora wa elimu na ujuzi wa wahitimu. Eneo hili ni muhimu sasa Serikali iliangalie. Mheshimiwa Rais amefanya mageuzi makubwa sana kwenye miundombinu na kwenye mambo kama hayo, lakini bado eneo la ubora wa elimu ni changamoto katika nchini yetu, sambamba na ujuzi wa wahitimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali yangu iliangalie eneo hili, na lipo katika maeneo mawili. Tunaposema ubora wa elimu, kuna wanafunzi au wahitimu, lakini pia kuna waalimu au wahazili. Kila mwaka takribani wahitimu 50,000 hadi 70,000 wanahitimu kutoka katika vyuo vikuu. Hapo bado hatujaweka watu au wahitimu wanaotoka kwenye Vyuo vya *VETA* na kwenye vyuo vya kati. Sasa hawa wote wanatengeneza zaidi ya 50% ya wahitimu wetu kukosa ajira, iwe ni za kujiajiri au zile ajira ambazo ziko katika mfumo rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujiulize, ni kwa nini vijana wengi wanakosa ajira? Kwa nini vijana wengi wako mtaani? Sasa basi, ni muhimu Serikali kutafuta ufumbuzi katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali tuangalie pia wahadhiri au waalimu ambao wamekuwa wanafundisha, hasa katika eneo la vyuo vikuu. Kumekuwa na changamoto. Juzi tulikuwa na ziara katika baadhi ya vyuo vyetu nchini, tumekuta mtu ambaye amepata *demotion* kwenye taasisi fulani anapelekwa kwenda kufundisha. Hii haikubaliki kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kabisa taasisi hizi zina vigezo vya namna ambavyo zinapaswa kupata wahadhiri au

waalimu. Mtu ambaye amepata *demotion,* anaendaje kufundisha mwanafunzi? Hii haikubaliki kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuangalie ujuzi wa vitendo au ubunifu wa hawa vijana wetu, namna ambavyo wako katika eneo hilo vizuri. Pia uwiano wa ujuzi na uhitaji wa soko la ajira ukoje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba Wizara zinazohusika ziliangalie suala hili. Pamoja na uwekezaji mkubwa katika eneo hili, kuna haja ya kuangalia ubora wa elimu, ili tuweze kupata *products* ambazo zitakuwa ni nzuri za kuweza kuajirika na pia kujiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nisemee upande wa wahadhiri. Mheshimiwa Waziri wa Elimu yuko hapa ananisikia. Kuna changamoto moja ambayo wahadhiri wamekuwa wanakutana nayo. Tuna vyuo vikuu ambavyo viko chini ya *TCU*, pia kuna taasisi nyingine ambazo ziko chini ya *NACTVET*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa *TCU retirement age* ni miaka 65, lakini upande wa *NACTVET retirement age* ni miaka 60. Sasa nimekuwa nikifanya ziara mbalimbali kuonana na wadau hawa. Wengi wanaomba *retirement age* iwe sawa, *TCU* pamoja na *NACTVECT,* kwa maana ya miaka 65 kwa wote wanaofundisha katika hizi taasi zetu. Hiyo itasaidia kuendelea ku-*maintain* wahadhiri ambao wana uzoefu ili waweze pia kuendelea kutoa huduma hiyo kwa wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine amblo ninataka niliongelee, ni kuhusiana na vyuo vyetu vya kati. Mheshimiwa Rais amewekeza sana, hadi sasa tuna vyuo vya *VETA* takribani nchi nzima, lakini vyuo hivi bado havina *programs* ambazo zinahusu eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoa mfano, kule ninakotokea mimi, Wilaya ya Ukerewe tuna Chuo cha *VETA*. Katika chuo hiki 99% ya watu wa Ukerewe tuna-*depend* kwenye uvuvi, lakini cha kushangaza Chuo hiki cha *VETA* hakina *program* yoyote ambayo inahusiana na masuala ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukilipigia kelele jambo hili. Vyuo hivi mahali vilipo viendelee kutoa *programs* ambazo zitawanufaisha wale walengwa au wanaokaa maeneo husika. Nina imani kabisa kuwa ushauri huu utafanyiwa kazi ili tuweze kuwa na wanufaika wanaotoka katika maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo moja ambalo nitaomba niligusie kidogo kuhusu ajira kwa vijana. Tumeona kabisa kila Mbunge anapiga kelele kuhusu ajira, lakini uwekezaji mkubwa umefanyika. Ninaomba *coordination* ya miradi mbalimbali ya vijana ambayo Mheshimiwa Rais ametenga iweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, na ufuatiliaji. Tumeona mambo ya ufuatiliaji yakiwa *raised* na watu, na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali hapa. Kwa hiyo, ninaomba Bunge lako Tukufu liweze kuhakikisha huduma hizi zinapatikana kwa vijana na kuondoa changamoto kubwa ya vijana ambayo inaonekana kuwa tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Regina ahsante kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu kwa mchana wa leo. Ninaomba niwataje watakaoanza kuchangia jioni, Mheshimiwa Haidary Hemed Sumry, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mheshimiwa John Stephano Luhende, Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule, na orodha itaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kukumbusha jambo moja. Kanuni yetu ya 76(3)(c) inatuelekeza au inatukataza kupita mbele ya Kiti cha Spika na Mbunge anayezungumza. Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tukumbuke kuzingatia Kanuni hii.

Nina tangazo limetoka kwa Mheshimiwa Agnes Hokororo, Katibu wa Wabunge wote wa Chama cCa Mapinduzi, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote wa Chama Cha

Mapinduzi kuwa kesho kutakuwa na Mkutano wa Chama *(Party Caucus)* utakaofanyika katika ukumbi wa *NEC* kuanzia saa tatu asubuhi. Wabunge wote wa Chama Cha Mapinduzi wahudhurie bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kusitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.56 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Cecilia D. Paresso) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tunaendelea na majadiliano. Sasa ninamwita Mheshimiwa Haidary Hemed Sumry, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, ajiandae.

**MHE. HAIDARY H. SUMRY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niendelee kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mpanda Mjini kwa kuniamini na kunichagua kuwa Mbunge wao, niendelee tu kuahidi kwamba sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri ambayo ameifanya kwenye Jimbo letu la Mpanda Mjini. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Jimbo letu la Mpanda Mjini limepiga maendeleo makubwa sana. Ninaomba tumpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri ambao anashirikiana nao katika Ofisi yake. Ni ukweli usiopingika kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu anafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 16, Machi, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa kwenye jimbo langu la Mpanda Mjini. Kwa namna ya pekee ninamshukuru sana sana sana kwa kazi kubwa aliyoifanya kwenye jimbo hili. Ametatua kero za wananchi wengi, lakini amesikiliza changamoto za wananchi wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, mimi kama Mbunge wa jimbo nilipata fursa ya kufikisha hoja zangu kwa maana ya changamoto za Jimbo la Mpanda Mjini, na Mheshimiwa Waziri Mkuu alizichukua na ninaamini katika bajeti ijayo zitafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, ninapenda kuwashukuru viongozi wangu wa Mkoa wa Katavi, kwa maana ya Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Katavi Mheshimiwa Mwanamvua Hoza Mrindoko kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya kwenye Mkoa wetu wa Katavi. Pia, na dada yangu Jamila Yusuf Kimaro, Mkuu wa Wilaya ya Mpanda, naye kwa kazi nzuri anayoifanya kwenye wilaya yangu ya Mpanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imeeleza wazi mambo mengi ambayo yalitekelezwa katika kipindi kilichopita ambacho tunaenda kuishia mwezi Juni, lakini matazamio na matarajio ya bajeti ijayo. Sasa mimi nitajikita kwenye maendeleo kwa sababu Mkoa wa Katavi ni mkoa mpya na mambo mengi yalikuwa hayajafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na eneo la nishati kwa maana ya umeme. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri aliyoifanya kwenye mkoa wetu kwa kuhakikisha Mkoa wa Katavi, unaunganishwa na gridi ya Taifa. Kwa kweli watu wa Mpanda sasa hivi nao wamekuwa kama watu wa mikoa mingine, lakini kubwa zaidi imepunguza mzigo kwa *TANESCO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu na mkoa wetu wa Katavi tulikuwa tunatumia *generators* ambazo zilikuwa zinaendeshwa kwa gharama kubwa, lakini kwa namna Serikali ilivyofikisha gridi ya Taifa, tunaamini sasa gharama za *TANESCO* zimeondoka na tunaamini sasa *TANESCO* inaanza kupata faida kwenye eneo letu la Mkoa wa Katavi, na pia kwenye jimbo langu la Mpanda Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hilo hilo la *TANESCO,* niendelee kuwaomba watu wa *TANESCO,* Mheshimiwa Waziri Mkuu atusaidie na watu wa Wizara ya Nishati watusaidie kupeleka kwenye maeneo ambayo yanahitajika ujazilizi wa umeme. Pale kwenye eneo langu la Mpanda Mjini kuna kata ambazo bado zina changamoto, ni kata ambazo ziko mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Mpanda unakua kwa kasi. Kwa mujibu wa Sensa, Mkoa wa Katavi unakua kwa karibia asilimia saba kila mwaka. Kwa hiyo, utaona ni namna gani Mkoa wa Katavi unavyokua kwa kasi na Mpanda Mjini ndiyo kitovu cha maendeleo ya mkoa wetu. Kwa hiyo, tunapoongelea kukua kwa asilimia saba, tafsiri yake ni kwamba asilimia saba hiyo itatafsirika kwenye jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba sana kwenye Kata za Shanwe ambapo umeme umefika lakini kuna maeneo mapya ambayo yanajengwa bado umeme haujafika na ningeomba ufike. Vilevile, kwenye kata ya Kazima nako umeme umefika lakini bado kuna maeneo mapya ambayo yamejengwa na umeme bado haujafika. Kata ya Nsemulwa, Kata ya Misunkumilo, Kata ya Magamba, Kata ya Kakese, na kata ya Mwamkulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo hayo bado tumefikishiwa umeme, lakini kwa kuwa kuna makazi mapya yanajengwa, kwa hiyo, kuna uhitaji mkubwa wa maeneo yale mapya. Kwa hiyo, ningeomba sana Wizara ya Nishati katika bajeti ijayo waangalie namna ya kutuongezea bajeti ili umeme uweze kufika kwa wananchi, nao wafurahi na watabasamu kama Mheshimiwa Rais alivyotuahidi tabasamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hilo hilo ningeomba kuiomba Serikali itusaidie kujenga ile njia ya umeme ambayo sasa hivi kuna kazi inaendelea kufanyika pale Mkoa wa Ruvuma kwa maana ya Sumbawanga, lakini mradi huu unatakiwa uje Mkoa wa Katavi ufike pia mpaka Kigoma ili sasa tuondokane na changamoto kabisa kwa sababu tutakuwa na maeneo mawili ambayo tunategemea ya umeme hata ikipata changamoto, njia hii tutakuwa tunatumia njia nyingine ili kuendelea kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoka eneo hilo, niende sasa kwenye eneo la *TARURA*. Ninakiri wazi kwamba *TARURA* inafanya kazi nzuri, na kwenye jimbo langu imefanya kazi nzuri, madaraja mengi yamejengwa na tunafurahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi na Mheshimiwa Lupembe tunapakana majimbo yetu, na juzi tu hapa tumepata mkandarasi anakwenda kujenga daraja la karibia shilingi bilioni tatu ambalo linapakana na Kata ya Itenka - jimbo la Mheshimiwa Lupembe na Kata ya Mwamkulu ambayo ni jimbo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa fedha hizi alizotuletea, lakini bado tuna changamoto kwenye eneo hilo la jimbo langu na Mheshimiwa Lupembe, kuna daraja lingine ambalo linaunganisha Kata ya Kakese kwenye jimbo langu na Kata ya Itenka kwenye jimbo lake Mheshimiwa Lupembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja hili lilijengwa, lakini bahati mbaya lilisombwa na maji. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali irudishe huduma pale kwa sababu tunaamini daraja hili likijengwa litawasaidia sana wananchi wa majimbo yetu haya mawili kuweza kufanya biashara na kuongeza uchumi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la *TARURA* niendelee kuiomba sana TAMISEMI watusaidie kwa kweli kutuangalia kibajeti. Sisi Mkoa wa Katavi kwa neema ya mvua, basi sisi tunaweza tukawa ni namba moja kwenye nchi hii. Tumepata neema ya mvua kubwa na mazao yamelimwa sana na tunaamini wananchi wetu watavuna mazao kwa wingi katika msimu huu, lakini mvua hizi zimebadilika kuwa changamoto kwenye miundombinu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuwaombe ndugu zetu wa *TARURA* waweze kutuongezea fedha ili tuweze kwenda kukarabati hizi barabara ambazo zimeharibika katika kipindi hiki cha mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kuwashukuru, wanafanya kazi nzuri na kwa kweli Mungu awabariki sana na Mungu ambariki Mheshimiwa Waziri, Mungu aendelee kumbariki Mheshimiwa Rais, hata Mtendaji Mkuu wa *TARURA* anafanya kazi nzuri. Sisi Waheshimiwa Wabunge tukimpigia simu amekuwa ni msikivu, anatusikiliza na anatatua changamoto zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hilo hilo la barabara, Mji wa Mpanda ndiyo kitovu cha Mkoa wa Katavi kama nilivyosema awali. Tunazo barabara za lami karibia kilometa 20 zimejengwa kwenye jimbo langu, lakini hazina taa za barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba sana ndugu zangu viongozi wangu wa Wizara hii ya TAMISEMI watusaidie angalau kila mwaka tupate bajeti kidogo ambayo itaendelea kuzipunguza hizi barabara, *at least* katika miaka mitano ijayo basi tuwe tumemaliza hizi barabara kuziweka taa za barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika, tunapoweka taa za barabarani kwenye maeneo ya miji yetu, tunasaidia wananchi wetu, wafanyabiashara wadogo wadogo, wachoma mahindi, wachoma ndizi na wafanyabiashara wadogo wadogo wananufaika na haya maeneo hasa wakati wa jioni wanaweza kufanya biashara zao. Kwa hiyo, niendelee kuomba sana sana sana kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la *TARURA* pia tuna fedha za mfuko wa jimbo...

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. HAIDARY H. SUMRY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Nilimtaja Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, wajiandae Mheshimiwa John Luhende na Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema kuniwezesha siku ya leo kuweza kusimama hapa katika Bunge lako hili Tukufu niweze kuongea machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya katika nchi yetu. Ni ukweli usiopingika, Mheshimiwa Rais wetu anaibadilisha Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kuijua Tanzania ilivyokuwa miaka 10 kwenda nyuma, na leo, tuna mabadiliko makubwa sana. Huo ni ukweli na utaendelea kuwa ukweli na utakuwa ukweli ukweli ukweli. Tanzania imebadilika na aliyeibadilisha ni Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa vile ni mara ya kwanza napenda nikipongeze chama change, Chama cha Mapinduzi na kukishukuru, kuanzia ngazi ya Taifa, mkoa, wilaya, kata, tawi mpaka kwenye mashina pamoja na wale Wajumbe wa Mashina kwa kuniwezesha kunipa kura nyingi za kishindo, lakini chama changu ngazi ya Taifa kikaweza kunichagua kuwa mgombea wa Ubunge katika Jimbo la Temeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakishukuru sana Chama cha Mapinduzi kwa kuniamini na mimi nawaambia kama chama, sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naomba niwashukuru wapigakura wangu wote wa Jimbo la Temeke, hakika walinipa ushindi wa kishindo, ushindi uliotukuka. Kipekee napenda niwashukuru na kuwapongeza wale wote wagombea wenzangu 17 kutoka vyama mbalimbali katika Jimbo la Temeke kwa kuniunga mkono na kunisaidia baada ya kumaliza uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo moyo wa kizalendo. Ninawashukuru sana vyama vyote, tuko pamoja tunajenga pamoja Temeke yetu na ninawaambia karibuni sana katika Ofisi ya Mbunge Jimbo la Temeke muweze kutoa maoni yenu, kuleta yale ambayo mliyakusudia wakati mnagombea. Sasa mimi ndiye niliyapata Ubunge, karibuni tushirikiane tuijenge Temeke yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninawashukuru na nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwanza kwa kuteuliwa kwake, na kwa kuwasilisha vizuri sana hotuba yake ya bajeti ya mwaka huu 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote walioteuliwa na waliochaguliwa, wanafanya kazi nzuri. Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Manaibu Katibu Wakuu na watendaji wote wa Serikali. Hakika katika kipindi hiki kifupi wameweza kutupa ushirikiano wa kutosha kabisa. Tunashukuru sana, endeleeni kuchapa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa siku ya leo, nitajikita katika Wizara mbili; Wizara ya Kazi, Ajira na Mahusiano na TAMISEMI. Katika Wizara ya Ajira na Mahusiano, ninampongeza sana Mwenyekiti wangu wa Kamati, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wenzangu wa Kamati hiyo. Hakika Wizara hii imefanya kazi kubwa sana, tumeona miradi yao, tumeona mambo mbalimbali ambayo walipanga kuyafanya katika awamu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika wanafanya kazi nzuri sana. Mimi nitaingia kwenye maoni ya Kamati yetu. Tumeielekeza Serikali kwamba wafike sehemu waangalie jinsi ya kuongeza fedha katika ile *project* ya uanagenzi. *Project* ile ni muhimu sana kwa maendeleo ya kijana, ukizingatia Taifa letu sasa hivi tumelimbikwa na ukosefu wa ajira, Serikali haiwezi ikaajiri watu wote na sekta binafsi haiwezi ikajiri watu wote. Hivyo, mpango wa Serikali wa kuamua sasa kuwapeleka vijana katika mafunzo ya uanagenzi baadaye wakimaliza, waweze kujiwezesha wenyewe kwa kufanya shughuli mbalimbali za kuwaongezea kipato, ni mpango mzuri sana sana sana na changamoto iliyopo ni ukosefu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba Serikali wawaongezee fedha kwa sababu ukiangalia bajeti, mwaka 2023/2024 walitakiwa wapewe shilingi 119,641,000,000 lakini kiasi walichopewa ni shilingi bilioni tisa. Ni kiwango kidogo sana. Najua hakuna kidogo, hata kidogo ni kikubwa, lakini kwa jinsi inavyoonekana na mwitikio wa vijana kwenda kujiunga kwenye hizo kozi, bado fedha zile hazitoshelezi. Tunaomba Serikali wawape fedha waweze kuendeleza hiyo kozi za uanagenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye mwaka 2024/2025 walitakiwa wapewe shilingi 77,000,858,000, lakini kiasi walichopata ni shilingi 10,800,000,000, bado ni kiwango kidogo. Ninaiomba Serikali katika bajeti hii, waangalie namna gani wanaweza wakaongeza bajeti hiyo kuwasaidia vijana. Sambamba na hilo, naomba utaratibu mzima wa kuwapata hao vijana uanagenzi uangaliwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninatoka Temeke na nimehudumu katika Kamati hiyo awamu iliyopita na awamu hii. Nimezunguka katika vyuo mbalimbali vya uanagenzi, sikuwahi kumwona hata mtoto mmoja aliyetoka Temeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, fursa hii lazima tugawane sawa. Fursa hiyo ya uanagenzi na kama itawezekana irudishwe kwenye halmashauri zetu tuone hapa Halmashauri ya Temeke waliokwenda kwenye mafunzo ya uanagenzi kutoka

kwenye Mfuko wa Ofisi ya Waziri Mkuu ni 20, Halmashauri ya Ubungo wamekwenda 20 na nyingine. Tukienda hivi nafikiri kila mmoja na kila kijana atafaidika na keki ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwenye suala zima la uanagenzi, lakini pia kwenye hiyo kodi ya *SDL* ambayo wanakatwa wafanyakazi katika sekta binafsi pia waangalie kwa sababu sekta binafsi ndio uti wa mgongo wa Taifa letu. Wao wanabeba watu wengi zaidi katika ajira zetu kuliko Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo sekta binafsi iangaliwe kwa sababu wao wanao wafanyakazi, lakini wale walioko viwandani na wao kama binadamu fungu hili zamani kabla halijaingizwa kwenye uanagenzi kupelekwa kwenye vyuo vikuu na maeneo mengine, lilikuwa linawasaidia wafanyakazi wa sekta binafsi na wao wakapate angalau *refresher course* ya zile kazi zao wanazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika mpango ule ule tuhakikishe kama kuna viwanda viko katika eneo husika basi na wao watoe hata wawili au watatu waingie kwenye zile kozi kujiongezea ujuzi. Mtu akienda pale, kama alienda mbeba mizigo, hapana afike sehemu awe hata fundi bomba. Afike sehemu; ndiyo namna mwananchi wetu wa Kitanzania na yeye anaweza akapata *promotion* akiwa katika sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza sana Wizara ya TAMISEMI, Mheshimiwa Waziri na timu yake wanafanya kazi nzuri sana, lakini pamoja na kazi nzuri, bado kuna limbiko la watu maeneo fulani. Katika Jimbo langu la Temeke kwa mujibu wa sensa, nina takribani watu 570,000, lakini ninaishukuru TAMISEMI imejenga shule za sekondari katika kata zote, bado kata moja ambayo shule bado inajengwa, lakini hata hivyo haiwatoshelezi vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Shule ya Sekondari ya Buza ina watoto 1,889. Shule moja ina vyumba vya madarasa 14. Vyumba vinne vinavuja nyang'anyang'a kabisa. Mvua ikinyesha

watoto hawawezi kusoma madarasani, hiyo ni changamoto tuangalie katika bajeti zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza sana Serikali, ilikwenda kwenye vile vyuo, shule za sekondari chakavu za muda mrefu, *project* hiyo imefanya vizuri sana. Sasa ije na mpango wa awamu ya pili ya kuboresha majengo na shule chakavu ili sasa vijana wetu waweze kusoma vizuri. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante, muda wako umeisha.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, lakini ninaomba pia kwenye sekta ya afya, nina Zahanati ya Sandari bado na Zahanati ya Kata ya Temeke. Kata ya Temeke ni kata mama, ilikuwa inategemea hospitali ya Temeke, lakini ile imekuwa ya rufaa, tunatakiwa tuanzishe hospitali. Ninaomba sana Serikali waangalie jinsi gani ya kupata zahanati au kituo cha afya katika Kata ya Temeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa John Luhende ajiandae, Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule na Mheshimiwa Henry Charles Kabeho ajiandae.

**MHE. JOHN S. LUHENDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii nami niweze kutoa niliyonayo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nianze kwa shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufika hapa leo nikiwa salama salimini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani za pili zielekee kwa Serikali yote ya Chama Cha Mapinduzi ikiongozwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Shukrani za tatu zielekee

jimboni kwangu kwa wananchi wote wa Jimbo la Bukene kwa kunichagua kwa kura za kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi mingi ambayo Serikali ya Awamu ya Sita imefanya ndani ya Jimbo letu la Bukene. Tunashukuru sana kwa hilo, lakini kulingana na uchache wa muda ninaomba nielekeze kwa mambo ambayo ni changamoto kubwa sana ndani ya Jimbo letu la Bukene.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Bukene hatuna stendi ya abiria. Wananchi wa Jimbo la Bukene walioko huko hawana usafiri kwa sababu hatuna stendi hata moja ndani ya jimbo letu la Bukene. Kwa hiyo, ninaomba Serikali kwenye mipango ya bajeti hususan Ofisi ya Waziri Mkuu uwekwe mpango wa stendi ndani ya Jimbo letu la Bukene. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, miundombinu ya barabara ndani ya Jimbo la Bukene ni mibaya, hairidhishi, ina changamoto kubwa na kwa kipindi hiki cha masika ni barabara nyingi sana hazipitiki. Baadhi ya mifano ya barabara ambazo ni changamoto kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI wanatakiwa wazishughulikie ni Barabara ya Sigiri - Bulende, barabara ya Itobo - Kalitu, barabara ya Mwamala - Ikindwa hadi Uduka, barabara ya Ngwatu hadi Gulyambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefikia mpaka mahali wananchi wanalazimika kukusanya magogo ili waweze kutengeneza daraja la dharura ili waweze kuwa wanapita kutoka maeneo ya Ngwatu kuelekea Gulyambi ambako ndiko kuna zahanati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Bukene tuna changamoto katika idara ya afya, kwa mujibu wa Sera ya Afya tuliyonayo ya nchi hii kwamba kila kata angalau iweze kuwa na kituo cha afya. Jimbo la Bukene tuna kata 17, lakini tuna vituo viwili vya afya: Itobo na Bukene. Vituo hivi vya afya vimeelemewa sana na mbaya zaidi kwa sasa hivi tunatumia *control* namba kulipia ili tuweze kupata huduma za kiafya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwenye hivyo vituo hatuna uhakika wa huduma ya kifedha. Mawakala hawapo pale na

wananchi hawatibiwi pasipo kuwa wamelipa ile fedha ambayo wanatakiwa walipe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba Serikali kupitia TAMISEMI ihakikishe kwamba mnaweka mawakala pale wafanye kazi masaa 24 ili wananchi wa Jimbo la Bukene waweze kupata huduma za kifedha kwenye vituo hivyo vya afya. Pia, tunazo kata mbalimbali ikiwemo Kata ya Mambali, Kata ya Semembela. Kata ya Mambali peke yake ina wakazi takribani 30,000, na Kata ya Semembela ina wakazi takribani 23,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kata nilizozitaja zote mbili hazina hata kituo kimoja cha afya. Wanatumia zahanati na zahanati hizo zilizoko kule zimezidiwa. Kwa hiyo, ninaomba kuishauri Serikali kupitia TAMISEMI wahakikishe kuwa katika mipango yao ya bajeti wanaweka kipaumbele kwenye hizo kata mbili za ndani ya Jimbo la Bukene. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya elimu ndani ya Jimbo la Bukene tunazo changamoto nyingi. Jimbo letu la Bukene hatuna shule ya sekondari ya kidato cha tano na cha sita. Zilizopo ni mbili tu ambazo zimeanzishwa hivi karibuni; na zina-*accommodate* wasichana, kwa maana ya wanafunzi wa kike, iko moja pale Mwangoye na nyingine ipo Kili pale Uduka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watoto wa kiume, ndani ya Jimbo la Bukene hawana shule ya kwenda kusoma kidato cha tano na cha sita. Elimu hiyo ya kidato cha tano na sita ndiyo daraja pekee la kuwawezesha wanafunzi wetu waweze kuelekea chuo kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba kuishauri Serikali iweze kuliangalia hilo na ihakikishe kwamba angalau tuanze kwa shule mbili. Jimbo langu lina tarafa mbili. Kuna Tarafa ya Bukene na Tarafa ya Mwakalundi, angalau shule moja kila tarafa tuweze kuwasaidia watoto wa kiume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninataka kuzungumza kwa niaba ya Halmashauri ya Wilaya ya Nzega. Shughuli zetu nyingi tumejikita kwenye kilimo, ufugaji na biashara

kidogo, lakini kwa sasa hivi kuna shughuli ambayo inaajiri vijana wengi sana, shughuli ya uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli ya uchimbaji wa madini imeingia dosari katika Wilaya ya Nzega. Eneo ambalo tunajishughulisha kwa uchimbaji huo ni eneo la Lusu, Nata na Mwangoye. Eneo la Lusu zamani kulikuwepo na mgodi mkubwa wa *Resolute*. Waliweza kuachia eneo hilo na wananchi wakawa wanaendelea kujishughulisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa limekuja jeshi, wanataka kuchukua hilo eneo kwa ajili ya mambo yao ya kijeshi. Hata hivyo, ukiangalia sisi kama Mkoa wa Tabora, ndio mkoa mkubwa kuliko yote nchini nzima na tuna kambi nyingi sana za kijeshi. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba Serikali tuwape fursa mikoa mingine kuweka kambi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kambi tulizonazo za kijeshi ndani ya Mkoa wa Tabora zinatutosha. Eneo hilo sasa libaki kwa ajili ya shughuli za kiuchumi za wananchi ikiwemo kilimo, ufugaji pamoja na uchimbaji wa madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya milima ambayo jeshi wanachukua ni ile milima ya dhahabu. Kwa hiyo, wananchi hatuna sehemu nyingine ya kufanya kazi hiyo ya uchimbaji wa madini ya dhahabu kwa sababu ndiyo eneo pekee tunalotegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba wakati wizara wanakuja kutoa mrejesho wa majibu, waje na majibu ya kuhusiana na hili suala la jeshi kuchukua eneo la uchimbaji wa madini ambalo wananchi wa Wilaya ya Nzega wanaendelea kulitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nijikite kwenye kuishauri Serikali kwenye hoja mbalimbali za Kitaifa. Ninaomba kushauri kuhusu uendeshaji wa Serikali. Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa akihutubia mkutano, alizungumza kwamba anaagiza ma-RAS ili wawe wanatoa taarifa ya fedha zinazokuja kwenye miradi ya maendeleo ndani ya majimbo yetu, wawe wanatuandikia barua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kitu kimoja. Tunatakiwa twende na wakati tulionao sasa hivi. Wanatakiwa wa-*digitalize* mfumo mzima wa uendeshaji wa Serikali, hasa kwenye masuala ya kifedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kwenye halmashauri ama kwenye wilaya, tuna watu kama wafuatao: Mkuu wa Wilaya, *DAS, OCD, DSO,* Mkuu wa TAKUKURU, Magereza, Mwenyekiti wa Halmashauri, na Mbunge. Utengenezwe mfumo ambao fedha ikingia kwenye halmashauri kwa ajili *maybe* ujenzi wa kituo cha afya katika Jimbo la Bukene, *message* hiyo i-*click* iingie *notification* kwa watu wote hao; iingie kwa *OCD,* iingie *notification* kwa TAKUKURU, kwa Mbunge, kwa Mwenyekiti wa Halmashauri na wengine wote wakubwa wakubwa ambao wanahusika na masuala haya ili kuongeza uwazi Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo tutapunguza *speed* ya ubadhilifu uliopo ndani ya Serikali na muda mwingi sasa tunaotumia kuzijadili taarifa ya *CAG,* tutatumia kufanya mambo mengine kwa sababu mkiwa wengi ambao mna taarifa juu ya hilo suala, tutaweza kuu-*control* wizi kwa urahisi zaidi, kwa sababu watu 10, watu nane hawataweza kuelewana kucheza dili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi mifumo ya ulipaji kwa mkandarasi, inaifanyika kama kuwa siri. Unakuta mkandarasi amelipwa 100%, mradi uko 20%. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba, mkiweka uwazi siku ambayo mkandarasi analipwa 100% ya mradi mzima, watu wote hao wanapata *notification*. Kwa hiyo, walio na uwezo sasa wanaweza ku-*intervene* na ku-*control* fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, juzi hapa tumekumbwa na tatizo la uhaba wa mafuta. Ninaishauri Serikali tutafute suluhisho la kudumu, tuanzishe benki ya mafuta hapa nchini, yaani *the Petroleum Bank*. Ili wananchi tunapofanya shughuli zetu za kiuchumi, tunapoamua kuhifadhi mapato yetu, unaweza ukahifadhi katika mfumo wa mafuta.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha.

**MHE. JOHN S. LUHENDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie, hoja yangu nataka kumaanisha kwamba, kwa mfano, sasa hivi tuna maghala ya mahindi, tuna maghala ya mpunga na kadhalika. Kwa hiyo, Serikali ijenge *underground storage facilities* kwa ajili ya mafuta na wananchi tutawekeza katika kununua mafuta, tutaweka kama akiba yetu, na Serikali ikipata dharura ya mafuta, wananchi tutawauzia mafuta hayo na kuwahudumia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mmheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule, ajiandae Mheshimiwa Henry Charles Kabeho na Mheshimiwa Bazilio Kapunda Mbwilo, ajiandae.

**MHE. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami ya kuchangia hotuba, mpango, na bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu sana kunifikisha siku ya leo na hata kunipa ujasiri na kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuchangia mchango kwenye mpango huu na bajeti hii mahususi ambayo ni kama jumuishi tu ya wizara nyingi ambazo zinafanya chini ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kabisa ninamshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa sana ambayo Rais amefanya. Kwa kweli tunasema kutoka kwenye dhati ya mioyo yetu ya kwamba amefanya kazi iliyotukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka kabisa alipoanza tu Urais, alihutubia wanawake wa Tanzania nzima kupitia wanawake wa Dodoma, akasema; "Jukumu hili ambalo nimepewa, tumepewa sisi wanawake wote. Hivyo basi twendeni tukafanye kazi kwa bidii, tuthibitishe uwezo wetu kwamba wanawake tunaweza." Kweli kabisa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan

ameweza kabisa na chenji imebaki. Shukrani nyingi nampa na kumpongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi nyingine za pili, basi ziende kwa Waziri Mkuu. Waziri wetu Mkuu toka alipoteuliwa amefanya kazi nzuri na hasa hapa juzi juzi ambavyo amepita kwenye ziara zake za kila halmashauri akisikiliza kero, na kubaini kero kwenye halmashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona watu wengi, makundi ya watu yakijitokeza wenye matatizo, kweli ametoa msimamo sasa kwa watendaji wote wa Serikali kuendelea kufanya kazi kwa haki. Yeye kama Msimamizi Mkuu wa Serikali, ametoa dira kwa wafanyakazi wengine wa Serikali kuendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani nyingine nazipeleka kwa Mawaziri wote na Naibu Mawaziri, wamefanya kazi kubwa kwa siku hizi 100 za utendaji wa Rais kwa awamu hii ya pili ambayo amefanya. Tumewaona, mimi Kamati yangu ya Utawala, Katiba na Sheria, tumezunguka na Mheshimiwa Ridhiwani kwenye ziara tulikuwa pamoja kila mahali. Kongole nyingi sana kwa Mawaziri na Naibu Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalize shukrani kwa Mwenyekiti wangu wa UWT wa Taifa, Mheshimiwa Mama Mary Pius Chatanda, ni Mbunge mwenzetu, lakini kwa kweli imetufurahisha sana Mbunge huyu kuwa miongoni mwetu sisi wanawake. Tumejisikia faraja kuwa na mwenyekiti wetu mahali hapa. Hivyo, inaonekana tuna nafasi kubwa wanawake kufanya maendeleo kwa niaba ya wanawake wenzetu Tanzania nzima kwa kuwa na mwenyekiti wetu hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, ninaomba sasa nitoe hoja zangu kupitia hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tumefurahishwa sana, kama nilivyosema, na utendaji kwa miaka hii minne ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, madarasa mengi yamejengwa, na shule zimejengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka takwimu zimetolewa hapa karibu madarasa 78,000 yamejengwa, lakini shule nyingi

sana. Watoto wetu walisoma kwenye shule mbovu sana, lakini sasa tuna shule za kisasa mpaka vijijini. Hii ni fahari kubwa sana kwa nchi yetu ya Tanzania hasa kwenye sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo na kwenye sekta ya afya, Rais amefanya na Serikali imefanya vizuri sana. Zahanati mpaka vijijini kabisa, lakini vituo vya afya, siyo hivyo tu, hospitali za wilaya, hospitali za mikoa, hospitali za rufaa, vifaa kwenye mahospitali yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi nyingi kwa Serikali yangu kwa kazi kubwa sana ambayo imefanyika. Mpango huu ambao umewakilishwa mahali hapa, tunaenda kufikia *level* nyingine Watanzania wenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupo kwenye uchumi wa kati, sasa tunaenda kwenye uchumi wa kati lakini wa juu. Kwa maana tunaenda kupanda kwa kutoa mipango mikubwa ambayo imepangwa kama itatekelezwa na kufuata kama tulivyopanga. Niseme tu kwamba, tunaweza kwenda kwa pamoja hivyo, sambamba na maendeleo yote pamoja na miundombinu, pamoja na huduma za kijamii ikiwemo hizo huduma za elimu, huduma za afya na miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaenda vizuri zaidi tukienda na huu uchumi shirikishi ambao tunashirikisha wanaume na wanawake kwenye maendeleo twende pamoja. Siyo hivyo tu, lakini tunaposema kwamba uchumi jumuishi, ni sekta zote zishirikiane kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama ni maji, wawe na kipande cha maendeleo; kama ni elimu, wawe na kipande cha maendeleo; kama ni afya, wawe na kipande cha maendeleo; kama ni kilimo ambacho ndiyo tunategemea Tanzania nzima, uchumi wetu utakuzwa na kilimo kwa 85%. Hata hivyo, sekta binafsi hatuwezi kuisahau ambako tunategemea katika Dira yetu ya 2025 mpaka 2050, *private sector* wana-*contribute* 75%. Huo ndio utakuwa uchumi shirikishi maana tunaenda wote kwa pamoja bila kuachana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposema hivyo, ninamlenga mwanamke. Sasa mwanamke lazima ashirikishwe kuanzia ngazi ya kupanga, kwenye utekelezaji, na pia ashirikishwe kwenye tathmini. Tukimwacha nyuma mwanamke, maendeleo hayataenda. Kwa hiyo, twende pamoja na wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *contribution* ya mwanamke katika maendeleo haya ni 80%, na ukimwendeleza mwanamke, moja kwa moja umeendeleza familia na moja kwa moja umeendeleza jamii. Hivyo basi, mipango yetu na bajeti yetu imhusishe mwanamke moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijikite katika kile kipengele cha uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Kuna mipango mingi imepangwa na ikiwemo hizi 10% za halmashauri. Ndugu zangu ni kitu ambacho kimekuwa faraja sana kwa wanawake, kama ukisikia michango mingi ya Wabunge, kila mtu amegusia kuhusu 10%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu hiki ni mtaji, wanawake wanahitaji mitaji kwa ajili ya biashara zao, kwa ajili ya miradi. Hivyo basi, Serikali i-*pay attention* na kitu hiki, na kukiangalia, na kukifuatilia kwa karibu sana ili kuona kama kweli kuna ugawaji sawa wa hizi 10%, na kuna ufuatiliaji wa karibu ili wale watendaji wanaokiuka kitu hiki, basi waweze kuchukuliwa hatua ili hao wanawake wapokee hiyo faraja yao ya 10%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kuna hizo shilingi bilioni 200 ambazo zimetengwa kwa ajili ya wajasiriamali ambazo zimewekwa benki. Hata hii pia ni faraja kubwa sana kwa wanawake. Uwekwe utaratibu mzuri wa kuhakikisha walengwa wanafikiwa na hii hela ili wanawake waweze kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu ukweli, mchango mkubwa ambao sisi wanawake tunataka katika Serikali yetu, la kwanza kabisa, wanawake wanahitaji hiyo mitaji. Hili ni hitaji la kwanza la wanawake. Pili, wanawake wanahitaji masoko. Wauze wapi biashara zao? Wanawake wafundishwe tu, wanaweza. Ukimfundisha mwanamke jinsi masoko yanavyopatikana au

namna hata ya kusafirisha bidhaa nchi za nje, wanawake wanaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo kuwe na *link* ya utengenezaji wa bidhaa na usafirishaji wa bidhaa, au kuwe na *link* ya utengenezaji bidhaa na masoko ili wanawake wakitengeneza bidhaa zao ziwe na ubora, lakini pia zipate masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ambalo wanawake wanahitaji, ni elimu. Elimu inayotakiwa ni elimu ya fedha, elimu ya ujasiriamali. Pia wanawake wapewe *skills* ndogo ndogo tu, jinsi ya kuwa na wazo la biashara na namna ya ku-*develop* wazo la biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, wafundishwe hata *skills* ndogo za kuandika *business plan*. Mwanamke ajifunze vitu hivyo ili ajue ya kwamba mradi wake ambao anaenda kuufanya utakuwa na faida au hauna faida? Hapo ndipo mwanamke apewe mkopo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. Ninaomba nimalizie kwa kusema kwamba wanawake watapata faraja kubwa sana wakipata hii mikopo na kama shida ni dhamana, ufunguliwe mfuko wa dhamana ambao utawasaidia wanawake na vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Henry Charles kabeho, Mheshimiwa Bazilio Mbwilo, ajiandae.

**MHE. HENRY C. KABEHO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni ya leo. Ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha sisi Wabunge wote

kupata nafasi hizi na kuingia leo hapa Bungeni tukiwa na afya njema kabisa. Tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninamshukuru sana Mwenyekiti wa Chama changu Cha Mapinduzi, daktari bingwa wa changamoto na matatizo ya Watanzania, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na kamati kuu yake kwa kuniteua kugombea nafasi hii katika jimbo langu baada ya kuongoza kura za maoni. Ahsanteni sana Kamati Kuu na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri za ulinzi, usalama na maendeleo ya nchi hii, kwani muda wote halali, anafikiria usalama na maendeleo ya nchi yake. Ninamwombea maisha marefu yeye na familia yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kutumikia vyema nafasi yake ya Umakamu wa Rais kumsaidia Mheshimiwa Rais, ninampongeza sana. Pia, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi kwani Uchumi wa Buluu tunauona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sijatenda haki nisipomshukuru au kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa kazi nzuri za usimamizi wa Serikali. Kazi zake tunaziona, akipambana na wezi na wazembe, akizunguka mikoani bila kuchoka kumsaidia Mheshimiwa Rais. Pongezi nyingi sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kusahau watu muhimu kabisa, wananchi wangu wa Jimbo la Igunga, bila wao pia nisingekuwepo hapa, walinipa ushindi mnono wa 91%, ahsanteni sana. Nitawatumikia bila kuchoka ndani ya miaka mitano Mwenyezi Mungu akipenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, imeonesha kujitegemea kwa fedha nyingi za shilingi trilioni 26. Pesa hizi ni nyingi, lakini sisi Waheshimiwa Wabunge tunaomba zioneshe *reflection* kwenye barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ndiyo tatizo kwenye majimbo yetu, kila Mbunge analia na barabara. Fedha hizi baadhi ziwekwe *TARURA*. Kwa hii bajeti ya *TARURA* ipelekwe kwa wakati na zipelekwe za kutosha kuweza kusaidia barabara majimboni kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba, jimboni kwangu kuna barabara ya kutoka Igunga – Mwalala – Lugubu – Itumba, tunaomba tupate fedha ikarabatiwe. Barabara za Mjini Igunga, tuliahidi kwenye Ilani, nazo zitengenezwe. Pia, kuna Daraja la Isugilo kwenye Kata ya Igunga. Watu wa Isugilo wametenganishwa kwa daraja hili. Limeharibika siku nyingi, wanafika kwa tabu kwenye Kata yao ya Igunga ili wasione wametengwa. Ninaomba tulitengeneze hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya maji, kuna Tanki la Bulenya. Tanki limejengwa, lakini wakati fulani kazi ilisimama muda mrefu. Baadaye nikaongea na Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso, mtu mstaarabu na msikivu sana, ameanza kupeleka fedha na tumepata mabomba, na yameanza kufungwa kwenye Kata ya Mwamakona kuelekea Kata za Kiningi'inila na Isakamaliwa. Pia, tunaomba safari hii, fedha zifike na miradi isisimame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Madiwani wana mishahara midogo, lakini ninajua uwezo wa nchi na tuna miradi mingi na hali siyo nzuri sana na wafadhili hawatupatii fedha za kutosha. Kwa hiyo, ninaomba au ninashauri halmashauri na Serikali zichangie. Serikali itoe na halmashauri, Wakurugenzi wajibane kidogo, wawape Madiwani fedha kidogo, ni watu muhimu sana kwenye maendeleo ya majimbo yetu na kata zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamkumbusha Mheshimiwa Waziri Shemdoe, tuliongea pembeni kuhusu *ambulance*. Alisema siku nyingi *ambulance* itakuja, haijaja. Sasa, leo ninamkumbusha mtani wangu, ni mtu mwema, rafiki yangu sana, ninaweka kwenye *Hansard* ili tupate *ambulance* moja hapo Igunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Igogo – Igurubi kuna mradi wa maji umesimama. Ninaomba nao uletewe fedha tuweze kwenda vizuri. Pia, tunaishukuru Serikali kwa kutuletea umeme vitongoji 69. Nguzo zimemwagwa kama mchanga, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia, Mwenyezi Mungu amsaidie kuishi maisha mazuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Ilani yake ya mwaka 2025/2030...

**MHE. FADHILI A. LIWAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. HENRY C. KABEHO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais aliahidi na ametekeleza. Pia, kuna barabara ya kwenda Igurubi kutoka Igunga, Mheshimiwa Rais ameleta fedha kiasi, imeanza kutengenezwa, panapitika vizuri, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. FADHILI A. LIWAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. HENRY C. KABEHO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata dawa na vifaatiba kwenye zahanati zetu, tunamshukuru Mheshimiwa Rais Samia. *(Makofi)*

**MHE. FADHILI A. LIWAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. HENRY C. KABEHO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wangu, Mheshimiwa Paul Chacha. Ninamshukuru Mheshimiwa Said Mkumba, Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa kusimamia Serikali vizuri katika mkoa wangu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Henry.

**MHE. HENRY C. KABEHO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote walionichagua. Kamati za siasa zote na mabalozi kwa kazi nzuri ya kunichagua na nitawatumikia kwa nguvu zangu zote. *(Makofi)*

**MHE. FADHILI A. LIWAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Henry, kuna taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. FADHILI A. LIWAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumpa taarifa mzungumzaji wetu mzuri kwamba Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inaendelea kuzingatia utekelezaji na kutoa fedha nyingi kwa ajili ya miradi yote ya maendeleo nchini. Jimbo lake ni moja kati ya maeneo ambayo tunaamini Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninampa hiyo taarifa ili aendelee kuchangia vizuri. *(Makofi)*

**MHE. HENRY C. KABEHO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaipokea taarifa yake nzuri na wananchi wa Igunga wanasikia...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Henry, kwa mujibu wa Kanuni, Mbunge akikupa taarifa inabidi Kiti kikutaje kwanza kama unapokea au unakataa taarifa hiyo ndiyo uendelee kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Henry, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. HENRY C. KABEHO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaipokea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, malizia mchango wako.

**MHE. HENRY C. KABEHO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaishukuru familia yangu, maana yake nimeisahau kabisa. Walikuwa hawalali, tunapambana pamoja kupata nafasi hii, na mwaka 2020 niliongoza kura ikawa bahati mbaya sikuteuliwa. Kipindi hiki nimeteuliwa, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia na kamati kuu yake na familia yangu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ninaunga mkono hoja, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru Mheshimiwa Henry Kabeho kwa mchango wako mzuri. Pamoja na changamoto ya macho uliyokuwanayo, umetoka kwenye *operation,* lakini umefanya vizuri, hongera sana. *(Makofi)*

Nilimtaja Mheshimiwa Bazilio Mbwilo, Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani na Mheshimiwa Aeshi Khalfan Hilaly wajiandae.

**MHE. BAZILIO K. MBWILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuongea katika Bunge lako hili Tukufu. Vilevile, mimi ninaamini upinzani siyo kusema hapana kwa kila kitu. Kilicho kizuri lazima kipongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa dhati ya moyo wangu nimshukuru Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hasa mimi nikiwa mkazi wa Wilaya ya Nkasi ambayo kipindi cha nyuma ilikuwa ni giza, tulikuwa kweli kwenye *peripheral* na sasa hivi ni tofauti kabisa. Wilaya yetu ya Nkasi sasa hivi inaweza kuwa inafahamika hata kwa watu wengi waliopo hapa. Ninasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ningependa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu hasa kwa ziara yake ya mwezi Machi ambapo alikuja Jimboni kwangu Nkasi Kaskazini. Ninaomba nitoe shukrani za wananchi wa Nkasi kwa maana kweli ziara hii imekuwa ni ya *win-win* kwa maana kwamba wananchi wenye kero zao hata wale wa shilingi 200,000 ziliweza kutatuliwa na papo kwa hapo wakaweza kulipwa fedha zao. Wananchi wanashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani hata Waziri Mkuu naye atakuwa amefaidi kuujua ukweli kwamba katika ngazi hizo kuna viongozi wengi hawatimizi wajibu kwa maana kwamba kesi ya shilingi 200,000 inamsubiri Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo limesaidia, na ninaamini katika ile timu yake iliyopo ya *monitoring and evaluation* itakuwa imeliona hilo, kwa sababu tuliambiwa tayari inazo *indicator* za kutosha. Kwa hiyo, itaweza kuona ni kwa namna gani hali hiyo iweze kuboreshwa kwa safari yake Mheshimiwa Waziri Mkuu asihangaike tena na kesi hizo bali ziweze kutatuliwa na viongozi waliopo katika ngazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa ninatokea wilaya ambayo uti wake wa mgongo ni kilimo, ninaomba vilevile niishukuru sana Serikali kwa kutuwezesha sisi wakulima wa Wilaya ya Nkasi pembejeo za ruzuku. Ninaomba nikwambie kwamba kwa msimu huu, Jimbo la Nkasi Kaskazini litavuna sana. Tegemea mavuno ya kutosha, zile *warehouse* ziandaliwe za kutosha kwani mavuno hasa ya mahindi yatakuwa ni mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa wilaya yetu, kilimo bado kina vikwazo ambavyo ninataka niishauri Serikali ikiondokana na hivyo, tunaweza tukavuna zaidi, tija ikaongezeka. Tatizo la kwanza ni hilo la wanyama; tembo. Kwa kweli limekuwa ni kero kubwa kweli kweli. Mimi na viongozi wa *TAWA* tunakesha kuwasiliana namna ya kuwafukuza tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi jana tu Kijiji cha Chongokatete kimevamiwa na kundi kubwa la tembo. Ninaishukuru *TAWA*, Wilaya ya Nkasi inafanya kazi vizuri sana. Sasa, ninaomba kuhusu tembo, uharibifu ule isiwe fidia. Ningeomba sana kushauri, iwe ni malipo sawa na uharibifu mwingine wowote. Kuna mifugo iko kule huwa inaharibu mimea ya wananchi, mabwana shamba wanafanya tathmini na fidia halisi inafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hawa nao ni mifugo. Wale ni wafugaji, hawa wengine ni wetu Serikali, ninaomba sana unapotokea uharibifu, tathmini ifanyike na malipo yasiwe fidia, bali yawe kwa kiwango cha uharibifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani suluhisho la kudumu katika kadhia hii ni kuweka fensi tu. Ingependeza kama tungeweka fensi maeneo yetu yote. Kwa Jimbo langu la Nkasi Kaskazini, ianzie Kalila ije hadi Masolo. Tukiweka fensi tutakuwa

tumekamilisha, tatizo hili tunaweza kuwa tumeliondoa kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, maono ya Mheshimiwa Rais wetu kuhusu kukuza kilimo nchini ni kwamba *by 2030* Tanzania itakuwa imejitegemea kwa suala la mbolea kwa 100%. Sasa, nina wasiwasi na kasi tuliyonayo kama kweli inaweza ikayafikia haya maono ya Mheshimiwa Rais. Ninaomba kutoa rai kwamba tuongeze kasi ya kujenga viwanda. Gharama tunayoitumia sasa hivi kuagiza mbolea kutoka nje ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutengeneze mbolea zetu *by* kipindi hicho kweli tuwe nayo. Sasa, ningetegemea nione kuanzia bajeti hii Waziri anasema nini kuhusu kuwa na viwanda vyetu vya mbolea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ruzuku za pembejeo, Waheshimiwa wenzangu wameongea, nami ningependekeza kwamba isiwepo namna yoyote ya kuondoa ruzuku katika awamu hii. Hii ruzuku iendelee, wakulima wetu bado ni wachanga, tukimwambia Mfuko wa *DAP* aununue kwa shilingi 120,000 uzalishaji utashuka sana. Kwa hiyo, ninaiomba Wizara husika, habari ya ruzuku ya pembejeo iendelee kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ninadhani ni wakati sahihi sasa hivi katika kukuza kilimo, tuwavutie vijana. Tunasema wanatoka vyuo vikuu hawana ajira, ajira wanapaswa kuwa nayo. Tunayo maeneo mengi sana yanayofaa kwa kilimo hasa Jimboni kwangu na wilaya kwa ujumla, lakini sidhani kwamba vijana watavutiwa na kutumia jembe la mkono, hilo sitarajii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashindwa nini sasa hivi kutengeneza viwanda vyetu hata kutengeneza *power tiller* au hata trekta? Tunazo taasisi zetu za majeshi, Nyumbu wanashindwa kweli kutengeneza *power tiller* au trekta? Ninaomba sana kwamba sasa tuwekeze zaidi kwenye kutengeneza viwanda kwa ajili ya zana za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niongelee suala la barabara. Mheshimiwa Rais alipokuja mwaka 2025 kwenye ziara

yake ya kampeni alituahidi sisi Watu wa Nkasi kutupatia barabara mbili kwa kiwango cha lami. Ya kwanza ni ya kutoka Namanyere – Kipili ambako kuna bandari. Barabara ya pili ni kutoka Lyazumbi – Kabwe, napo ni kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo hayo ni muhimu sana. Wakati uchumi wetu unakua kwa asilimia tano nukta tano mpaka asilimia sita, ninaamini ni kwa sababu hatujaweza kulitumia Ziwa Tanganyika. Kama hizi barabara zitawekwa vizuri, na hizi Bandari mbili za Kipili na Kabwe zikaimarishwa, ninaamini tutapata fedha nyingi kwa maana *Eastern Congo* kuanzia Mji wa Moba kuja Kusini wanategemea bandari hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba sana Wizara hizi mbili zinazohusika mzione hizi Bandari za Kabwe na Kipili pamoja na barabara zake kama lango muhimu kwa ajili ya uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nisikie kauli ya Serikali maana ninaona kama vile ina utata. Je, *children under five* wanatakiwa walipie matibabu? Akina mama wajawazito kwa huduma za kliniki, iwe wazi nao je, walipie? Wazee zaidi ya miaka 60 tunasemaje? Maana kunakuwa na kauli tofauti tofauti. Ningeomba hilo liweze kufafanuliwa vizuri katika kikao chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nkasi bado ina changamoto kubwa ya maji. Inapofika mwezi Septemba lile Bwawa la Likopo hukauka kabisa na *water table* hushuka kiasi kwamba visima vya wananchi walio wengi huwa vimekauka na hivyo mama hutumia hadi masaa sita kupata ndoo moja ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na mradi wa maji ambao Serikali ilisaini bwawa liweze kujengwa, ulisainiwa Novemba, 2024, ikafika Novemba, 2025 ambapo ndiyo mradi ulitakiwa ukamilike, hilo bwawa likawa bado halijapatiwa fedha. Tukafanya *renew* ya mkataba kwamba sasa ianzie Novemba, 2025 mpaka Juni, 2026, hadi leo ninaongea hakuna shilingi iliyopelekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri alione hili, kwani Wilaya ya Nkasi na hususan Mji wa Namanyere una shida kubwa sana ya maji ya kutumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani, Mheshimiwa Aeshi Khalfan Hilaly na Mheshimiwa Mariam Anzuruni Mungula wajiandae.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi, lakini nitakuwa mchoyo wa fadhila na shukrani kama sitamshukuru kwa dhati Mwenyezi Mungu aliyenipa uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, ambaye aliongoza vikao vikubwa na jina langu likawa miongoni mwa wagombea na mwishowe nawashukuru wapigakura wa Jimbo la Tandahimba kwa kunirejesha tena kwa kipindi cha tatu. Mungu awabariki sana Wanatandahimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mambo ya kuzungumza kwenye Bajeti ya Wizara hii ya Waziri Mkuu. Kwenye jambo la barabara, mimi napongeza sana, nafurahi sana kazi inayofanywa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, anafanya kazi kubwa sana. Nilitamani wakati anafanya ziara yake, basi angepata ziara moja ya Mkoa wa Mtwara, hasa kipindi hiki cha masika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunayo barabara ambayo fedha zake zimetoka Benki ya Maendeleo ya Afrika, maana yake ni fedha ambazo hazina mashaka. Tunaye mkandarasi anayetengeneza Barabara ya Mtwara – Mnivata – Tandahimba – Nanyamba – Masasi. Barabara hii kama Mheshimiwa Waziri Mkuu angefika kipindi hiki cha masika, nadhani kuna hatua zingechukuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi huyu amekuwa mtu ambaye haoneshi dhamira njema ya kuwafanya watu wa Tandahimba, Nanyamba, Newala mpaka Masasi kupita kwa kiwango cha lami. Kutoka Mnivata kwenda Tandahimba ni kilometa 46, lakini leo ikinyesha mvua unatembea saa tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana mkandarasi huyu tumeingianaye mkataba, na mwezi wa 10 mwaka huu ilitakiwa akabidhi barabara ile. Kwa hiyo, matamanio yangu kama itampendeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, na kama atapata nafasi, twende Mtwara aone namna anavyoweza kusaidia watu wa Mtwara, ili barabara hii iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunao Mradi wa Maji wa Makonde ambao mpaka sasa umekamilika kwa 32%. Ninayo mashaka makubwa ya mradi huu kutokamilika kwa wakati. Sasa kwa sababu tuko kwenye bajeti, na hili siyo jambo dogo, Mradi wa Maji wa Makonde unakwenda kuwasaidia wananchi zaidi ya milioni moja wa Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mradi ambao, kama mtaweka macho, tunakwenda kuzungumza tatizo la maji likiwa limepungua kwa kiasi kikubwa sana. Sasa kama utapata fursa ya kuja kwenye mradi wa barabara, nadhani miongoni kwa kero kubwa tutakazosikia Mkoa wa Mtwara ni ujenzi wa barabara na Mradi wa Maji wa Makonde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kwenye hoja ya fedha ya Mfuko wa Vijana, ile shilingi bilioni 200 ambayo Mheshimiwa Rais ameitoa kwa dhamira njema. Ile fedha imeenda Wizara tofauti tofauti, dhamira ni njema, lakini kwa sababu tunayo Wizara yenye dhamana ya vijana, na ina *full instruments,* nadhani ni busara fedha ile ingesimamiwa na Wizara ya Vijana yenyewe kwa sababu, fedha yenyewe inaeleweka, ni shilingi bilioni 200, na tunazo wilaya hapa zaidi ya mia moja themanini na kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingekuwa jambo la busara Serikali ikasema tu, kwenye hizi fedha za vijana, basi kila wilaya itenge shilingi bilioni moja na fedha kidogo, ili kila wilaya iguswe. *Otherwise,* kuna watu watalalamika fedha iliyoenda kwenye

mifugo inaweza ikawa nyingi wakati tuna Sera ya Viwanda ambayo kila wilaya watajenga viwanda. Kama fedha hii ingeenda kwenye Wizara ya Vijana tafsiri yake ingewagusa vijana moja kwa moja maeneo walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingekuwa jambo jepesi sana, tunao Wakuu wa Wilaya wazuri, tunao Wakurugenzi wazuri na tunao maafisa vijana kila wilaya. Ushauri wangu ni kwa sababu, michakato bado inaendelea, Serikali ione kama kuna uwezekano fedha hii irejeshwe kwenye Wizara ya Vijana, ili Waziri mwenye dhamana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Vijana wawe na nguvu ya kuisimamia fedha hii kuhakikisha kwamba, imewafikia vijana wenyewe kwa uzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenzangu amezungumza hapa, TAMISEMI ni katika Wizara ambazo zinagusa uti wa mgongo wa Taifa letu. Mimi ukiniuliza bajeti tuliyonayo, natamani kabisa tuongeze fedha kwenye Wizara hii ya TAMISEMI, ili itusaidie sisi wakulima wa korosho, wakulima wa miwa, wakulima wa mbaazi, na wakulima wa choroko. Taifa hili 76% ni wakulima. Barabara zetu vijijini ni mbovu kuliko unavyofikiria. Leo ukienda, mvua zinavyonyesha kwenye Taifa hili hali ya barabara za vijijini ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Waheshimiwa Wabunge watakubaliana nami, tuongeze fedha kwenye Wizara ya TAMISEMI, hususan kwenye *TARURA* kwa sababu, ndiyo wanalisha Watanzania tulionao. Leo ukienda kwenye Jimbo langu la Tandahimba, barabara zake haziko sawasawa kabisa, na tunazo barabara ambazo ndiyo zinatoa korosho vijijini kupeleka mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama zinapanda, barabara ni mbovu, wenye magari wanataka gharama kubwa kwa sababu, wanatengeneza vipuli kila uchao. Kama Wabunge wenzangu wataridhia, tuone namna ya kuongeza bajeti kwenye Wizara hii ya TAMISEMI, ili wapeleke fedha za *TARURA* tukatengeneze barabara zetu vijijini kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukibaki hapo TAMISEMI, wenzangu wamezungumza vizuri suala la Waheshimiwa Madiwani. Fedha

wanayopewa Waheshimiwa Madiwani, haikidhi mahitaji ya Tanzania ya leo. Kumpa posho Mheshimiwa Diwani ya shilingi 350,000/= siyo sawasawa. Kwa kuwa Wizara hii iko chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, aone namna ya kuongeza posho ya Waheshimiwa Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama itawapendeza Serikali, Waheshimiwa Madiwani wanafanya kazi kubwa. Sisi tukiwa Bungeni hapa wapate vipando, japo pikipiki. Kila Mheshimiwa Diwani apate pikipiki ya kufanyia kazi kwenye eneo lake, na jambo hili linawezekana. Mheshimiwa Waziri Mkuu akisema, zipo halmashauri ambazo zina fedha, ni kutoa maelekezo tu, Wakurugenzi wanunue pikipiki, Waheshimiwa Madiwani wapewe vitendeakazi, wakimaliza muda wao wataweza kuziacha au zinaweza kutumika kwa namna nyingine kwa sababu, zitakuwa ni vipando vya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wanafanya kazi kubwa. Kuna kata kama yangu, Kata ya Ngunja yenye vijiji saba, ukienda kuangalia utoke Mangombya uende Ngunja, utoke Ngunja uende Namindondi Chini au Namindondi Juu, ni zaidi ya kilometa 10 au 12. Mheshimiwa Diwani hana pikipiki, anatembeaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali kuona namna wanavyoweza kuwasaidia wenzetu, Waheshimiwa Madiwani, ambao wakati wote ndio wapo na wananchi na wanasimama badala yetu kuisemea Serikali, ndio wanaosimama kutafuta kura za Rais, na ndio wanaosimama kutafuta kura za Waheshimiwa Wabunge. Hawa waweze kuongezewa posho na wenyewe wajione kwamba wapo kwenye *base* moja ya kusimamia maendeleo ya wananchi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Wenyeviti wa Serikali za Vijiji. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuchukua mihuri. Ile migogoro ilikuwa mingi, lakini na wenyewe kama Serikali itaona inafaa na wenyewe wanapaswa kupewa posho. Serikali ione ni namna gani Wenyeviti wa Serikali ya Vijiji kwa sababu, wakati wote wanafanya kazi kubwa, inawezekana kuliko hata watumishi wa Serikali. Wao ndio wako na wananchi wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati Afisa Mtendaji amepata dharura, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji ndio anasimama pale kutatua matatizo, lakini migogoro yote ya jamii tuliyoizungumza usiku na mchana wenzetu Wenyeviti ndiyo wanafanya kazi kubwa. Serikali ione namna ya kuwapa posho hawa Waheshimiwa Wenyeviti wa Serikali ya Vijiji na wenyewe wafanye kazi zao kwa weledi mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Aeshi Khalfan Hilaly, ajiandae Mheshimiwa Mariam Anzuruni Mungula, ajiandae Mheshimiwa Kija Limbu Ntemi.

**MHE. AESHI K. HILALY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Awali ya yote, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninampongeza Mheshimiwa Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri na kubwa wanayoifanya. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina masuala matatu au manne hivi. Kama muda utanijalia kufanikisha kumaliza, la kwanza ninaishukuru Serikali kwa kukamilisha Uwanja wa Ndege ndani ya Jimbo la Sumbawanga Mjini na Mkoa wetu wa Rukwa. Uwanja ule umekamilika na muda wowote sasa ndege zitaanza kutua na hatimaye Rukwa yetu itakuwa imefunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wameongea humu ndani kuhusu barabara. Kila Mheshimiwa Mbunge aliyesimama hapa ameongelea barabara, siyo barabara za *TARURA* wala za *TANROADS*. Hii mifuko miwili tulitenga *plan* humu ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na *Road Fund* ambayo ni mfuko wa barabara, tumetenga fedha ziwe zinakwenda kule. Fedha zile zinapatikana na tozo za mafuta ili ziweze kila mwaka kuweza kuboresha barabara zetu ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka ninaposimama hapa, 80% ya barabara tulizozitangaza na tukapata wakandarasi mpaka leo zimesimama. Kuanzia Rukwa, Mpanda na maeneo yote yale ndani ya Tanzania hii 80% ya barabara zimesimama. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kila mkandarasi aliyeshinda tenda alipewa *site*, akapewa *advance payment*. Baada ya hapo, hakuna mkandarasi hata mmoja aliyepokea fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini hasara zake? Mkandarasi anapokuwa ameshinda na amekwenda *site*, amepewa *advance payment* na hatuna fedha za kumlipa, yule mkandarasi ataendelea kutu-*charge* siku hadi siku mpaka pale atakapokuwa amemaliza kujenga barabara. Sasa natoa mfano, mkandarasi ameshinda labda tenda moja au Barabara ya kutoka Muzi – Ntendo kwa shilingi bilioni 52, lakini mpaka leo hii Barabara ya Ntendo – Muzi ina miaka minne haijawekwa hata kilometa moja ya lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo mpaka barabara ikamilike ndani ya miaka mitano mingine ijayo au miaka minne tutakuwa tumelipia barabara ile kwa shilingi bilioni 100, zaidi mpaka shilingi bilioni 110. Sasa tuna barabara ngapi kiasi hicho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuishauri Serikali, bajeti hii ya mwaka huu tusiwe na mradi wowote mpya, twende tukakamilishe miradi ya zamani kwa wananchi wetu hawa kwa sababu, tumewaahidi kujenga barabara, angalau hata tungejenga kilometa kumi kumi, wangeona kuliko sasa hivi, mkandarasi yuko *site,* na hakuna hata kilometa moja ya lami iliyoweza kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapata hasara kubwa, lakini hili nataka kumshauri Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu, najua ni mzalendo, tunapoteza fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, *TARURA*. Wote humu ndani wanaipongeza *TARURA*, nami ninaipongeza *TARURA,* lakini fedha hawana. Barabara za mwaka 2025, tenda za mwaka 2025, tumeziahirisha. Nataka tena kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali inapokuja, basi tukubaliane zile barabara ambazo

tulizipitisha mwaka 2025 twendenazo mwaka huu ziweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza ni mwaka 2025 huo huo tumetenga fedha tukasema sasa tuongeze kodi kwenye mafuta, zile fedha zikipatikana ziende *TARURA*. Tukajenga kuna kitu kinaitwa *ringfence*, mimi hiyo ninaamini, sasa hivi siyo *ringfence,* ni *open fence*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ambazo tunazitenga ziende kwa ajili ya barabara, haziendi, sasa tunakaa humu Bungeni tunatafuta *source* ya fedha, tunakubaliana kwamba, fedha hizi sasa ziende *TARURA* ili kujenga barabara zetu. Fedha zile haziendi, zinakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo yanasikitisha sana. Bajeti ya mwaka 2025, nikiwemo humu ndani, tumepitisha kwamba, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Rukwa itajengwa, tumepitisha shilingi *2.5 billion* hapa, mpaka ninaposimama hapa leo hata senti tano moja haijaenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Waheshimiwa Wabunge wanielewe kidogo. Kuna habari Wizara ya Afya inataka kukopa fedha, shilingi *1.4 trillion,* kwa ajili ya ukarabati Muhimbili. Nawaambia Waheshimiwa Wabunge, hili jambo tusilikubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama lipo kwenye Wizara ya Afya huko, limeshakuja kwenye Kamati, kuna *lobbying* zinafanyika. Naomba Bunge hili nendeni mkafanye *research*, tusikubali kwenda kujenga Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili kwa shilingi bilioni 1,400, haiwezekani. Nami niko hapa...

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa. Mheshimiwa Dkt. Samizi.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa mchango wake mzuri sana. Naomba kumpa taarifa tu, ili kwa uelewa wa jambo linaloendelea, kwa ajili ya Muhimbili siyo ukarabati, ni ujenzi wa Muhimbili mpya. Ni kweli kabisa ujenzi huo utatumia shilingi trilioni 1.2 na ni mkopo, lakini lengo ni kutaka Muhimbili iwe Hospitali bora kwa sababu, imeshindwa kupata ithibati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majengo ya Muhimbili ukiyaona yamesambaa sana, yametumia eneo kubwa. Mpango huo ni mahsusi kwa ajili ya kujenga Muhimbili mpya, Muhimbili ambayo itakuwa na uwezo wa kulaza wagonjwa 1,300. Ni ujenzi wa hospitali pamoja na usimikaji wa mitambo yote ya Muhimbili; na itajengwa kwa awamu ya miaka saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kuweka vizuri tu, siyo ukarabati wa Muhimbili, lakini ni ujenzi wa Muhimbili mpya. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aeshi unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. AESHI K. HILALY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Waheshimiwa Wabunge sidhani kama wataipokea, hainiingii akilini. Tuiache, tuna mzigo mkubwa bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miradi mingi imesimama, tuna mikopo mingi, tunalipa madeni mengi, kwa nini tukaongeze mzigo zaidi na Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili bado ipo? Twendeni jamani na kimoja kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende tukamalize *SGR* yetu, twende tukamalize barabara zetu, twende tukakarabati meli zetu. Kule Kigoma, leo ni bajeti ya mwaka wa tano tunasema tunajenga meli, meli haijajengwa mpaka leo. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, inawezekana ni mkopo, lakini nendeni kwenye mikoa mingine, hospitali za rufaa za mikoa hazijajengwa. Kwa nini twende tukabomoe kitu ambacho sasa hivi kinafanya kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, una gari bado zima, acha kwanza liendelee, endelea kufufua mengine. Hizi hela ni nyingi, tunaenda kukopa na tutalipa na mwisho wa siku tutaendelea kuwa na madeni. Ninaishauri Serikali kwa nia njema, tuachane na hili jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama fedha hizo tumeenda kuzikopa tayari, basi ziende zikajenge hospitali za rufaa kila mkoa, ili kupunguza mzigo wa wagonjwa kwenda Muhimbili, yako maboma kule. Mimi nataka kushauri sana, ninaamini Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mzalendo, liangalieni jambo hilo. Najua litakuja Bungeni, tutapigwa siasa, tutaweza kulipitisha. Ninaomba sana liangalieni mara mbili mara tatu. Yaani kwa sasa hatuna uwezo huo wa kujenga Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili kwa bilioni zote hizo. Twendeni kidogo kidogo tutafika, lakini tukienda haraka hatutaweza kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ndani ya Bunge, na ninaamini katika hili ipo siku mtanikumbuka, nilisimama hapa nikashauri hili. Tusiweke mzigo mzito kwa wananchi tukashindwa kuendelea. Mheshimiwa Waziri Mkuu, twende tukasimamie na kukarabati miradi mingine ambayo haijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Mradi wa Meli, *Lake Tanganyika.* Nimesimama hapa mwaka wa saba, hapa Liemba imekufa, Mwongozo imekufa, tukaambiwa inajengwa meli mpya hapo, hiyo meli ni hadithi, mpaka leo hatuna meli hata moja. Matokeo yake Waheshimiwa Mawaziri wa Uchukuzi wanatuchukua sisi Wabunge kwenda kushangaa meli za Mchina ambazo ziko kule *Lake Tanganyika!* Siyo meli zetu zile. Meli zetu lini zitajengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaambia Waheshimiwa Wabunge wa kutoka Mkoa wa Rukwa, Kigoma na Katavi, wananchi wanakufa sana, wanazama sana na hawana usafiri. Tukasema, basi twendeni tukakarabati angalau meli moja, wakanijibu hapa tukarabati *Mv. Sangara; Mv. Sangara* inabeba mafuta, haibebi watu. Kwa hiyo, kule usafiri wa *Lake Tanganyika* wanasafiria maboti ya mbao, kila siku wanazama, wanapotea.

Nakuomba sana, Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi anapokuja hapa na bajeti yake, aje kutuhakikishia lini meli inajengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia. Kuna karakana ya meli kule Kigoma, wameingia mkataba na mkandarasi miaka minne iliyopita, wamempa asilimia tano sijui, asilimia kumi ya ule mradi, kama *advance payment*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wako umeisha.

**MHE. AESHI K. HILALY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka leo hawajatoa zile fedha, mradi umesimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani kidogo namalizia. Kwa uelewa kidogo wa Waheshimiwa Wabunge...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha.

**MHE. AESHI K. HILALY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *advance payment* inayotolewa kwenye miradi ni hela za watu. Ikishatolewa *advance payment* mradi hauendelei, umekufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, lakini nitakuja tena baadaye. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kweli, akipata nafasi tuongee, tujadili kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Mariam Mungula, ajiandae Mheshimiwa Kija Limbu Ntemi.

**MHE. MARIAM A. MUNGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi hii adhimu kuchangia katika hotuba ya Waziri Mkuu. Kwa kuwa leo ndiyo nimesimama kuchangia kwa mara ya kwanza, ninaomba kuanza kwa shukrani nyingi sana kwa Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa uzima na uhai wa kunifikisha siku ya leo nikiwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia kumshukuru kwa dhati Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi na vikao vyake vyote anavyoviongoza vya Chama cha Mapinduzi kwa kuniteua na hatimaye nikachaguliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na shukrani hizo ninaomba kumpongeza sana Rais na Amiri Jeshi Mkuu kwa kazi kubwa anayoendelea nayo ya kuendeleza taifa letu. Hata leo tumeona amezindua minara zaidi ya 750 ambayo itachangia kwa kiasi kikubwa sana kutuletea maendeleo ya mawasiliano katika wilaya zetu na nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi nyingine za mwisho, lakini siyo kwa umuhimu na shukrani ninaomba ziwaendee Wabunge wenzangu wote humu ndani, kwanza shukrani kwa kunichagua kuwa mmoja wa wawakilishi wa nchi yetu katika Bunge la Afrika, vilevile niwapongeze na ninyi kwa kuteuliwa kuingia humu ndani ninafahamu haikuwa kazi rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwenda moja kwa moja kwenye mchango wangu kwa hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza nimpongeze Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri, bora kabisa inayoenda sambamba na dira yetu ya maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia kwa upande wa ardhi na makazi. Waziri Mkuu kwenye hotuba yake amesema kwamba Serikali itaendelea kutekeleza au kujenga nyumba za bei nafuu, tunapongeza sana. Kwanza ninaomba kuipongeza sana Serikali kwa ujenzi wa nyumba hizi za bei nafuu ambao unaendelea nchi nzima katika halmashauri tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza vilevile Serikali kwa jitihada zake za kutaka kuendelea kuwapa Watanzania makazi bora. Niliona kwenye Dira ya Maendeleo ya Taifa, ulisema tuna upungufu wa nyumba takribani milioni 3.8 mpaka tutakapofikia mwaka 2050. Huu ni upungufu mkubwa sana na Dira ya Maendeleo ya Taifa iliainisha suluhisho mbalimbali za kukabiliana

na changamoto hii ya upungufu au uhaba wa nyumba za bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kihistoria suala la ujenzi wa nyumba za bei nafuu nchini kwetu lilikuwa linasimamiwa na Shirika la Nyumba la Taifa *(National Housing),* ambalo tangu tulipopata uhuru muasisi wetu au waasisi wetu Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere na Mzee Abeid Amani Karume walianzisha *initiatives* tofauti za kuhakikisha kwamba Watanzania wazawa wanapata makazi bora. Baba wa Taifa alipoanzisha ninadhani Shirika la Nyumba la Taifa lilikuwa ni moja ya mashirika yaliyoanzishwa mapema sana, vilevile kule Zanzibar Mheshimiwa Karume nae alijenga nyumba za makazi nyumba za bei nafuu pale Michenzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na utaratibu huo wa kuwa na nyumba za bei nafuu kupitia *National Housing,* kwa bahati nzuri kutokana na maendeleo Shirika la Nyumba la Taifa mwaka 2005 lilibadilika kutoka kuwa Shirika la kutoa huduma kwa jamii kwa maana ya hizo nyumba za bei nafuu, likaenda kuwa Shirika la kibiashara linalojiendesha kibiashara zaidi na liliwekewa sheria yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pale ndiyo tukapata *vacuum* kwamba tumekuwa na pengo. Sasa hivi nchini kwetu tunavyoongea hakuna utaratibu maalum wa kuweka hizi nyumba za bei nafuu zaidi ya Serikali, ndiyo inafanya na hakuna utaratibu kwa maana ya kwamba hatuna sheria inayosimamia hili eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kushauri kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu waangalie uwezekano wa sisi kuanzisha Sera ya Nyumba. Tunayo Sera ya Ardhi, mpaka sasa hivi Tanzania tunayo Sera ya Ardhi, tunayo Sheria ya Ardhi, tunayo sheria mbalimbali ambazo zinafanya kazi katika eneo hili, lakini hatuna Sera Maalum ya Nyumba, wala hatuna sheria maalum inayosimamia makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivi kwa sababu gani umuhimu wa kuwa na hii sera, tunakoelekea kwenye ujenzi au upungufu wa kuwa na nyumba milioni 3.8 bila ya kuwa na sera ya usimamizi, Serikali bila ya kuwa na sera muhimu au maalum

ambayo itaweza kusimamia hii sekta tutashindwa, kwa sababu nyumba nyingi za bei nafuu au zinazojengwa, zinajengwa kwa kutumia *private sector* na *private sector* mara nyingi wako kwa ajili ya faida. Sasa hili ongezeko linaweza likazidi ikawa imetuwia ugumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ninaomba Serikali iangalie uwezekano, Bunge hili kwa sababu sisi ndiyo tuliopitisha Dira ya Taifa ya Maendeleo ili dira yetu iweze kufanya kazi kiufasaha lazima tuitambulishie vitendea kazi, kwa hiyo kuwa na Sera ya Ardhi ni moja ya njia ambazo zitafanya Dira yetu ya Maendeleo ya Taifa ifanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo suala la nyumba na Sera ya Ardhi nilikuwa ninaomba kuangalia vilevile, leo asubuhi alikuwa anachangia Mbunge nimemsahau amenitoka, aliongelea kuhusu nyumba za watumishi, upungufu wa nyumba za watumishi na Naibu Waziri wa Afya alitoa takwimu kwamba tuna upungufu wa nyumba za watumishi wa afya takribani 25,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaomba kuelekeza kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, sasa imefikia muda tuweze kutenga maeneo maalum kwa ajili ya kujenga nyumba za watumishi. Kwa sababu tunapoelekea *population* yetu kama nchi inakua na hawa watumishi hususan watumishi wa afya na watumishi wa elimu ni jadi ya kazi yao wanahamahama sana, anaweza akatoka Dodoma akaenda kufanya kazi Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akifika kule anakuta hana makazi maalum ya kukaa, inamfanya kazi yake inakuwa ngumu sana. Hivyo, tutakapoweza kutenga maeneo rasmi au tuseme *land bulks* sasa hivi ambazo zitatumika kujenga nyumba za watumishi, hiyo itatusaidia sana hata kwa baadaye kuhakikisha kwamba watumishi wetu wanapata makazi bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wa 16 wa Marekani, Abraham Lincoln kuna usemi mmoja maarufu unahusishwa nae unasema kwamba: '*If I had six hours to chop down a tree, I would spend the first four hours sharpening the axe*'. Kwamba ukinipa masaa sita ya kukata mti nitatumia manne ya kwanza kunoa lile shoka.

Sasa hivi tuko katika kuelekea au tunaanza kutekeleza Dira yetu mpya ya Maendeleo ya Taifa, kwa hiyo ni muhimu sana tuipe hii dira uwezo wa kufanya kazi na kutekelezeka kiurahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa na sheria au sera ya nyumba…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge muda wako umekwisha.

**MHE. MARIAM A. MUNGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru na ninaomba kumalizia kwamba, kuwa na sheria au sera ya nyumba itakuwa ni kiungo muhimu sana katika kutekeleza na kuifanya dira yetu ifanikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Kija Limbu Ntemi, wajiandae Mheshimiwa Nyamizi Simon Mhoja na Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa.

**MHE. ENG. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Nami nipate fursa ya kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuongoza mpaka kufika wakati huu tukiwa salama salimini kama Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru na kumpongeza pia Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyenipendekeza mimi kuwa Mbunge wa Jimbo la Katoro, siyo mimi tu na vijana wote waliopendekezwa na Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kuingia Bungeni mara ya kwanza, wengine wakachaguliwa kuwa Mawaziri, Naibu Mawaziri kwa mara ya kwanza katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza vilevile Makamu wa Ras, Dkt. Emmanuel Nchimbi aliyesimama, kumtetea na kumwombea kura Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan naye pia kuwa

Makamu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia nimshukuru na kumpongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kaka yetu, Ndugu yetu Dkt. Mwigulu Nchemba anayefanya kazi katika sehemu nyingi, amezunguka nasi tumemwona, mambo mengi ameyatatua papo kwa papo ili kuonyesha kwamba Serikali iko pamoja na wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dkt. Mwigulu alisema anakuja Katoro na nikapata taarifa kwamba atafika Katoro, tulijiandaa sana watu wa Katoro kumpokea ili azungumze nasi, atutie moyo, awatie moyo watu wa Samia ila sasa kwa sababu ya ratiba akashindwa kufika. Tunamwomba baada ya Bunge hili Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania afike Katoro ili watu wa Katoro aone wanavyokuzungumza na wanavyomzungumza Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwampongeza pia Spika wa Bunge, Naibu Spika na viongozi wote walioteuliwa na Rais wakiwemo Mawaziri na Naibu Mawaziri wanaofanya kazi vizuri, akiwemo mtu ambaye tumepewa Jimbo kwa pamoja, tukagawiwa tukapewa, kaka yangu Dkt. Jafar, Naibu Waziri TAMISEMI, huyo ni pacha wangu kabisa ambaye tuko naye sehemu moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungmze kidogo kwa kuwashukuru Chama changu cha CCM, kuanzia Mjumbe aliyenipigia kura mpaka Kamati Kuu walionipendekeza walioko Jimbo la Katoro, walionichagua mimi kuwa Mbunge wa Jimbo la Katoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru nami mke wangu aliyeniombea sana kila siku wakati tunaomba kura, kila siku asubuhi tuliomba tunakwenda kwenye kampeni tukimwombea Rais tunapiga magoti, tukiombea na wagombea wote hata wale ambao tulikuwa tunaomba nao kura, tulikuwa tunawaombea pia afya njema ili tuendelee kufanya kazi kwa pamoja kuomba kura kwa wananchi. Kwa hiyo, ninamshukuru sana mke wangu Mariam aliyenipigania sana kusimama hapa kufika sehemu hii pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nizungumze basi machache baada ya shukrani hizo, lakini kama kuna shukrani ambazo nimezisahau ninaomba Mungu atawakumbusha kwa mioyo yao kwamba nimewashukuru pia na wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan juzi niliomba gari la zimamoto hapa, Waziri wa Mambo ya Ndani alitamka gari litakuja na Dkt. Samia Suluhu Hassan akanipatia gari la zimamoto leo lipo Katoro, leo hii nikimshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan, leo tena nimeambiwa kiwanja cha kujenga ofisi za zimamoto ndani ya wiki hii kitapatikana usipomshukuru mtu unafanyaje? Ninamshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa haya mambo anayoendelea kutufanyia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kampeni za Dkt. Samia Suluhu Hassan alisimama Katoro tukamshuhudia tukamwona, wakati anasimama Katoro, barabara za Katoro zilikuwa zinajengwa mitaro na sasa barabara nyingi zinapitika alipoapishwa na barabara zimeanza kupitika, mitaro imejengwa, tunawaomba *TARURA* watuongezee mitaro ili Rais hata kama siku moja akija Katoro aweze kupita barabara yoyote anayopenda yeye mwenyewe, kwa sababu zitakuwa zimekuwa salama zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo barabara moja inaitwa Luhuha ambayo iko chini ya *TARURA* inayopitisha mazao kutoka katika Kata Sita kuleta Mji wa Katoro, ambazo hizo Kata ni pamoja na Kata ya Butundwe, Kata ya Nyakagomba, Kata ya Chigunga, Kata ya Bukondo, Nyamwilolelwa na Nachiluluma ambazo zilikuwa zinasumbua sana, lakini kwa sababu tunao viongozi wazuri wa *TARURA* na Meneja wetu wa Wilaya ya *TARURA* tulizungumza naye amerekebisha zile barabara zinapitika vizuri mpaka sasa tunawapongeza sana *TARURA*, mnafanya kazi vizuri endeleeni kusimamia kila sehemu ili barabara hizi ziweze kupitika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba TAMISEMI kuna Kata mbili ambazo zinazo changamoto za vituo vya afya, Kata ya Magenge na Kata ya Kaseme, ikiwezekana katika bajeti hii basi wale watu waweze kupatiwa kituo cha afya ili waweze

kujiendesha wenyewe, ili waweze kupata huduma ya afya katika mazingira yao na siyo kutoka kule kuja Katoro kwa ajili ya kupata huduma ya hospitali. Ninaamini ninyi ni wasikivu ninaamini tunayo Serikali sikivu itatufanyia haya mambo na baada ya bajeti zao wafike kwenye maeneo yetu ili waweze kufanya kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina Kata tatu au Kata mbili, Kata ya Ludete na Kata ya Katoro yenyewe ambazo ziko mjini zinazohitaji kuunganishiwa sana maji. Rais ameyatoa maji mbali kabisa ambako hata wengine hawapajui panaitwa Chankolongo. Chankolongo ni mbali ametoa maji kwa gharama ya bilioni sita ameyaleta katika Mji wa Katoro, kilichobaki ni usambazaji wa maji na naamini kwa sababu Waziri wa Maji yupo na Naibu wake na tumezungumza nao mara nyingi sana, wamesema wataanza kuyasambaza maji yale yaliyoletwa na Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ili watu wa Katoro waendelee kupata maji safi na salama katika Mji wa Katoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, Mbunge wa Jimbo la Katoro ninaunga mkono hoja bajeti ya Waziri Mkuu, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kija kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Nyamizi Simon Mhoja, wajiandae Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa pamoja na Mheshimiwa Pascal Lucas Lutandula.

**MHE. NYAMIZI S. MHOJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Awali ya yote ninapenda nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kutufikisha kuwa wazima mpaka dakika hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia shukrani za pekee zimwendee Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutujumuisha katika kila sekta watu wenye ulemavu Nchini Tanzania. Pia shukrani zingine zimwendee Waziri Mkuu ambaye kwa sisi wenye ulemavu kuwa chini yake na kuendelea kuratibu mambo yetu ya wenye ulemavu. Kwa kuthibitisha hili hata kwenye hotuba yake amezungumza kuwa yeye ni mdau mkubwa wa watu wenye ulemavu, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja kwa kuokoa muda mchango wangu utajikita katika ukurasa wa 71 na 72 ambao ni uratibu wa masuala ya watu wenye ulemavu. Hotuba ya Waziri Mkuu ilieleza kwamba Serikali imewezesha bohari ya dawa kuzalisha na kusambaza vifaa saidizi na mafuta kinga kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa saidizi kwa watu wenye ulemavu ninaweza nikatolea mfano, ni sawasawa na samaki na maji huwezi kuvitenganisha. Ukimweka samaki nchi kavu atatapatapa mwisho wa siku mambo yataharibika, hivyo hivyo hata sisi watu wenye ulemavu. Nimefika hapa kwa sababu tu nina vifaa saidizi vimeniwezesha kuingia humu na kutekeleza majukumu yangu ya kiubunge kama Wabunge wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali kuwa vifaa hivi vimekuwa ni gharama na wote tunafahamu watu wenye ulemavu hali zetu wanazifahamu, ni duni. Nitolee mfano, mguu bandia kwa aliyekatikia juu ya goti miwili nitolee mfano moja kwa moja kwenye hospitali yetu ya Muhimbili pale Moi, wanauza unapata *invoice* ya milioni saba miguu miwili. Sasa niambie mtu mwenye ulemavu wa kawaida hiyo gharama anaipata wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, vifaa saidizi tukimaanisha hata magongo na *crutches* kama hizi ninazotembelea mimi nazo ni gharama kwa mtu mwenye ulemavu. Ninamzungumzia mwenye ulemavu wa hali ya kawaida kule kijijini, kwenye kata na kwenye Wilaya kule ambapo anapatikana, hizi gharama anazipata wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri Waziri Mkuu, Serikali imewezesha *KCMC* kuzalisha mafuta kinga kwa watu wenye *Ualbino,* wako wadau mbalimbali ambao wanazalisha vifaa saidizi maana vimekuwa adimu ndiyo maana hata gharama zinakuwa kubwa, wawezeshe hizi hospitali kila Mkoa pawepo basi hata hospitali ambayo inatoa vifaa saidizi na ili kurahisisha maisha kwa watu wenye ulemavu, vinginevyo hali zetu zinakuwa ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ninazungumzia suala la mikopo ya 10%, kwa wenye ulemavu tunapata asilimia mbili. Imezungumzwa sana na wenzangu wazungumzaji waliotangulia. Sisi watu wenye ulemavu nchini Tanzania; kuna aina 13 za watu wenye ulemavu. Kuna aina moja ya ulemavu ambayo ni ya ulemavu wa akili, hawana sifa ya kupata huu mkopo, lakini ikumbukwe kwamba kuwa na ulemavu maisha yanaendelea kama kawaida. Atahitaji kula, atafanya biashara; na tukumbuke kwamba kuna dawa ambazo wanatumia, akitumia anakuwa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali imewatoa kabisa kwamba hawa watu hawapati hii mikopo. Ikumbukwe kwamba sisi wenye ulemavu hatuishi peke yetu, tunaishi na ndugu zetu, *either* ni mama, ni baba, ni mume, mke, tunaishi nao. Serikali inaweza ikaja na mpango mwingine wa kuwafikiria hawa walemavu wa akili ili nao waingie kwenye kuwapatia mikopo hii ya asilimia mbili ili nao waweze kufaidika na keki hii ya Taifa, ambayo wenye ulemavu wengine wanaipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikishindikana hilo, ushauri mwingine basi wafikiriwe wapewe ruzuku, ilimradi tu kurahisisha maisha yao, waendelee kuishi kama watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba pia ya Mheshimiwa Waziri amezungumza kabisa kwamba Serikali imewezesha kituo atamizi kilichopo Singida pale Sabasaba. Chuo hiki ni miongoni mwa vyuo vingi ambavyo Serikali imeviboresha. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama ataona inafaa aweze kuvitembelea vyuo hivi, vina changamoto, ikiwemo wakalimani wa lugha ya alama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri Chuo cha Luanzali Mkoani Tabora, hakina mkalimani. Hata juzi likizo nimetoka huko nimeona bado mkalimani hayupo. Hawa wanafunzi wanasomaje bila mkalimani? Ninaomba hili lichukuliwe kwa uzito ili kusaidia; na tutashukuru kama watatembelea na kutatua changamoto nyingi ambazo zinahusiana na hivyo vyuo vyuo vya watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja nizungumzie watumishi wenye wa umma ulemavu. Kuna mwongozo upo, mwongozo wa watu wenye ulemavu mahali pa kazi. Mwongozo huu hautambuliki kwa waajiriwa. Ninaomba Serikali, Ofisi ya Utumishi na Utawala Bora waweze kuwatambulisha waajiri wote huu mwongozo ili wafanyakazi wenye ulemavu waweze kupata haki zao kutokana na mwongozo, ambao Serikali ilikaa na kufikiria na kuona kutengeneza huu mwongozo na si kuuweka tu kapuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hiyo, kupitia Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, tunaomba waajiri wasiwanyime wafanyakazi wenye ulemavu fursa za safari za kazi kwa sababu ya mitazamo chanya ambayo wanayo kichwani mwao. Sisi watu wenye ulemavu tunafanya kazi na sisi tunatamani tupate hiyo fursa ya kusafiri ili tuweze kupata hicho kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kuna waraka wa *per diem* kwa mwanamke ambaye ananyonyesha, akisafiri kikazi analipwa nusu *per diem* kwa ajili ya kumsaidia mtoto anayesafiri naye kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, sisi watu wenye ulemavu, mimi mwenyewe siwezi kutembea peke yangu, ninahitaji msaidizi. Wafanyakazi wengi wa watu wenye ulemavu wanapokwenda safari za kikazi wanapewa fedha iliyo sawa na mtu mwingine. Kwa hiyo, yeye atamchukua mtu wa nyumbani amsaidie kwenda naye. Atamkatia ile ile *per diem* ambayo ndiyo anayopata; *of which* inakuwa sasa hela anayoipata ni kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ofisi ifikirie kutengeneza basi na waraka mwingine kwa watu wenye ulemavu, watambulike kuwa na msaidizi mahali pa kazi na hasa wakisafiri kwenye kuelekea kwenye safari za kikazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, Ofisi ya Waziri Mkuu inaandaa maazimisho ya siku ya Kimataifa na pia sisi watu wenye ulemavu tuna siku yetu maarufu kama *D Day (Disability Day)*

ambayo ni tarehe 3 mwezi Desemba. Siku hii imekuwa ikidorora siku hadi siku. Mfano mzuri, mwaka jana tulifanyia Morogoro, ikawa kama ni kikao tu cha walemavu kutoka kata fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Ofisi ya Waziri Mkuu waendelee kuratibu hii Siku ya Watu Wenye Ulemavu Duniani kama siku nyingine za kimataifa za UKIMWI na maadhimisho mengine. Waichukulie kwa uzito na sisi tutafurahi; maana siku hiyo ndiyo siku ambayo wadau wanaweza kutoa mambo yao na pia tunaweza tukawajua wadau wanaojishughulisha na mambo yetu. Sisi wenyewe pia tutajulishana mambo mengi ambayo yanatuhusu sisi watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo ninaunga mkono hoja, ninashukuru kwa kunipa fursa. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge ninaomba tutambue wageni walioko Bungeni jioni ya leo.

Wageni 20 wa Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, ambao ni wananchi kutoka Kata ya Makurumla, Ubungo Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaendelea, Waheshimiwa, nilimtaja Mheshimiwa Zainab Rashid Kawawa.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanya maamuzi ya haraka ya kupunguza matumizi ya mafuta kwa kuanzia na ofisi ya kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ushauri tu kwamba, ni muda muafaka sasa wa kutumia nafasi hii ya changamoto ya

upatikanaji wa mafuta kama fursa kwa kuanza kutumia gesi yetu ambayo inatumika kwenye magari. Wataalam wajielekeze kwenye kupanua mradi wa gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo gesi wananchi wanaitumia kwenye magari Mkoa wa Dar es Salaam. Kwa hiyo, si vibaya kama wataalam watatushauri vyema kuongeza wigo na kuileta katika mikoa mingine ili tuweze kuitumia hii gesi ambayo pia ni ya gharama nafuu sana kama njia mbadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye kwa kweli amelivaa joho lake la Uwaziri Mkuu na ameenea kwenye kiti chake sawasawa. Mheshimiwa Waziri Mkuu amezunguka katika maeneo mbalimbali na katika Mkoa wetu wa Lindi pia amezunguka. Tunaona ambavyo inaleta tija ya uwajibikaji na inaleta funzo la uwajibikaji. Ninataka niwaambie Watanzania, kwamba Taifa hili lina-*operate* katika mfumo wa *decentralization* tangu wakati wa Azimio la Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *decentralization* maana yake ni ugatuaji wa Madaraka; mgawanyo wa majukumu na wa madaraka kuanzia ngazi ya wananchi ambao wanachagua viongozi wao kwenda kwenye ngazi za vitongoji, vijiji, mitaa na mijini. Vilevile kwenda kwenye ngazi za kata ambapo wanawapata Madiwani, kwenda kwenye ngazi za wilaya ambako wanapata Wabunge wa majimbo, kwenda kwenye ngazi za mkoa kwa maana ya upande wa Serikali Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni vizuri kila mmoja akatambua wajibu wake katika eneo lake, kwa sababu dhumuni la kufanya huu ugatuaji wa madaraka lilikuwa ni kumpunguzia Rais mzigo wa uwajibikaji katika kuwahudumia wananchi. Hivyo, ni vyema kila mtu kwenye eneo lake akawa tayari kuwahudumia wananchi. Si vyema kusubiri masuala ambayo yanahitaji kuhudumiwa ngazi ya chini kumsubiri mpaka Mheshimiwa Waziri Mkuu aje kumhudumia mwananchi huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema tujitathmini, ni vyema tutende haki, tuwahudumie wananchi wetu kwa kuwa hiyo ni

dhima ambayo Mwenyezi Mungu ametupa. Kesho atakwenda kutuuliza nilikupa nafasi yako uliitumikiajie kwa waja wangu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuendelea na jitihada za kukuza ajira katika nchi yetu. Mheshimiwa Rais ametuletea mradi mkubwa sana, Mradi wa Bandari ya Uvuvi; bandari ya kisasa, bandari kubwa ambayo haijawahi kutokea katika nchi za Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari hii inatarajiwa kuzalisha ajira zisizopungua 300, ajira rasmi. Bandari hii kama itafanya kazi ipasavyo upo mnyororo wa thamani wa huduma mbalimbi zitakazofanyika pale zinazohusiana na bandari moja kwa moja; ajira zisizopungua 30,000. Thamani ya bandari hii ni shilingi bilioni 280.5; na mpaka sasa utekelezaji wake umekwishafikia 97%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna matumaini makubwa sana na bandari hii, hasa kwenye hili eneo la ajira. Tunaona kuna fursa ya vijana kwenda kufanya shughuli za uvuvi wa samaki, tunaona kuna fursa ya vijana na wanawake, maana wanawake wengi huwa wanafanya biashara za samaki. Kwa hiyo, tunaiona fursa kubwa sana ya ajira katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kwamba, mpaka sasa hali ya umeme katika eneo la bandari bado si ya uhakika. Hali ya umeme kwenye eneo lile ambalo litahitaji kuwa na majokofu ya kuhifadhi tani zisizopungua 60,000 kwa mwaka si ya uhakika. Umeme tunaoambiwa unaohitajika pale si chini ya megawati 300. Mpaka sasa tunaambiwa tunatumia umeme, tunavuta umeme kutoka Songosongo ambao sina uhakika kama unaweza kukidhi haja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali, kwa uzito wa mradi huu na kwa gharama ambazo Serikali imekwishaingiza pale, watuletee umeme wa gridi ya Taifa. Pale sisi Wabunge tunapofanya majukumu yetu tunalala Kilwa, tunalala wapi tunahamahama. Ukikaa Kilwa umeme unakatika kwa siku si chini ya mara 10, ndio ukweli wenyewe ‘Haki ya Mungu’. Siyo chini ya

mara 10. Sasa, tunawezaje kuleta mradi mkubwa kama huu halafu hatuna umeme wa uhakika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, samaki wanahitaji kuhifadhiwa ili wasiharibike, ni *perishable*; sasa watahifadhiwaje kama hakuna umeme wa uhakika? Kwa hiyo, ninaomba, ili tuweze kuleta matumaini makubwa kwa Taifa letu na kwa vijana wetu na kwa wananchi wetu wanaoitegemea bandari hii, hasa kwenye ajira, basi tunaomba tutekelezewe jambo hili kwa haraka. Kwa sababu, kama tumeshafikia 97% tumebakiza muda mchache wa kumalizia na kuanza, ni vyema basi likatekelezeka hili jambo kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya barabara pia inahitajika. Kutoka Kilwa Masoko hadi kwenda Nangurukuru na kuelekea sehemu nyingine barabara ile ni mbovu. Kwa hiyo, ni vizuri ikatengenezwa ili kusudi usafirishaji wa samaki na vyombo vya moto vitakavyokuwa vinapita pale viweze upita kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze tena Mheshimiwa Rais kwa kukuza ajira kwenye sekta ya kilimo. Katika Mkoa wetu wa Lindi tumeona jitihada kubwa zimefanyika za kuchochea ajira kwenye eneo hili la kilimo, kwa sababu kitendo cha Mheshimiwa Rais kuendelea kutuletea pembejeo za ruzuku kumechochea vijana wengi kuingia kwenye kilimo na uzalishaji umeongezeka, hasa kwenye mazao ya kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazao ya ufuta tumezalisha kilogramu milioni sabini na tano laki saba na sitini, ukilinganisha na mwaka uliopita ambapo tulizalisha kilogramu milioni sitini na nane laki mbili na hamsini na nne. Kwenye zao la korosho tumezalisha kilo milioni mia moja arobaini na tatu laki nne na sitini ukilinganisha na kilo milioni 115, kwa msimu uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata zaidi ya shilingi bilioni 360 kwenye korosho na takribani shilingi bilioni 200 kwenye zao la ufuta. Hii ina-*reflect* namna ambavyo vijana wetu wanahamasika katika ajira na kujiajiri wenyewe kwenye eneo hili la kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ombi langu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umekwisha?

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia. Tunaomba tusaidiwe kuondolewa migogoro ya wafugaji kwa sababu kuna wafugaji wengi sana wanahamia kwenye Mikoa yetu ya Lindi, mkoa ambao ni wa wakulima. Tunashindwa kufanya kilimo kizuri kutokana na mashambulizi makubwa ya mifugo.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Nilimtaja Mheshimiwa Pascal Lucas Lutandula, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava.

**MHE. PASCAL L. LUTANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami niungane na wachangiaji wengine; niaanze na kumshukuru sana Mungu mwingi wa rehema aliyenijaalia mimi mtoto wa mama ntilie niseme nanyi Watanzania jioni ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema Fungu Takatifu la Biblia; Wagalatia 4:16, Mtume Paulo anasema: "Nimekuwa adui yenu kwa sababu ya kuwaambia ukweli?" Hili ninaanza na swali. Kwa nini nimeanza na swali? Ninataka niseme, hakuna nchi nzuri kama Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakubaliana na mimi; hakuna nchi ambayo ni nzuri inawaandaa viongozi katika Taifa hili kuwa viongozi wa kuwatumikia watu, ni Tanzania peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na Mheshimiwa Rais, Mama huyu Dkt. Samia nianze kwa kumshukuru sana. Ninataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, watakubaliana nami, kwenye tikisiko hili la mafuta; mimi ni mfanyabiashara, mimi ni mchimbaji; kwa siku ninatumia mafuta zaidi ya lita 1,400. Kuna rafiki zangu nje ya nchi wananiuliza wewe mitambo yako inaendelea na kazi? Ninawaambia mama mafuta yapo ya kutosha, kazi zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanapanga foleni hawaoni mafuta. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa suala la mafuta, nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimshukuru sana Makamu wa Rais ambaye muda wote ameendelea kumshauri Rais kufanya mambo yawe mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, kabla ya mchango wangu, ninamshukuru sana Mkuu wa Mkoa wangu kaka yangu Mheshimiwa Martin Shigela. Kwa kweli Rais alituletea mtu sahihi. Sisi Geita tunajivunia tuna Mkuu wa Mkoa tofauti na wengine, msimwombe Wabunge kuja kwenye mikoa yenu. Mama atuachie Geita bado tuna kazi naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mkuu wa Wilaya yangu Bura; kwa kweli muda wote amekuwa akinisaidia kazi zangu za kibunge, nikiwa sipo jimboni. Ninamshukuru sana kaka yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana vilevile Mkurugenzi wangu wa Wilaya ya Chato. Aaah! huyu bwana hapana, apewe maua yake. Sasa, ninawashukuru sana wananchi wema wa Chato Kusini. Watu wema, watu waungwana, watu hawa rahim sana, walikubali mimi niwe sauti yao humu ndani ya Bunge, walikubali mimi niwe mwakilishi wao. Ninajua wananisikia. Ndugu yangu Toyi mahali alipo, ndugu yangu Masamaki; hawa ni wapambanaji. Wamenishika mkono; ninaendelea kuwapongeza.

Nitakuwa nao na nitawatumikia katika siku zote za utumishi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kwa sababu ya muda ninaomba nianze kwa kuchangia sehemu kubwa tatu. Nianze na mifugo kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Wafugaji inaonekana leo kwenye hili Taifa sisi si watu wa kuzungumziwa mazuri. Shida ni nini? Wachangiaji wote wanalalamika tunavamia mashamba. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na naomba niulize, hawa wataalam wanaowasaidia Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wana mpango gani na sisi wafugaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani mpaka leo hawawezi kututafutia maeneo ambayo sisi wafugaji tutachunga bila kugombana na wakulima? Kweli inaingia akilini miaka 60 ya Uhuru? Mfano mdogo tu, Mheshimiwa Rais Samia, alipoingia madarakani aliwaambia watu wa madini, Waziri wa Madini yupo hapa, dhahabu haziwezi zikaliwa na simba; waachieni Watanzania wachimbe, leo tumeongeza uchumi wa Taifa mpaka 10% kwa sababu tumeruhusiwa kuchimba kwenye hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niwaulize watu wa Wizara ya Mifugo, wameshindwa kutengeneza mpango kwenye hili Taifa, wameshindwa kuja na wazo la kumshawishi, hata kulishawishi Bunge tukazibadilisha hizi sheria kwenye hizi *TFS* (haya mapori tu ambayo hata fisi hayana), wakatumegea sisi wafugaji vipande vipande, wakatupa masharti tusikate miti, tusiue swala, wameshindwa kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu sisi Watanzania nani ameturoga? Hawa wataalam wanawaza sisi wafugaji tupunguze mifugo; tukipunguza mifugo baadaye itazaliwa nini na wanajua sisi wasukuma hawa ng'ombe ndiyo tunatolea mahari na mwanamke anapokuwa mweupe ndiyo tunaongeza kutoa mahari ya ng'ombe nyingi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli hawaoni sababu ya kutuongezea kipato cha ng'ombe? Sasa leo tumalize ng'ombe zetu zote, watoto wetu wataolewa na nini? Ninataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana na nimefanya utafiti,

ndoa nyingi zinazovunjika ni wale waliopeana zawadi na mahari za fedha za ng'ombe hazivunjiki. *(Makofi/Vicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waje na mpango wataalam wasaidieni Waziri na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, ni watu wazuri, waje na mpango wa kutusaidia sisi wafugaji tusigombane na wakulima. Tupo tayari kuchangia pato la Taifa, hizi hela wanazolalamika, vyumba vya madarasa, wafugaji tuna ng'ombe unauza ng'ombe 10 unailipa Serikali, unakatiwa kitalu chako unachunga, unalinda mtu asikate mti, unalinda mtu asiue swala na lenyewe limekuwa shida mpaka profesa tu ndiyo wanamkubali? Aaah!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nichangie hotuba ya ndugu yangu Waziri Mkuu, nilikuwa sijaanza ndiyo naanza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimshukuru sana Waziri Mkuu, anafanya kazi nzuri, nimeona akizunguka kila mkoa. Hii kazi anayofanya ni kazi iliyotukuka. Ninataka nimwambie kwa namna anavyokwenda ndiyo namna tunayotaka Watanzania. Watanzania *story* na maneno tulishapigwa mno, nimwombe Waziri Mkuu, aendelee na *style* hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakubaliana na mimi, sisi Wasukuma tuna kilimo tunalima na ngoma moja inaitwa *bugobogobo*. Ninataka nimwambie Mheshimiwa Waziri Mkuu, hawa wasaidizi wake wasimfanye kuwa yeye ni ngoma ya *bugobogobo*. Ngoma hii unaweza ukapiga ngoma mwenyewe, ukacheza mwenyewe, ukalima mwenyewe, hapana! Awachezeshe kwata, akigeuka nao pia wageuke. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nirudie, wanaweza wakamfanya yeye kuwa na ngoma ya *bugobogobo*, anapotoka kwenye mkoa wanalala wote, akienda huku tena wanaamka. Awachezeshe zile kwato za kwenye harusi, hawa wasaidizi kuanzia mikoani na humu ndani, mpaka kule kwenye vijiji na kata, haiwezekani kesi ya mpaka nayo hadi aje Waziri Mkuu, kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu wanampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu yeye ni mzuri, nadhani anafananishwa na Sokoine, hawa watoto wa *Gen Z* wanamjua Sokoine? Aanze naye wamjue kwanza yeye, akiwachezesha ile ngoma ya kwato ninayoionaga kwenye harusi, akigeuka huku wanageuka nao, ukigeuka huku, halafu wewe utaangalia nani anakosea *style*, hiyo ndiyo kazi tuliyomwamini sisi Wabunge humu, tukampigia kura zote za ndiyo, tunataka afanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nikwambie ukweli, unajua ukweli hata Mtume Paulo aliusema kwa Wagalatia kwamba, mnaniona adui kwa kusema ukweli, hawa watu ukisema ukweli unaweza ukazoa uadui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimwambie Mungu wa Mbinguni atasimama na yeye na Mungu hatampunguzia na bahati nzuri ninataka nimwambie mimi ni mtoto wa mamantilie, nilikuwa ninaanza kuwaza kwa nini Waziri Mkuu anafanikiwa, kumbe pembeni yake kuna mamantilie, kwa kweli mamantilie wa Mwigulu naye apigiwe makofi jamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio haya…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. PASCAL L. LUTANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aaah! Namalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho; wananchi wangu wa Chato Kusini, Waziri Aweso, alituahidi maji kutoka Buzilayombo kuja Chato Kusini, hatujayaona na muda mwingi amekuwa akisema, wali wa kujaa unaonekana kwenye sahani. Rafiki yangu Mheshimiwa Aweso, wananchi wangu wa Chato Kusini, hata sahani hawajaiona, tunataka maji, tofauti na hapo maneno yake ya wali wa kushiba unaonekana kwenye sahani, Chato Kusini hatuelewi, tunataka maji, tunataka maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitakuwa Mbunge wa kulialia, ninataka nione matokeo, wananchi waliniamini, nitawapelekea maendeleo, ndiyo mzee wa mitambo ya greda, mimi kwangu hakuna kulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Pascal, kwa mchango wako.

Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, ajiandae Mheshimiwa Cornel Lucas Magembe.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa ninapenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunipa kibali. Kwa sababu toka Bunge la Kumi na Tatu limeanza leo ni mara yangu ya kwanza kusimama kuchangia. Kwa hiyo, ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu, bila yeye nisingekuwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikishukuru sana chama changu, Chama cha Mapinduzi, kikiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ni Mwenyekiti wetu kwa vikao vyote vilivyofanyika kututeua na kuniteua kuwa miongoni mwa wagombea na baadaye kuwa Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Rais, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Alitembea Tanzania nzima, akinadi Ilani ya Chama cha Mapinduzi, nini atakifanya. Pia, aliahidi ndani ya siku 100 kuna mambo manne ambayo atakwenda kuyafanya, katika yale mambo manne ambayo aliahidi kwamba atakwenda kuyafanya yamekwishaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni suala zima la kuwawezesha wananchi kiuchumi. Katika suala la kuwawezesha wananchi kiuchumi, mikopo ya 10% kwa mkoa wangu wa Shinyanga, tumefanya vizuri. Rais amefanya vizuri kwa sababu

alitoa maelekezo, alitoa ahadi na wale watendaji wa Mkoa wa Shinyanga wameyatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, dada yangu Mboni Mhita, lakini niwapongeze watendaji ambao ni Wakurugenzi wa Halmashauri zote zilizopo katika Mkoa wa Shinyanga pamoja na Wakuu wa Wilaya kwa kusimamia, kuhakikisha kwamba ule utekelezaji, ile ahadi ambayo Mheshimiwa Rais, aliahidi inatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninawapongeza? Kwa Mkoa wa Shinyanga mpaka kufikia Januari, 2026 tayari halmashauri zote kwa ujumla wake zimetoa mikopo ya shilingi bilioni 3.4. Siyo fedha ndogo lakini haitoshi kila halmashauri imejitahidi kutoa mikopo kwa makundi maalum. Wanawake wamekopeshwa shilingi bilioni moja, watu wenye ulemavu wamekopeshwa shilingi milioni 56, vijana wamekopeshwa zaidi ya shilingi milioni 985. Siyo jambo dogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya vikundi 269 vimekopeshwa. Kwa hiyo tunaona ni jinsi gani maono na mipango ya Mheshimiwa Rais inavyotekelezwa kwa wakati. Aliahidi na kweli ametekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na kukopesha, mbali na makundi haya kupata mikopo, lakini kuna changamoto. Mwanzoni hizi fedha zilikuwa zinakopeshwa moja kwa moja kutoka halmashauri, lakini sasa hivi kwa ile mikoa ambayo imepewa kipaumbele kuweka majaribio ya ukopeshaji kuna changamoto. Sasa hivi wanatumia mfumo, unakuta kuna kikundi ambacho toka mikopo imeanza kinakopa na kurejesha, lakini kinashindwa kuja kupata mkopo mwingine baada ya kuwa wamemaliza rejesho kwa sababu tu mfumo hauwasomi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwenye suala zima la mfumo kuna haja ya kuangalia ni kitu gani kifanyike kuweza kuboresha hii mifumo. Kuna changamoto nyingine, watu wengine vikundi vingine wanawake wanakosa mkopo kwa sababu tu kwenye kile kikundi kuna watu hawana *NIDA*, kosa ni la nani? Wameshajiandikisha, wameshasajili kwa ajili ya kupata *NIDA*, lakini

*NIDA* haipatikani, wanatumia muda mrefu, wakienda hata kuomba zile namba za *NIDA* sasa kwenye Ofisi za *NIDA* wanaambiwa mtandao haufanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wanakata tamaa, vijana wanakata tamaa, watu wenye ulemavu wanakata tamaa. Tunaomba Serikali, chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kuhakikisha kwamba, vile vigezo ambavyo vimewekwa visiwe na vikwazo vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kupata mikopo ambayo imepangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ulikuwa mchango wangu wa kwanza. Mchango wangu wa pili katika mambo ambayo Mheshimiwa Rais alisema atayatekeleza ni suala zima la bima ya afya kwa wote. Ni ukweli usiopingika mpango huu wananchi wameupokea kwa shangwe na nderemo. Tukiangalia Mheshimiwa Rais, toka ameahidi siku 100 tayari zaidi ya wanufaika 1,400 na zaidi wameweza kunufaika, sawa na kaya 276,000, siyo jambo dogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu wa bima kwa wote umepokelewa vizuri, niiombe Serikali kusimamia sasa upatikanaji wa dawa. Haipendezi mtu ana bima ya afya, anakwenda hospitali, anahudumiwa, anamwona daktari, anakwenda kwenye vipimo, inapofika kwenye suala la dawa anaambiwa hii dawa haipo nenda ukanunue, hii dawa siyo ya bima ya afya, lakini mtu akija na *cash* anapata ile dawa; haipendezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kumchonganisha Mheshimiwa Rais, ambaye amerahisisha huduma za afya kwa kuhakikisha kwamba Sheria ya Bima ya Afya inaanza kutumika Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaombe sana mamlaka ambazo zinahudumia, hasa kwenye ngazi ya afya ya msingi; kwenye vituo vya afya, kwenye zahanati na kwenye hospitali za wilaya ambazo zipo chini ya TAMISEMI, tuwaombe sana bima ya afya tunahamasisha kama Wabunge, tunatoa elimu ya afya, elimu kuhakikisha kwamba kila mtu anajiunga na bima ya afya kwa wote, itakapofika kwenye huduma basi apate huduma ambazo

amezitarajia, ambayo ni matamanio ya Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba watu wake wote wanatibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuweza kuwalipia watu wanaopata magonjwa yasiyoambukiza wasio na uwezo ikiwemo saratani, kisukari na magonjwa mengine ya mifupa. Siyo jambo dogo ni jambo kubwa na niwaombe Waheshimiwa Wabunge, sisi Wabunge tunatumia muda mwingi sana kukaa humu Bungeni, toka asubuhi tunakuja mpaka sasa hivi bado tupo tumekaa, tufanye mazoezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa yasiyoambukiza yanazuilika, ni wewe mwenyewe kuamua unataka uwe na kisukari, unataka uwe na magonjwa yasiyoambukiza mengine ni suala la kufanya mazoezi, ni suala la kuamua uishi vipi. Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge wote, tumeshaanza mazoezi karibuni kwenye mazoezi, mazoezi yanafanyika Jamhuri na viwanja vingine, ili tuweze kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, ninaunga mkono hoja, ni hotuba nzuri iliyosheheni matamanio ya Watanzania, ni hotuba nzuri inayokidhi matarajio ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuwatekelezea mahitaji yao Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Christina kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Cornel Lucas Magembe, ajiandae Mheshimiwa Jacqueline Chrisant Mzindakaya.

**MHE. CORNEL L. MAGEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii njema jioni ya leo ili niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika kujadili bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kama ilivyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, niungane na Watanzania wote kuendelea kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa namna ambavyo ameendelea kutujalia afya Watanzania wote wakiwemo viongozi wetu na kiongozi wetu mkuu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, niendelee kumwombea sana Mheshimiwa Rais aendelee kuongoza Taifa letu kwa busara hiyo aliyonayo, lakini akisaidiwa na Makamu wake wa Rais, akisaidiwa na Waziri wake Mkuu, lakini pia na Mawaziri wote pamoja na watendaji wote wa Serikali; kuanzia ngazi ya Taifa mpaka kwenye vijiji vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia, kuendelea kuwashukuru sana wananchi wa Chato Kaskazini. Wananchi hawa wa Chato Kaskazini ni watu wema sana, walinipigia kura kwa mahaba makubwa kwamba nije niwe mwakilishi wao katika Bunge lako Tukufu hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekuwa na mimi siku zote, toka uchaguzi umekwisha, tumekuja Bungeni tumeapishwa, wamekuwa na mimi katika changamoto zote ambazo Mbunge wao nimekuwa nikizipitia na mazuri yote na mema yote tumekuwa bega kwa bega nao. Ninawashukuru sana wananchi wa Chato Kaskazini kwa kuendelea kuniunga mkono na ahadi yangu kwao ni kwamba sitawaangusha katika uwakilishi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupo kwenye kuchangia hotuba ya Waziri. Katika hotuba ile ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, yapo mambo mengi na mazuri ambayo Serikali imeyaweka mbele yetu kuonesha ina mpango mzuri wa kwenda kutekeleza kwa ajili ya Watanzania. Pamoja na mipango ambayo imewekwa yapo mambo mazuri na makubwa ambayo yametengwa kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wananchi wa Chato Kaskazini, ninatumia nafasi hii kumshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali yake, lakini ikiwemo chama change, Chama cha Mapinduzi kwa

makubwa na mazuri na mengi yaliyoletwa kwa wananchi wa Chato katika kipindi cha miaka minne ya utangulizi wa utawala wake. Tunamshukuru sana sisi watu wa Chato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya yetu ya Chato, ipo miradi mingi ya kimkakati ambayo ililetwa, ambayo nikianza kuitaja hapa nadhani, muda hautatosha lakini itoshe kusema tu kwamba mabilioni ya fedha kwa ajili ya miradi, kwa ajili ya Watanzania waliopo Chato, kwa kweli sisi tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na fedha zile ambazo zimeletwa kwa wingi, nilitamani niseme mambo haya. Zipo fedha ambazo zimeletwa kwenye miradi mingi kwenye maeneo yetu, lakini inapokwenda kukamilika miradi ile haisimamiwi sawasawa kwa ajili ya kuleta tija ambayo ilikusudiwa na Serikali yetu. Kwa mfano, leo tukitembea kwenye miji mingi ikiwemo Mji wa Dodoma, Dar es Salaam, Mwanza na miji mingine, wako Wabunge wenzetu hapa wanaomba kujengewa stendi katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Chato ni moja ya mji ambao tulipata bahati ya kupata mradi mkubwa wa kujengewa stendi ya kisasa, kama zilivyo stendi nyingine kama Dodoma na kwingineko. Serikali ikifanya *intervention* ya kwenda kuona yale ambayo yanaendelea kwenye stendi zile utagundua kwamba fedha nyingi zimekwenda kule lakini tija iliyokusudiwa haiendi sawasawa kama ambavyo ilitarajiwa na Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ile stendi ukienda kuna maeneo mengine ambayo hayafanyi kazi kama ambavyo ilitarajiwa kwenda kutumika. Vilevile hata ukienda kwenye stendi yetu ya Chato ambayo imetengewa mabilioni ya fedha mpaka leo, haijakamilika katika ubora ambao unatakiwa na haifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, fedha zile zilizokwenda pale zinaishia huko bila kuleta matokeo yaliyokusudiwa. Kumbe, pengine tusingejenga ule mradi mkubwa unaoonekana sasa upo, ilhali umetumia fedha nyingi, lakini haufanyi kazi ipasavyo; badala yake, tungelielekeza fedha hizo katika kujenga vyoo kwenye shule

zetu ili watoto wetu wapate kusoma katika mazingira bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwenye hii miradi: nimemwona Mheshimiwa Waziri Mkuu amepita huko kwenye mikoa yetu, anapofika kwenye mikoa yetu na maeneo yetu, nimwombe sana aende akashughulike na miradi mikubwa ya kimkakati aone kama tija yake iliyokusudiwa inakwenda kufanya kazi, hilo ndilo lililokuwa ombi langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na miradi hiyo kwetu pale Chato kuna uwanja mkubwa wa ndege, ulitumia mabilioni ya fedha na uwanja ule ukaanza kutumika na wananchi wa kule Chato na maeneo mengine ya jirani mpaka na nchi za jirani, uwanja ule ulikuwa unatumika kwa ajili ya kusafirisha watu, lakini mpaka leo ninavyozungumza, mabilioni ya fedha yamepotea katika uwanja ule. Sasa umebaki kwenda kwa Wasukuma kwenda kuanika pale mihogo ili wapate udaga waende wakale chakula badala ya kuweka ndege pale. Sasa shida iko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninamwomba sana Waziri anayeshughulika na mambo ya usafirishaji na uchukuzi, wahakikishe kwamba Chato bado tunahitaji tupate ndege kwa sababu fedha ya Serikali ilikufa pale kwa kujenga kiwanja cha ndege katika eneo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka minne ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ziko bandari mbili ambazo zilijengwa kwa fedha kubwa zaidi ya shilingi 6,000,000,000, iko Bandari ya Nyamirembe, iko na bandari ya Bwina. Bandari hizo zilitarajiwa kwamba baada ya kukamilika, meli zingeanza kutia nanga katika maeneo hayo, wananchi wapate huduma ya usafiri na pia kuwezesha upatikanaji wa mizigo kutoka maeneo mbalimbali kwa ajili ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza miaka minne iliyopita ya bandari zile kuchukuliwa shilingi bilioni sita mpaka sasa hazitumiki na meli zipo kutoka Mwanza kwenda huko kwetu, lakini haziwezi kufika pale zinakwenda kwenye maeneo mengine. Kwa hiyo, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba

mahali ambapo Serikali imeamua kuwekeza fedha zake, basi fedha zile zikatutumike kama ambavyo zimekusudiwa kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ninaomba niishauri Serikali hasa wakati inapokuwa inatoa miradi kwa wakandarasi, ninaona wakandarasi ambao ni *private* wanaweza wakafanya vizuri kuliko wakandarasi ambao ni taasisi za Serikali. Nina mfano pale kwangu pale Chato, kuna mkandarasi ambaye alikuwa *National Housing* alikuwa amepewa kujenga shule... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. CORNEL L. MAGEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie tu hili, kwamba wako wakandarasi ambao wamepewa kujenga shule zetu, iko Shule ya Mbuye ya watoto wenye mahitaji maalum. Shule imejengwa kwa fedha nyingi lakini mpaka sasa haijakamilika na mkandarasi ameacha mradi amekwenda na ile shule inahitajika watu wasome pale na fedha zilipelekwa nyingi.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. CORNEL L. MAGEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sababu ya muda, ninaomba niseme ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Jacqueline Chrisant Mzindakaya na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Fadhili Ally Liwaka.

**MHE. JACQUELINE C. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza, kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunipata kibali cha kuwepo mahali hapa ikiwa ni mara yangu ya kwanza katika Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda vile vile, kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kwangu, lakini pia na Chama changu Cha Mapinduzi. Hata hivyo, kipekee ninaomba niwashukuru wapiga kura wangu wa Mkoa wa Rukwa (wanawake) walioweza kunipigia kura na kupata ushindi wa kishindo, ninawaahidi sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba niendelee kwa kumpongeza kwanza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo ameweza kuifanya na ambayo anaendelea kuifanya. Sote ni mashuhuda katika siku zake 100 yale aliyoahidi katika kampeni za uchaguzi na ameweza kuyatimiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niendelee kwa kumpongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, ambaye ameanza kwa kasi kubwa. Sisi Mkoa wa Rukwa amepita katika mkoa wetu, nami kwa niaba ya Mkoa wa Rukwa ninaomba nifikishe salamu za wakazi wa Mkoa wa Rukwa kwa kile ambacho umeweza kukifanya kwa kusikiliza na kutatua kero mbalimbali za wakazi wa Mkoa wa Rukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuendelea kufanya ziara hizo katika mikoa mingine, hakika Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hakukosea kupendekeza jina lake na Waheshimiwa Wabunge hatukukosea kumpa kura za kishindo Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, ninawapongeza sana, lakini nimtakie Mheshimiwa Waziri Mkuu kila la heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na hapo, nitakwenda kupeleka mchango wangu katika maeneo mawili na maeneo hayo nitagusa eneo la afya; lakini vilevile nitagusa eneo la kilimo kwa kutambua mchango wa mkubwa wa Serikali yetu katika afya kwa kuboresha huduma ya mama na mtoto katika wodi ya wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Rukwa umeweza kupunguza vifo vya mama wajawazito kutoka vifo 128 katika vizazi hai 100,000 hadi kufikia vifo 60 katika vizazi hai 100,000. Vifo vya

watoto wachanga vilevile katika Mkoa wetu wa Rukwa vimeweza kupungua kutoka vifo 11 katika vizazi hai 1,000 hadi kufikia vifo saba katika vizazi hai 1,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni mapinduzi makubwa na hii yote inatokana na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mchango wake mkubwa na tumeona alipatiwa tuzo ya kitaifa kupitia *Gate Foundation* ambayo ni *The Gate Goal Keeper Award* ambayo aliipata mwaka jana 2025, lakini hivi juzi tumeona mwezi Februari alipokuwa Addis Ababa ametunukiwa kuwa kinara wa kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto wachanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, tunatambua pia mchango mkubwa wa Serikali katika Mkoa wa Rukwa katika sekta ya afya ambapo tumeweza kujengewa hospitali za wilaya nne na vituo vya afya 39 na zahanati 219. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hospitali hizo za wilaya, kuna Hospitali ya Wilaya ya Kalambo ambayo Serikali ilielekeza shilingi bilioni nne katika ujenzi wa hospitali hiyo ya Wilaya ya Kalambo. Hospitali hiyo ya Kalambo ina changamoto ya wahudumu wa afya ama watumishi wa afya kwa 70%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ninaomba Serikali sikivu katika dira ya maendeleo ili kupitia TAMISEMI waweze kulisimamia hilo na wahudumu hao au watumishi hawa wa afya waweze kuongezwa: hususan, madaktari wa upasuaji wa wanawake wajawazito, ambao katika kutimiza azma na dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kupunguza vifo ya wanawake wajawazito na watoto tutakwenda kwa kiasi kikubwa kusaidia kwa kupeleka madaktari hao wa upasuaji wa wanawake wajawazito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ninaomba nizungumzie Kituo cha Afya cha Kasu: Kituo hicho cha Afya cha Kasu, tumeona kimetengewa shilingi bilioni 1.3 katika ujenzi na Serikali na kinatoa huduma zote za afya ikiwepo huduma ya wodi ya mama na mtoto, *OPD,* vifaa tiba na kadhalika. Kituo hicho kina

changamoto kubwa ya barabara na Mbunge wa Nkasi Kusini, kaka yangu jana alizungumzia hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru kipekee Mheshimiwa Waziri Mkuu katika ziara yake alielekeza barabara hiyo kupitia *TARURA* watupatie shilingi milioni 500 ili barabara hiyo iaanze kujengwa na kusababisha wananchi wa Nkasi na eneo la Kasu kupata urahisi wa kufika katika kituo hicho cha afya na kupatiwa matibabu na kuimarisha ustawi mzima wa afya ya Wanankasi na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba nijikite katika sekta ya kilimo, Mkoa wetu wa Rukwa uti wa mgongo wa uchumi wetu ni kilimo. Hata hivyo, tunaishukuru Serikali kwa kuendelea kusaidia programu mbalimbali za maendeleo ya kilimo ikiwepo skimu za umwagiliaji sita ambazo zimejengwa katika Mkoa wa Rukwa. Vilevile, kwa Serikali kuendelea kununua mazao kupitia Wakala wa Hifadhi ya Mazao wa Taifa *(NFRA)*. Pia tunaishukuru Serikali kwa kuendelea kutoa ruzuku kwa pembejeo za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu: ninaomba Serikali ituangalie kwenye suala la ulipaji wa *NFRA* kwa mazao hayo ambayo wamenunua kwa wakulima waweze kuwalipa kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba pia kiwango cha ununuzi wa mazao kutoka kwa wakulima kiongezwe; kwa sababu uzalishaji ni mkubwa sana, lakini kiasi cha mazao kinachonunuliwa hakikidhi, hivyo wakulima kubaki na mazao mengine bila soko. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iliangalie hilo katika mipango ya dira ijayo, ili kubaini namna bora ya kuongeza ununuzi wa mazao kutoka kwa wakulima wa Mkoa wa Rukwa, waweze kujikwamua kiuchumi, kwa kuwa sisi Rukwa tunategemea kilimo kama uti wetu wa mgongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, tunaomba pia kupitia skimu za uwagiliaji ziweze kuongezwa ili tuwe na kilimo endelevu tusitegemee tu msimu wa kilimo ili vijana wa Mkoa wa

Rukwa na wanawake wa Mkoa wa Rukwa wazidi kujiajiri katika kilimo hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba pia kwa mfano, kuhusu Skimu ya Umwagiliaji ya Katongoro ambayo Serikali ili elekeza shilingi bilioni 60. Tunaomba skimu hiyo ya umwagiliaji ambayo ilianza toka mwaka 2023 mpaka leo haijakamilika. Hivyo, tunaomba Serikali itusaidie ili skimu hiyo ya uwagiliaji ya Katongoro iliyopo katika Wilaya ya Nkasi, ikamilike na wakazi wa Mkoa wa Rukwa waweze kujiajiri na kujinyanyua kiuchumi kupitia kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja kwa 100%, lakini vilevile ninasema katika falsafa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kazi na utu, tunasonga mbele, tuendelee kupiga kazi na kuthamini utu wa Mtanzania, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Jacqueline, kwa mchango wako, nilimtaja Mheshimiwa Fadhili Ally Liwaka, ndiyo atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo.

**MHE. FADHILI A. LIWAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninaungana na waja wema kumshukuru sana Mwenyezi Mungu wingi wa rehema kwa kutujalia baraka ya uzima na afya na hatimaye kuweza kuwa kwenye jengo hili Tukufu kwa ajili ya kujadili mustakabali wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia niungane na wenzangu kuwa sehemu ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye amewasilisha hapa Bungeni. Kwa kuanza kabisa ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uwasilishaji na mpangilio wa vipaumbele vya kitaifa ambavyo yeye kama msimamizi wa shughuli za Serikali hapa Bungeni na msimamizi wa shughuli za Serikali nchini ametenda haki inayotosha kabisa kutupa matumaini kwamba tunakwenda kupata matokeo chanya kutokana na hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwanza moja kati ya hotuba yake wakati tukipitisha jina

lake kwenye Bunge hili, alipokuwa anawasilisha salamu zake za awali za shukrani na mwelekeo wa namna atakavyomsaidia Mheshimiwa Rais kazi, aliweka wazi hotuba iliyoakisi huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limekwenda kujionesha pasi na mashaka yoyote alipokuwa akifanya ziara zake nchini kwa kuyafikia matatizo ya watu pengine na kuyatatua kabisa kwa wakati muafaka na kuleta matumaini mapya. Hii ni dira njema na huu ni mwelekeo ambao sisi tunaufurahia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika hotuba yako ume-*quote* vizuri kabisa Kitabu cha Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere cha Mwaka 1974 kinachoitwa, Mtu na Maendeleo, katika nukuu ya kitabu hiki kinasema: *"Maendeleo ya kweli huanza pale wananchi wanapoanza kuzalisha chakula cha kuwatosha wenyewe"*, msingi wangu katika kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kuona umuhimu wa sekta ya uzalishaji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeweka kipaumbele na msisitizo mkubwa sana wa kuongeza uzalishaji kupitia ongezeko la mbolea na ruzuku zinazotolewa katika pembejeo mbalimbali za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwenye hotuba imeweka wazi kabisa jumla ya tani 1,000,000 za mbolea zimetolewa na kupelekwa kwa wananchi na jumla ya wakulima zaidi ya 500,000 wamenufaika kwa fedha za kitanzania shilingi trilioni moja, hii ni ishara tosha kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametazama sekta ya uzalishaji kama ndiyo kichocheo muhimu kitakachotuvusha na kutupa uchumi wa uhakika nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunajua Serikali haiwezi kuchoka kuhudumia, Serikali haiwezi kuchoka kutengeneza matajiri na Serikali yetu haiwezi kuchoka kutengeneza uzalishaji wenye tija utakaotoa matokeo ndani na nje ya nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri kwenye maeneo mawili kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, moja...

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Zuberi Mfaume.

**TAARIFA**

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kama Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni vema tukakinukuu kwa usahihi Kitabu cha Mwalimu Nyerere hakuna kitabu cha Mtu na Maendeleo bali ni Binadamu na Maendeleo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fadhili Liwaka, unapokea, taarifa hiyo?

**MHE. FADHILI A. LIWAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea. Ninashukuru kwa masahihisho hayo mazuri na nukuu yetu iko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mchango kwenye maeneo mawili, eneo la kwanza, ili tuweze kuboresha na kuhakikisha uzalishaji wa watu wetu unakuwa stahimilivu ni muhimu tukatazama eneo la wanyama waharibifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niweke *record* yangu vizuri kabisa Tanzania inielewe, Afrika inielewe na dunia inielewe. Mimi sina shaka na rasilimali za wanyama pori hususani ndovu walioko nchini. Kwanza, ninaipongeza Serikali yangu kwa kuweza kupambana na ujangili na kuweza kusaidia ongezo la wanyama hawa wenye thamani kubwa dunia, ninatoa pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ni mmoja kati ya mabalozi wazuri wanaotaka wanyama hawa walindwe, lakini utakubaliana nami hata mwili wa binadamu ukiongezeka uzito ni sumu. Hivyo, basi wanyama hawa sambamba na jitihada kubwa na ninamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu alijibu swali la papo kwa papo kwa usahihi kabisa kwa kulinganisha kwamba wanyama

hawa wanaingia kwenye sura ya mikataba ya kimataifa, lakini sisi kama nchi tunaomba jitihada ziongezeke katika kuhakikisha kwamba wakulima wetu wanabaki salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoka Jimbo la Nachingwea, Jimbo la Nachingwea pekee yake takwimu za uzalishaji mwaka 2023/2024 tulizalisha tani 140,535, mwaka 2024/2026 tumezalisha tani 103,470 kuna upungufu wa tani 37,065.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini, kuna upungufu huu? Kwa sababu wakulima moja, wameacha kulima kwa kiwango kikubwa kwa kuhofia ndovu waliopo kwenye maeneo yetu. Wameacha kuweka jitihada kwa sababu hata wakiweka kwa ekari nyingi bado wanyama waharibifu wanakwenda kuharibu mazao yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali itazame nyongeza ya jitihada za kuhudumia maeneo haya: moja, waongeze hizi ndege nyuki kazi nzuri inafanyika; pili, kuongeza vituo vya askari wa wanyama pori; na tatu, elimu iendelee kutolewa wakati tunaangalia njia bora za kiteknolojia ya dunia ya sasa katika kukabiliana na hawa wanyama (ndovu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwenye eneo hili, ni kuomba fidia kwa wakulima waliopata madhara. Serikali imefanya kazi kubwa wanatoa fidia, lakini bado fidia hii haiwezi kuwafikia wote. Hivyo tunaomba usimamizi na *speed* katika kulipeleka jambo hili ili wananchi wetu waweze kupata manufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili pia la uzalishaji tuna jambo la migogoro ya wakulima na wafugaji: ninaomba Serikali ilichukue jambo hili kwa uzito mkubwa na bahati nzuri sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mbobezi katika eneo hili la utatuzi wa migogoro ya wakulima na wafugaji, alifanya hivyo kwa miaka iliyopita na sasa ninaamini anao uwezo wa kusimamia sekta zilizopo ili tatizo hili liishe. Tusiwe na jambo la uadui kati ya wakulima na wafugaji bali tuwe na maelewano na uzalishaji unaofaa sambamba na jitihada ambazo zinafanywa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nimalize mchango wangu kwa jambo moja na hapa niruhusu tu nizungumze kwa rika yangu ya ujana. Sisi vijana tuliolelewa kwenye misingi ya Chama cha Mapinduzi ambao tuko ndani ya Bunge na tuko nje ya Bunge huwezi kutushauri chochote juu ya kumpigania, kumsemea na kumsimamia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nikuhakikishie kwa umri wangu nimeanza kuipenda siasa mwaka 2005 wakati Rais wa kwanza akiwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, nilimsemea, nilimpigania na nilikuwa *form two* na alivuka salama hiyo ni kazi ya kijana wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015 aliingia Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, nilikuwa Mjumbe wa *NEC* nilimsemea, nilimpigania, nilimwombea kura mpaka Mungu alipoamua, bado nilikuwa ninamsemea kwa nguvu kubwa na nina ujasiri wa kusimama mbele ya Bunge lako bila uwoga wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2021 akaingia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye tunaye mpaka sasa, ninataka nikuhakikishie tutamsemea, tutamsimamia, tutamshauri. Hatutaogopeshwa na majina yanayoitwa mara chawa au tunaitwa majina ya kujipendekeza, huu ni wajibu wa msingi kwa kijana aliyepata malezi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalize kwa kusema jukumu hili hatujipi ili tulipwe, jukumu hili tunajipa kwa sababu tunamtaka Mama Mheshimiwa Dkt. Samia tunapomsemea na kumtia moyo akajenge mabweni ya watoto wetu wasitembee umbali mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tunapomsemea Mheshimiwa Dkt. Samia akawatue mama zetu ndoo kichwani watembee na maji kwenye ndoo kutoka jikoni kwenda kuyaweka ndani. Tunapomsemea na kumlinda Rais wetu hatutaki malipo tunataka Mama huyu aimarishe diplomasia ya uchumi watu wa Mataifa waendelee kumwamini na nchi yetu izidi kupata heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, ninakushukuru sana kwa nafasi na Mungu awabariki. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri.

Waheshimiwa Wabunge, tumehitimisha shughuli za leo katika Kikao chetu cha Sita, Mkutano wa Tatu. Hivyo, ninaahirisha Shughuli za Bunge hadi Siku ya Jumatatu, tarehe 13 Aprili, 2026 saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.43 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 13 Aprili, 2026, Saa Tatu Asubuhi)*

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA